epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US

# Nipashe

Ijumaa Julai 26, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581749

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



UKURASA 22

**DE GEA AFIKIRIA OFA TATU KUREJEA KWENYE SOKA**



# Dawa za pumu, fangasi zatumika kujichubua ngozi

• **Maprofesa** wabaini tatizo; madhara kuanzia nje hadi ndani ya mwili yaanikwa... *Endelea ukurasa 2*

UKURASA WA 21

## MAN UNITED YATAFUTA BEKI MPYA



KLABU ya Manchester United imeongeza kasi ya kutafuta mlinzi mpya wa pembeni, chanzo kiliiambia ESPN, huku Tyrell



## Abiria 1,000 treni ya SGR wasafiri Dar- Dom, wengi wakosa nafasi

UKURASA 3



Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan akiweka silaha za asili mkuki na ngao kwenye mnara wa mashujaa, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kumbukumbu ya Mashujaa, jijini Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

UKURASA WA 19

**Kamala** Harris akwaa mtihani mzito vita Gaza



UKURASA WA 19

**Mwalimu** jela miaka 20 kisa kuingiliwa na mwanafunzi

UKURASA WA 19

**Walimu**, wanafunzi kortini mashtaka ya wizi mitihani

# ACT yalia magari ya serikali kutafuna mabilioni ya bajeti

UK.2

**MICHEZO** **GOLIKIPA AWATOA HOFU MASHABIKI SIMBA** UK.24 **KATUNI** UK.6

# ACT walia magari ya serikali kutafuna mabilioni ya bajeti

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha ACT Wazalendo kimesema matumizi ya serikali, hasa katika ununuzi wa magari na kugharamia mafuta na matengenezo yake, vinaongeza ugumu wa maisha kwa wananchi.

Viongozi wakuu wa chama hicho wamesema wanaumia kuona wakati wananchi wakiteswa na umaskini mijini na vijijini na kujifunga mikanda kiuchumi kukabiliana na kupanda kwa bei za bidhaa na huduma, serikali imeendelea na matumizi yasiyo na tija huku ukaguzi ukibaini kuwapo upigaji fedha za umma.

Walilalamikia hayo jana katika mikutano ya hadhara iliyofanyika mikoa ya Simiyu, Dodoma, Kigoma na Ruvuma.

Kwa mujibu wa taarifa iliyowasilishwa na Wizara ya Fedha bungeni mwaka 2022, serikali ilikuwa na magari 15,742, pikipiki 14,047 na mitambo 373 huku ikitumia zaidi ya Sh. bilioni 500 kila mwaka kwa ajili ya ununuzi wa magari mapya, mafuta, vipuri na matengenezo.

Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba aliarifu Bunge kuwa serikali ina mpango wa kupunguza matumizi katika eneo hilo kwa kuwakopesha fedha za kununua magari watumishi wa umma badala ya kutumia magari ya serikali.

Kiongozi wa Chama hicho, Dorothy Semu, akiwa wilayani Bahi, mkoani Dodoma jana alisema, "Tunashuhudia ubadhirifu na upotevu mkubwa wa fedha unaofanywa na watendaji wa serikali. Mwaka huu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG - ripoti ya 2022/23) ameonesha fedha zilizo hatarini kupotea kutokana na vitendo vya ubadhirifu ni Sh. trilioni 3.4.

"Hakuna aliyewajibishwa. Wakati huohuo viongozi wanaendelea kufanya matumizi ya anasa kwa kujinunulia magari ya kifahari, kujiongeza posho, safari za nje na mishahara. Kwenye bajeti ya mwaka huu, katika kila Sh. 1,000 itakayokusanywa wamejipangia Sh. 700 ni kwa matumizi yao."

Doroth alilalamika kuwa serikali inatumia fedha nyingi kununua mafuta ya petroli na diseli kwa ajili ya magari yake, akisisitiza kuwa upo uwezekano wa kupunguza matumizi hayo kwa kutumia nishati ya gesi asilia iliyopo nchini.

Alisema gesi asilia ingelisaidia taifa kupunguza nauli za mabasi na usafiri na kuongeza ajira, hivyo kupunguza ugumu wa maisha kwa wananchi.

Makamu Mwenyekiti wa ACT Wazalendo Tanzania Bara, Isihaka Mchinjita, akiwa Peramiho, mkoani Ruvuma jana, alisema ubadhirifu unaongeza mzigo kwa wananchi. Fedha zinazotengwa haziendi kushughulikia matatizo ya msingi ya wananchi. Ndio maana serikali imekuwa na madeni makubwa.

"Wote tunaona hali ilivyokuwa ngumu. Ninataka niwaambie wana Peramiho na Watanzania wote, ACT Wazalendo tumedhamiria kuifikisha mwisho hali hii. Wajibu wenu ni kuikataa CCM na kuichagua ACT Wazalendo.

"Tutahakikisha tunaondosha hali hii kwa kuilinda kila senti ya fedha zenu zinazokusanywa kutokana na jasho lenu inatumika kujenga taifa la wote kwa maslahi ya wote," alisema Makamu Mwenyekiti.

Ado Shaibu, Katibu Mkuu wa chama hicho, akiwa Busega, mkoani Simiyu jana, alisema ugumu wa maisha umeongezwa na ukopaji wa serikali, akisisitiza kuwa athari kubwa za ukopaji holela zinaangukia kwenye mabega ya wananchi walalahoi.

"Wananchi wanaongezewa kodi, ushuru na makato katika huduma muhimu kama vile ushuru kwenye mazao ya kilimo ili kulipa madeni haya.

"Wakulima, wachimbaji wadogo, wafanyabisahara na wafanyakazi wote wanalia utitiri wa kodi, ushuru na tozo. Serikali inawakamua wananchi wake kulipa madeni ambayo hawakunufaika nayo.

"Serikali inatumia sehemu kubwa ya fedha zetu kwenda kuhudumia deni badala ya kutoa huduma kwa wananchi walio wengi. Kila Sh. 1,000 tutayokusanya, Sh. 370 inakwenda kulipa deni," alisema.

Kiongozi mstaafu wa chama hicho, Zitto Kabwe, akiwa Jimbo la Kigoma Kaskazini, alisema sera alizodai "mbovu" za uchumi wa nchi zimesababisha serikali kushindwa kuongeza tija katika kilimo, uwekezaji na matumizi ya rasilimali za nchi kuondoa umaskini.

"Kwa sasa gharama za maisha ni tatizo kuu kwa Watanzania, wananchi wamechoshwa na umaskini wanataka mabadiko. Tunaelewa mzigo wa gharama kubwa za maisha na tunaahidi kuanzisha sera zinazodhibiti mfumuko wa bei na kupunguza bei za bidhaa na huduma muhimu," alisema.

Viongozi wakuu wa ACT Wazalendo wanaendelea na ziara ya kuzunguka majimbo yote Tanzania Bara, awamu ya kwanza ikihusisha majimbo 125.

Jana walikuwa majimbo ya Bahi, Maswa, Itilima, Kigoma Kaskazini na Peramiho. Na leo wataendelea na ziara katika majimbo ya Buhigwe, Rorya, Tarime Mjini, Manyoni, Buyungu na Songea Mjini.



Baadhi ya wafanyabiashara wadogo wakiwa wamepanga bidhaa zao katika barabara ya Morogoro, eneo la Kimara Temboni, Manispaa ya Ubungo Dar es Salaam jana, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama wao. **PICHA: BEATRICE MOSES**

# Dawa za pumu, fangasi zatumika kujichubua

**Na Christina Mwakangale**

DAWA za pumu ya ngozi na fangasi zinatumiwa na baadhi ya watu kujichubua ngozi, mamlaka za serikali zimeonya ni hatari kiafya.

Mamlaka hizo pia zimeeleza kukabiliwa na changamoto katika kudhibiti uuzwaji, usafirishaji na uingiaji dawa kiholela na vipodozi haramu nchini kutokana na biashara hiyo kufanywa kinyemela.

Ofisa Udhibiti Ubora katika Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Athumani Kissumo, anasema vipodozi vina tafsiri yake kama ilivyo katika Sheria ya Viwango iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2019 baada ya baadhi ya majukumu ya Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (TMDA) kuhamishiwa TBS.

Anasema vipodozi vyenye madhara vilivyopigwa marufuku nchini, vimeendelea kuingizwa, kuuzwa na kutumiwa kinyume na sheria kutokana na kuingizwa kwa njia za panya kama vile bandari bubu na magari ya malori ya mafuta kutumika kuvisafirisha.

"Kipodozi ni kitu chochote kinachotumiwa kupaka, kujipulizia, kujifukiza na kujimiminia kwenye mwili kwa lengo la kujipamba, kujisafisha na kubadili mwonekano na bila kuathiri mwonekano wa asili.

"Vipodozi havikisudii kutibu magonjwa wala kubadilisha maumbile ya mwili. Lengo la kipodozi ni kujiremba na kusihusishwe na kubadili maumbile au kuzuia magonjwa, hii ndio dhana kisheria,," anasema Kissumo.

Anasema vipodozi hivyo huwa na viwango kulingana na mtumiaji atakavyo na kwamba vipodozi ambavyo vinalenga kutibu au kubadili maumbile vinabadili tafsiri ya kipodozi na kuwa dawa.

"Shirika linahakikisha vipodozi vinadhibitiwa, viwango kwa mujibu wa makubaliano ya kimataifa, kikanda na mashirika mengine.

"Lakini, utakuta tu kipodozi tayari kipo sokoni. Hivi karibuni tulisikia kuna gari lilipita la mafuta ila ndani yake vimebebwa vipodozi," anasema.

Meneja Ukaguzi na Udhibiti wa Dawa kutoka Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania (TMDA), Emmanuel Alphonce anasema mtu akipata athari kutokana na matumizi ya kipodozi, hushirikiana na TBS kubaini aina ya bidhaa hiyo sokoni.

"Tukibaini tatizo huwa tunasimamisha matumizi na tunatoa taarifa kwenye vyombo vya habari kuufahamisha umma. Athari nyingi katika dawa ni ambazo zimeainishwa kisayansi kwamba ukitumia dawa hii utapata usumbufu fulani.

"Elimu kwa umma ni muhimu, wapo wanaotumia dawa za pumu ya ngozi na fangasi ili kung'arisha ngozi," alisema Alphonce.

Ofisa Viwango Mwandamizi TBS, Alexander Mashalla anasema utaratibu wa kupokea malalamiko kuhusu bidhaa zilizowaathiri watumiaji huwasilishwa kwa njia tofauti, ili hatua zichukuliwe.

Ofisa Lishe kutoka Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania (TFNC), Glory David, anasema uzito uliokithiri huwaathiri watu walio na mafuta mengi mwilini kulinganishwa na umri, jinsi na kimo.

"Pamoja na matumizi na dawa za kupunguza uzito, kuna vitu vya kuzingatia kwa ushauri wa daktari na mtindo wa maisha. Unaweza ukapunguza uzito kwa dawa kwa njia ya dawa hizo ila baadaye ukarudia hali ya awali," anahadharisha Glory.

Daktari wa binadamu, Fredrick Mashili, anasema vipodozi ni bidhaa zinazochangia kubadili ngozi na kuwa nyeupe zikiwa na 'steroids' na kuifanyia ngozi kuwa nyeupe, ndizo zinashika kasi na kuharibu mfumo wa homoni mwilini.

"Mtu anapoanza kutumia vipodozi hivi anasababisha mwili wake ushindwe kutengeneza homoni. Steroids ni homoni ambazo zinahusika kuweka uwiano wa mwili wake usiongezeke sana.

"Na wanawake kwa kiasi kikubwa hupasuka ngozi, hii hutokana na matumizi haramu ya steroids," anaonya.

Mkuu wa Kitivo cha Famasia Chuo Kikuu cha Kimataifa Kampala (KIU), Prof. Wilbroad Kalala, anasema katika utafiti waliofanya kuhusu vipodozi hadi hatua ya ngozi kung'aa, walibaini, steroids zilizomo katika vipodozi hivyo ni viambata vinavyofanya ngozi kuwa nyembamba na kuhatarisha afya.

"Dhana zilizopo katika jamii ni kwamba mwanamke mweupe ndio mrembo, zimefanya wanawake baadhi kuanza kutumia vipodozi ambavyo vina athari katika uzazi," anaonya Prof. Kalala.

Anaongeza: "Mtu anayetumia kipodozi hatarishi, akipata ajali ni ngumu kumshona kwa sababu vipodozi hivi huingilia 'melanin' ya ngozi isifanye kazi kiasili."

HABARI KITAIFA

# Abiria 1,000 treni ya SGR wasafiri Dar- Dodoma, wengi wakosa nafasi

**Na Mwandishi Wetu**

SAFARI ya kwanza ya treni ya kisasa (SGR) kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma, ilianza rasmi jana kwa takriban abiria 1,000 huku maelfu ya watu wakijitokeza na wengi kukosa nafasi baada ya mabehewa yaliyoandaliwa kujaa.

Safari hiyo ilianza katika kituo kikuu cha Dar es Salaam saa 11:19 alfajiri huku Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), Masanja Kadogosa, akiwaambia waandishi wa habari kwamba mabehewa 14 yaliandaliwa lakini kutokana na mwitikio wa abiria kuwa mkubwa, wengi walikosa nafasi.

“Kwa jumla walijitokeza abiria wengi jambo ambalo hatukulitarajia kwamba kungekuwa na mwitikio kama huu. Hakuna hata siti (kiti) iliyosalia katika mabehewa ya madaraja yote. Hata tungefunga mabehewa 20 kwa ajili ya safari hii ya kwanza kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma, ni dhahiri kwamba yangejaa kutokana na hamu ya Watanzania wengi kutumia usafiri huu ambao kwa kweli unaokoa muda,” alisema Kadogosa.

“Tunamshukuru Mungu safari ya kwanza tumeianza leo Julai 25 kama ilivyokuwa imepangwa. Tumesafiri na baadhi ya viongozi wakiwamo wakurugenzi, wabunge na baadhi ya wajumbe wa bodi kwa kutumia usafiri huu,” aliongeza.

Pamoja na kuanza kwa safari hiyo, alisema wanamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa juhudi zake kubwa kwa kuwaulizza kila hatua pamoja na changamoto walizokuwa wanakabiliana nazo katika kuanza safari hiyo. Alisema Rais pia alikuwa anawauliza mara kwa mara nini wanahitaji ili mradi safari hiyo ianze.

Licha ya kuanza kwa safari hiyo, Kadogosa alisema usafiri huo utazinduliwa rasmi na Rais Samia ndani ya wiki mbili kuanzia sasa.

Akizungumza baada ya kufika Dodoma baada ya kuwasili kwa treni hiyo saa 4:00 asubuhi, Kadogosa alisema treni hiyo ingefika mapema zaidi lakini walisimama kwa muda njiani kwa ajili ya kupisha treni iliyotoka Dodoma.

“Lakini kadiri siku zinavyokwenda tutaendelea kuboresha changamoto ambazo zimejitokeza leo (jana) kama ilivyokuwa wakati tulipoanza safari za Dar es Salaam hadi Morogoro,” alisema.

Kuhusu mwitikio wa abiria kutumia usafiri huo, Kadogosa alisema ni mkubwa hali ambayo inawapa kazi ya kufanya ili kukidhi mahitaji.

“Leo treni ya asubuhi tayari imejaa ya jioni na ya kesho pia imejaa, hivyo tutaendelea kuangalia mwenendo utakavyokuwa ili kuongeza safari kama ilivyokuwa katika safari za Dar- Morogoro” alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (LATRA), Habibu Suluo, aliishukuru serikali kwa kufanikisha safari ya kwanza ya treni ya SGR kutoka Dar es Saalam kuja Dodoma.

“Maono ya Rais wetu yametimia leo (jana). Tumepokea kwa mara ya kwanza treni ya umeme kutoka Dar es Saalam. Nitumie fursa hii niwaombe Watanzania tutunze miundombinu hii ambayo serikali imewekeza kiasi kikubwa cha fedha kufanikisha mradi huu wa kimkakati,” alisema.

**KAULI YA ABIRIA**

Baadhi ya abiria, akiwamo Rose Mchau, mkazi wa Dar es Salaam, walionyesha furaha kwa kutumia aina hiyo ya usafiri ambayo inatumia muda mfupi kulinganisha na aina zingine za usafiri wa nchi kavu.

“Kwanza nimevutiwa sana na kutumia saa chache ya kusafiri. Pili, nimependa mazingira ni masafi sana kama tuko airport (uwanja wa ndege), hivyo nitawahimiza watu wa Dodoma ambako kwa sasa nafanya kazi, waje kwa wingi kutumia usafiri huu kwa kuwa si uzushi kama tulivyojua awali,” alisema.

Mohamed Makongoro, mkazi wa Tabata ambaye amepata tenda ya shughuli zake za uchukuaji picha, alisema ameona atumie usafiri huo ili kuendana na muda kuliko kutumia usafiri wa basi.

“Tumpe hongera sana Mama (Rais) kutukamilishia usafiri huu. Nimefurahi sana kwani usafiri huu umekuja kuimarisha uchumi kwa sisi watu wenye uchumi wa chini na kati tutafanya biashara na mambo yetu kwa wakati” alisema

Amina Hassan alisema usafiri huo wa treni ya kisasa utakuwa mkombozi kwa makundi yote kutokana na kuokoa muda wa safari tofauti na ilivyokuwa kwa usafiri mwingine.

**• Imeandikwa na Pilly Kigome (DAR) na Paul Mabeja, DODOMA.**


KILOMBERO
SUGAR COMPANY

ZABUNI . 7/2024 **MNADA WA MALI MBALIMBALI ZA KAMPUNI YA SUKARI KILOMBERO**

| AINA A | KIASI |
|---|---|
| TREKTA | 7 |
| MALORI | 4 |
| LDV'S | 8 |
| VIFAA VIZITO | 1 |
| PAMPU ZA MKONONI ZA UMWAGILIAJI | 10 |
| TRELA | 7 |
| **AINA B** | |
| MAGARI | 18 |
| **AINA C** | |
| IMPLIMENTS | 7 |
| MASHINE NYINGINE NDOGO | 18 |

Kampuni ya Sukari Kilombero, inayoongoza kwa uzalishaji wa sukari Nchini kwa ushirikiano na Illovo Distillers (T) sasa inawaalika wazabuni kuwasilisha zabuni zilizofungwa ili kuondoa mali za kampuni.
Mali hizo zitauzwa kwa njia ya zabuni ya wazi katika viwanja vya kampuni hiyo vilivyopo Kidatu, mkoani Morogoro.

1. Wazabuni wenye vigezo wanaweza kupata maelezo na kukabidhi Zabuni zao katika ofisi ya Meneja wa Ununuzi na Mali, Ofisi Kuu ya K1 iliyoko Kilombero, P.O. Box 50 Kidatu, Morogoro kuanzia saa 9.00 asubuhi hadi saa 4.00 jioni kwa siku za Jumatatu hadi Ijumaa isipokuwa siku za sikukuu.

2. Wazabuni wanaalikwa kukagua mali zitakazouzwa katika mnada wa kampuni hiyo iliyopo Kidatu, Morogoro kuanzia saa 2:00 hadi saa 4:30 usiku kwa saa za ndani kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa isipokuwa siku za mapumziko kwa muda wa wiki mbili kuanzia tarehe ya kuonekana kwa tangazo hili.

3. Seti kamili ya hati za zabuni na seti za ziada zinaweza kununuliwa na wazabuni wanaovutiwa kwa kuwasilisha maombi yaliyoandikwa kwa anwani iliyotolewa katika aya ya 1 hapo juu baada ya malipo ya ada isiyoweza kurejeshwa kulingana na kitengo maalum wanachoshiriki., Ambayo ni
   ***TZS 50,000 (Kundi A),***
   ***TZS 30,000 (kundi B);***
   ***TZS 10,000 (Kundi C).***
   Zingatia: Kiasi kisichorudishika kitalipia bidhaa zote zilizoonyeshwa kwenye kila kundi.

4. Malipo yafanyike kupitia hundi ya Banki. Wasilisha risti ya uthibitisho wa malipo baada ya kukusanya seti za hati za zabuni.
   - ***Account CRDB – 01J1020025101 –Tawi la Kilombero***
   - ***Account NMB – 21706600001 – Tawi la Kilombero***

5. Wasilisha nakala moja halisi ya zabuni zilizokamilika na copi ya nakala katika bahasha iliyofungwa na kuwekwa muhuri TENDA NAMBA 7 , KUUZWA KWA MALI ZA KAMPUNI YA SUKARI KILOMBERO, na kuelekezwa kwa katibu, Kamati ya zabuni, kampuni ya sukari kilombero.S.L.P 50 Kidatu, Morogoro.Na kuweka kwenye sanduku la zabuni lililopo jengo la ofisi kuu ya K1, kitalu cha utawala kabla ya tarehe ya mwisho ya kuwasilisha zabuni.

6. Zabuni zilizochelewa, zabuni zisizokamilika, zabuni za kielektroniki, zabuni ambazo hazijapokelewa, zabuni ambazo hazijafunguliwa na kusomwa hadharani katika hafla ya ufunguzi wa zabuni hazitakubaliwa kwa tathmin..

7. Wazabuni wanaweza kuomba vipengele mbalimbali vya zabuni,Muunganiko wa vipengele au vipengele vyote kwa pamoja.Ushindi wa zabuni utatolewa kwa kila kipengele.

8. Zabuni zote zitafunguliwa hadharani mbele ya wazabuni wote, wawakilishi na mtu yoyote atakaye hudhuria katika ofisi ya kiwanda cha K1 ya Kidatu, mapema baada ya tarehe ya mwisho ya kuwasilisha zabuni.

9. Kumbuka kuwa Kampuni ya Sukari Kilombero haitalazimika kupokea zabuni ya juu au zabuni yoyote.

10. Wazabuni walioshinda watatakiwa kulipa angalau asilimia 30 ya bei ya zabuni ya mali husika siku ya mnada

11. Wanhusika walioshinda zabuni watatakiwa kuzingatia sheria na kanuni zizasimamia mabadiliko ya umiliki wa mali husika kabla ya kuchukua.

12. Wazabuni walioshinda wanapaswa kuhakikisha kuwa mali zimelipwa kikamilifu na kuondolewa katika majengo ya kampuni ndani ya miezi mitatu tangu tarehe ya kushinda zabuni:Vinginevyo tuzo itatolewa kwa mzabuni mwingine anayefuati

13. Gharama za usafirishaji kwa ajili ya kuondolewa kwa mali na wazabuni waliotunukiwa zitalipwa na mzabuni.

14. Waombaji wanaovutiwa wanaalikwa kuwasilisha zabuni zilizotiwa muhuri ipasavyo kupitia anwani iliyo hapa chini kabla ya tarehe 30 Agosti 2024 mnamo, au kabla ya 12:00 jioni kwa saa za ndani.

**a) Kilombero Sugar Company Limited,**
**P.O. Box 50,**
**Kidatu,**
**Morogoro;**

15. Wazabuni wanaohitaji wanaweza kupata maelezo zaidi kutoka kwa anwani zifuatazo:

**KILOMBERO SUGAR COMPANY LIMITED**
**Tenders and Contracts Specialist**
**Jacqueline Macha**
**JMacha@illovo.co.tz**

# SELCOM MICROFINANCE BANK TANZANIA LIMITED
# MINIMUM DISCLOSURES OF BANK CHARGES AND FEES

| DESCRIPTION | | | CHARGE/FEE | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **SELCOM RAHISI,NORMAL SAVINGS, RAHISI CAA, ELIMU, AND KIKUNDI ACCOUNT(RAHISI ACCOUNT)** | | | **TZS** | **USD** | |
| Required minimum opening balance | | | 10,000.00 | - | |
| Monthly service fees | | | 2,000.00 | - | |
| Cash withdrawal over counter up to 10M | | | 3,000.00 | - | |
| Cash withdrawal over counter >10M | | | 10,000 | - | |
| Bank statement 1free per month | | | FREE | - | |
| Bank statement subsequent months | | | 10,000.00 | - | |
| New ATM card issuance | | | 10,000.00 | - | |
| ATM card renewal or replacement | | | 10,000.00 | - | |
| Replacement of the PIN | | | 10,000.00 | - | |
| Standing order Internal | | | 2,000.00 | - | |
| Standing order External | | | 12,980.00 | - | |
| Dormant account fee | | | FREE | - | |
| Interbank Transfer | | | | - | |
| 0-10,000,000 | | | 2,000.00 | - | |
| 10,000,001-50,000,000 | | | 5,000.00 | - | |
| >50,000,000 | | | 10,000.00 | - | |
| International transfer | | | | Up to USD 55 | |
| Closure of account | | | 10,000.00 | - | |
| **NUFAIKA TRANSACTIONAL ACCOUNT** | | | | | |
| Required minimum opening balance | | | 50,000.00 | 25.00 | |
| Monthly service fees | | | 6,000.00 | 3.00 | |
| Bank statement 1free per month | | | FREE | FREE | |
| Bank statement subsequent months | | | 10,000.00 | 10.00 | |
| New ATM card issuance | | | 15,000.00 | N/A | |
| Fees per ATM withdrawal | | | 2,000.00 | N/A | |
| Interbank transfer | | | | | |
| 0-10,000,000 | | | 2,000.00 | 1.00 | |
| 10,000,001-50,000,000 | | | 5,000.00 | 2.10 | |
| >50,000,000 | | | 10,000.00 | 4.20 | |
| International transfer | | | N/A | Up to USD 55 | |
| ATM mini statement | | | 1,000.00 | N/A | |
| Standing order Internal | | | 2,000.00 | 1.00 | |
| Standing order External | | | 12,980.00 | 12.98 | |
| Dormant account fee | | | FREE | FREE | |
| Reactivation of Dormant account | | | FREE | FREE | |
| Letter of recommendation and certificate of balance | | | 50,000.00 | 23.00 | |
| **NORMAL CURRENT ACCOUNT (NUFAIKA ACCOUNTS)** | | | **TZS** | **USD/EURO** | |
| Required minimum opening balance | | | 100,000.00 | 50.00 | |
| Monthly service fees | | | 6,000.00 | 3.00 | |
| Cash withdrawal over counter up to 10M | | | 3,000.00 | 0.18% | |
| Cash withdrawal over counter >10M | | | 10,000 | 10 | |
| Fees per ATM withdrawal | | | 2,000.00 | N/A | |
| ATM mini statement | | | 1,000.00 | N/A | |
| Bank statement once free per month | | | FREE | FREE | |
| Bank statement subsequent months | | | 10,000.00 | 10.00 | |
| Cheque book 25 leaves | | | 20,000.00 | 10.00 | |
| Cheque book 50 leaves | | | 35,000.00 | 15.00 | |
| Dishonored cheque | | | 30,000.00 | 30.00 | |
| Bankers Cheque | | | 50,000.00 | N/A | |
| Stop payment | | | 30,000.00 | 30.00 | |
| Standing order Internal | | | 2,000.00 | 1.00 | |
| Standing order External | | | 12,980.00 | 12.98 | |
| Balance enquiry | | | 1,000.00 | 1.00 | |
| New ATM card issuance | | | 15,000.00 | N/A | |
| ATM card renewal or replacement | | | 15,000.00 | N/A | |
| Interbank transfer | | | | | |
| 0-10,000,000 | | | 2,000.00 | 1.00 | |
| 10,000,001-50,000,000 | | | 5,000.00 | 2.10 | |
| >50,000,000 | | | 10,000.00 | 4.20 | |
| International transfer | | | $55 | 55.00 | |
| Dormant account fee | | | FREE | FREE | |
| Reactivation of Dormant account | | | FREE | FREE | |
| Letter of recommendation and certificate of balance | | | 50,000.00 | 23.00 | |
| **SPECIAL ACCESS NUFAIKA ACCOUNT** | | | **TZS** | **USD/EURO** | |
| Required minimum opening balance | | | 100,000.00 | 50.00 | |
| Monthly service fees | | | 60,000.00 | 50.00 | |
| Minimum monthly turover | | | 20,000,000.00 | 10,000.00 | |
| Cash withdrawal over counter | | | FREE | 0.18% | |
| Fees per ATM withdrawal | | | 2,000.00 | N/A | |
| ATM mini statement | | | 1,000.00 | N/A | |
| Bank statement once free per month | | | FREE | FREE | |
| Bank statement subsequent months | | | 10,000.00 | 10.00 | |
| Cheque book 25 leaves | | | 20,000.00 | 10.00 | |
| Cheque book 50 leaves | | | 35,000.00 | 15.00 | |
| Dishonored cheque | | | 30,000.00 | 30.00 | |
| Bankers Cheque | | | 50,000.00 | N/A | |
| Stop payment | | | 30,000.00 | 30.00 | |
| Standing order Internal | | | 2,000.00 | 1.00 | |
| Standing order External | | | 12,980.00 | 12.98 | |
| Balance enquiry | | | 1,000.00 | 1.00 | |
| New ATM card issuance | | | 15,000.00 | N/A | |
| ATM card renewal or replacement | | | 15,000.00 | N/A | |
| Interbank transfer | | | | | |
| 0-10,000,000 | | | 2,000.00 | 1.00 | |
| 10,000,001-50,000,000 | | | 5,000.00 | 2.10 | |
| >50,000,000 | | | 10,000.00 | 4.20 | |
| International transfer | | | N/A | 55.00 | |
| Dormant account fee | | | 5,000.00 | 5.00 | |
| Reactivation of Dormant account | | | FREE | FREE | |
| Letter of recommendation and certificate of balance | | | 50,000.00 | 23.00 | |
| **MIKAKATI SAVING ACCOUNTS** | | | **TZS** | **USD/EURO** | |
| Required minimum opening balance | | | 20,000.00 | 20.00 | |
| Monthly service fees | | | FREE | FREE | |
| Bank statement 1free per month | | | FREE | FREE | |
| Bank statement subsequent months | | | 10,000.00 | 10.00 | |
| Cash withdrawal over counter | | | 1 FREE WITHDRAW PER MONTH | 1 FREE WITHDRAW PER MONTH | |
| Subsequent Cash withdrawal over counter | | | 20,000.00 | 20.00 | |
| Dormant account fee | | | FREE | FREE | |
| International transfer | | | N/A | Up to USD 55 | |
| Account closure | | | 12,000.00 | 5.00 | |
| **MIKAKATI PLUS SAVING ACCOUNTS** | | | **TZS** | **USD/EURO** | |
| Required minimum opening balance | | | 10,000.00 | | |
| Monthly service fees | | | FREE | | |
| Bank statement once free per month | | | FREE | | |
| Bank statement subsequent months | | | 10,000.00 | | |
| Cash withdrawal over counter | | | ONCE FREE PER MONTH | | |
| Subsequent Cash withdrawal over counter | | | 5,000.00 | | |
| Dormant account fee | | | FREE | | |
| International transfer | | | N/A | Up to USD 55 | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Account closure | | | 12,000.00 | | |
| **KIKUNDI SAVING ACCOUNT** | | | **TZS** | | |
| Required minimum opening balance | | | 10,000.00 | | |
| Monthly service fees | | | FREE | | |
| Bank statement once free per month | | | FREE | | |
| Bank statement subsequent months | | | 10,000.00 | | |
| Cash withdrawal over counter | | | 3,000.00 | | |
| Subsequent Cash withdrawal over counter | | | 3,000 | | |
| Dormant account fee | | | FREE | | |
| International transfer | | | N/A | Up to USD 55 | |
| Account closure | | | FREE | | |
| **BARAKA JUNIOR ACCOUNT** | | | **TZS** | **USD/EURO** | |
| Required minimum opening balance | | | - | - | |
| monthly service fees | | | FREE | FREE | |
| Bank statement 1free per month | | | FREE | FREE | |
| Bank statement subsequent months | | | 10,000.00 | 10.00 | |
| Cash withdrawal over counter | | | FREE | FREE | |
| Subsequent Cash withdrawal over counter | | | FREE | FREE | |
| Dormant account fee | | | FREE | FREE | |
| International transfer | | | N/A | Up to USD 55 | |
| Account closure | | | FREE | FREE | |
| **TERM DEPOSIT RATES 2023** | | | | | |
| **Amount** | | | **Interest Rates** | | |
| 5,000,000 - 500,000,000 | | | 3% - 12% p.a | | |
| > 500,000,000 | | | Negotiation | | |
| **AGENCY BANKING** | **To Govt** | | **To SMFB** | **To Agent** | **New Customer Fee** |
| **Withdrawal (TZS) (agents) Range** | **TZS** | | | | |
| 100-2999 | 10 | | 450 | 350 | 810 |
| 3000-3999 | 14 | | 450 | 350 | 814 |
| 4000-4999 | 27 | | 450 | 350 | 827 |
| 5000-6999 | 54 | | 450 | 350 | 854 |
| 7000-9999 | 56 | | 450 | 350 | 856 |
| 10000-14999 | 102 | | 450 | 350 | 902 |
| 15000-19999 | 195 | | 450 | 350 | 995 |
| 20000-20000 | 306 | | 450 | 350 | 1,106 |
| 20001-29999 | 306 | | 1,400 | 700 | 2,406 |
| 30000-39999 | 351 | | 1,400 | 700 | 2,451 |
| 40000-49999 | 419 | | 1,400 | 700 | 2,519 |
| 50000-99999 | 573 | | 1,400 | 700 | 2,673 |
| 100000-100000 | 707 | | 1,400 | 700 | 2,807 |
| 100001-199999 | 707 | | 2,620 | 980 | 4,307 |
| 200000-200000 | 821 | | 2,620 | 980 | 4,421 |
| 200001-299999 | 821 | | 3,325 | 1,275 | 5,421 |
| 300000-300000 | 838 | | 3,325 | 1,275 | 5,438 |
| 300001-399999 | 838 | | 3,950 | 1,650 | 6,438 |
| 400000-499999 | 982 | | 3,950 | 1,650 | 6,582 |
| 500000-599999 | 1,245 | | 3,950 | 1,650 | 6,845 |
| 600000-699999 | 1,532 | | 3,950 | 1,650 | 7,132 |
| 700000-750000 | 1,700 | | 3,950 | 1,650 | 7,300 |
| 750001-799999 | 1,700 | | 4,850 | 2,250 | 8,800 |
| 800000-899999 | 1,500 | | 4,850 | 2,250 | 8,600 |
| 900000-1000000 | 1,776 | | 4,850 | 2,250 | 8,876 |
| 1000001-3000000 | 1,875 | | 4,850 | 2,250 | 8,975 |
| 3000001-5000000 | 2,000 | | 4,850 | 2,250 | 9,100 |
| **Deposit (TZS) (agents) Range** | **To Govt** | | **To SMFB** | **To Agent** | **New Customer Fee** |
| 0 - 20,000,000 | - | | - | 100 | - |
| **MOBILE BANKING** | | | | | |
| **Withdrawal - Bank to Wallet (TZS)** | **To Govt** | | | | **New Customer Fee** |
| 1000-100000 | | | | | 1,200 |
| 100000.1-300000 | | | | | 2,200 |
| 300000.1-500000 | | | | | 3,200 |
| 500000.1-1000000 | | | | | 4,200 |
| 1000000.1-3000000 | | | | | 5,000 |
| 3000000.1-5000000 | | | | | 7,500 |
| **Deposit (TZS) (Wallet to Bank)** | **To Govt** | | | | **New Customer Fee** |
| 0 - 9,999,999,999 | - | | | | - |
| **Air-time top-up** | - | | | | - |
| **Utility payments** | - | | | | - |
| **Balance inquiry** | - | | | | 400 |
| **Mini-statement** | - | | | | 500 |
| **Full account statement request** | - | | | | 700 |
| **Cheque book request** | - | | | | 700 |
| **SMFB internal transfers (same account holder)** | **To Govt** | | | | **New Customer Fee** |
| 1 - 5,000,000 | - | | FREE | | - |
| **SMFB internal outgoing transfers (other account holder)** | **To Govt** | | | | **New Customer Fee** |
| 1000-750000 | | | | | 750 |
| 750000.1-2000000 | | | | | 1,000 |
| 2000000.1-5000000 | | | | | 1,000 |
| **SMFB External outgoing transfers (Bank to Bank)** | **To Govt** | | | | **New Customer Fee** |
| 1000-100000 | | | | | 3,000 |
| 100000.1-300000 | | | | | 3,000 |
| 300000.1-500000 | | | | | 3,000 |
| 500000.1-1000000 | | | | | 3,000 |
| 1000000.1-3000000 | | | | | 3,000 |
| 3000000.1-5000000 | | | | | 3,000 |
| **FOREIGN EXCHANGE TRANSACTION** | | | **TZS** | **USD** | |
| Telegraphic Transfer - Normal Customer (SWIFT) | | | N/A | Up to USD 55 | |
| TISS- Normal Customer | | | 10,000.00 | 4.20 | |
| TISS-Staff | | | 6,000.00 | 2.10 | |
| **LOAN PRODUCT LENDING RATES** | | | **TZS** | **USD** | |
| MICRO LOANS (Rahisi Loans) TZS 500,000 to 10,000,000 | | | from 3.0% per month to 6.0% per month Based on risk profile/risk group of client - on reducing balance | N/A | |
| MICRO LOANS TZS 10,000,001 to 35,000,000 | | | from 3.0% per month to 5.0% per month- Based on risk profile/risk group of client - on reducing balance method. | N/A | |
| AGRO LOANS TZS 500,001 TO 35,000,000 | | | from 2.5% per month to 6.2% per month - Based on risk Profile/Risk Group of client - on reducing balance method | N/A | |
| SME LOANS/ODs 35,000,000 to 200,000,000 | | | from 2.2% per month to 2.8% per month- Based on risk profile/Risk Group of client.- on reducing balance method | N/A | |
| Loans/OD Secured by Fixed Term Deposits | | | 20.40% | N/A | |
| **Loan Processing Fee** | | | **TZS** | **USD** | |
| MICRO LOANS (Rahisi Loans) TZS 500,000 to 10,000,000 | | | 3.40%Inclusive of excise duty and VAT | N/A | |
| MICRO LOANS TZS 10,000,001 to 50,000,000 | | | 3.40%Inclusive of excise duty and VAT | N/A | |
| AGRO LOANS TZS 500,001 TO 50,000,000 | | | 3.70%Inclusive of excise duty and VAT | N/A | |
| SME LOANS/ODs 35,000,000 to 200,000,000 | | | 2.90%Inclusive of excise duty and VAT | N/A | |
| Loans/OD Secured by Fixed Term Deposits | | | 1.5% Inclusive of excise duty and VAT | N/A | |
| **Application Fee** | | | **TZS** | **USD** | |
| MICRO LOANS (Rahisi Loans) TZS 500,000 to 10,000,000 | | | 20,000.00 | N/A | |
| MICRO LOANS TZS 10,000,001 to 50,000,000 | | | 20,000.00 | N/A | |
| AGRO LOANS TZS 500,001 TO 50,000,000 | | | 20,000.00 | N/A | |
| SME LOANS/ODs 35,000,000 to 200,000,000 | | | 20,000.00 | N/A | |
| Loans/OD Secured by Fixed Term Deposits | | | 20,000.00 | N/A | |
| **Insurance Fee Annual** | | | **TZS** | **USD** | |
| MICRO LOANS (Rahisi Loans) TZS 500,000 to 10,000,000 | | | 1.5% | N/A | |
| MICRO LOANS TZS 10,000,001 to 50,000,000 | | | 1.5% | N/A | |
| AGRO LOANS TZS 500,001 TO 50,000,000 | | | 2.9% | N/A | |
| SME LOANS/ODs 35,000,000 to 150,000,000 | | | 1.5% | N/A | |
| Loans/OD Secured by Fixed Term Deposits | | | 1.5% | N/A | |

# TANGAZO

## SELCOM MICROFINANCE BANK TANZANIA LIMITED

# UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA ZISIZOKAGULIWA KWA UMMA

### IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014

**WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 JUNI 2024**

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | | Robo Mwaka ya sasa 30 JUNI 2024 | Robo Mwaka iliopita 31 MACHI 2024 |
|---|---|---|---|
| **A.** | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 5,133 | 6,191 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 10,152 | 7,017 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | - | - |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 95 | 221 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 24 | 13 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 200 | 200 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 61,505 | 59,216 |
| 12 | Mali Nyingine | 5,482 | 4,803 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 3,150 | 3,189 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **85,741** | **80,850** |
| **B.** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 1,200 | - |
| 18 | Amana za Wateja | 67,277 | 64,068 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 958 | 889 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 1,611 | 1,569 |
| 27 | Dhima Nyingine | 5,570 | 5,381 |
| 28 | Madeni | - | - |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **76,616** | **71,907** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI *(16 kutoa 29)*** | **9,125** | **8,944** |
| **C.** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 40,000 | 40,000 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | - | - |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (31,371) | (31,371) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 496 | 314 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | - | - |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **9,125** | **8,943** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 88 | 235 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 3,243 | 3,573 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 4,547 | 4,514 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | 64 | 64 |
| **D.** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 10.64% | 11.06% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 4.91% | 5.61% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 96.46% | 99.47% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 71.73% | 73.24% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 71.97% | 73.49% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 6.88% | 2.94% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 6.05% | 2.89% |

**TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA**
**KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 JUNI 2024**

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | Robo Mwaka ya sasa 30 JUNI 2024 | Robo Mwaka iliyopita 31 MACHI 2024 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30 JUNI 2024 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30 JUNI 2023 |
|---|---|---|---|---|
| **I: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | 261 | 417 | 677 | 1,085 |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | |
| - Hasara Katika Mali | 333 | 409 | 742 | 1,631 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (2,289) | (3,976) | (6,265) | (6,104) |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | (1) | (8) | (9) | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 4,409 | 1,833 | 6,242 | 4,402 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 524 | 479 | 1,004 | (129) |
| -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (953) | (261) | (1,214) | 244 |
| - Kodi Iliyolipwa | (63) | (63) | (126) | (465) |
| - Mengineyo (bainisha) | (47) | (278) | (325) | (145) |
| *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji* | **2,174** | **(1,449)** | **726** | **520** |
| **II: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (35) | (129) | (164) | (200) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | 1 | 8 | 9 | 6 |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mapato ahirishwa | (20) | (31) | (51) | (20) |
| *Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji* | **(54)** | **(152)** | **(206)** | **(214)** |
| **III: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | (204) | (324) | (528) | (527) |
| Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha | **(204)** | **(324)** | **(528)** | **(527)** |
| | | | - | - |
| **IV: Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | **1,916** | **(1,925)** | **(9)** | **(221)** |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Kipindi | **9,819** | **11,744** | **11,744** | **10,277** |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Kipindi | **11,735** | **9,819** | **11,735** | **10,056** |

**TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI**
**KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 JUNI 2024**

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | Robo ya Mwaka sasa 30 JUNI 2024 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30 JUNI 2023 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30 JUNI 2024 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30 JUNI 2023 |
|---|---|---|---|---|
| 1 Mapato ya Riba | 6,946 | 6,134 | 13,623 | 12,006 |
| 2 Gharama za Riba | (1,286) | (1,185) | (2,460) | (2,384) |
| 3 Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2) | 5,660 | 4,949 | 11,163 | 9,622 |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (528) | (310) | (884) | (775) |
| **6 Mapato Yasiyo ya Riba:** | **1,224** | **1,125** | **2,415** | **2,392** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | (48) | 33 | (94) | 58 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 430 | 368 | 816 | 719 |
| 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | 843 | 725 | 1,694 | 1,615 |
| **7 Gharama Zisizo za Riba:** | **(6,095)** | **(5,251)** | **(12,017)** | **(10,149)** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | (3,701) | (3,085) | (7,007) | (6,232) |
| 7.2 Ada na Kamisheni | (149) | (145) | (304) | (274) |
| 7.3 Gharama Nyingine | (2,246) | (2,022) | (4,706) | (3,642) |
| **8 Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **261** | **513** | **677** | **1,085** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | (78) | 65 | (181) | (107) |
| **10 Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **183** | **578** | **496** | **978** |
| 11 Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | - | - | - | - |
| **12 Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **183** | **578** | **496** | **978** |
| 13 Idadi ya Waajiriwa | 384 | 392 | 384 | 392 |
| 14 Mapato kwa Hisa | 18 | 58 | 50 | 49 |
| 15 Idadi ya Matawi | 8 | 8 | 8 | 8 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0.87% | 3.11% | 1.20% | 2.67% |
| (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 8.06% | 28.11% | 11.08% | 24.54% |
| (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 74.60% | 72.34% | 74.93% | 70.49% |
| (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 37.01% | 37.87% | 37.44% | 37.90% |

**Tarakimu za wastani zitakokotolewa kwa kujumlisha salio la mwisho kwa miezi inayohusika katika kipindi na kugawanya kwa idadi ya miezi katika kipindi hicho.**

**TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 JUNI 2024**

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Kipindi cha sasa hadi 30 Juni 2024** | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka 2024 | 40,000 | - | (31,371) | - | - | 8,629 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 496 | - | - | 496 |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa 30 Juni 2024** | **40,000** | **-** | **(30,875)** | **-** | **-** | **9,125** |
| **Kipindi cha Mwaka uliopita hadi 31 Disemba 2023** | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka 2023 | 40,000 | - | (32,537) | - | - | 7,463 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 1,166 | - | - | 1,166 |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa 31 Disemba 2023** | **40,000** | **-** | **(31,371)** | **-** | **-** | **8,629** |

**BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 JUNI 2024**

| | | |
|---|---|---|
| Imesainiwa na: Julius J Ruwaichi | Mtendaji Mkuu | Tarehe: 25 Julai 2024 |
| Imesainiwa na: Tajinder Singh | Mkuu wa Idara ya Fedha | Tarehe: 25 Julai 2024 |
| Imesainiwa na: Derrick Rushekya | Mkaguzi Mkuu wa Ndani | Tarehe: 25 Julai 2024 |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya Mwaka 2016, na zinaonyesha hali halisi.

| | | |
|---|---|---|
| Imesainiwa na: Thomas Engelhardt | Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi | Tarehe: 25 Julai 2024 |
| Imesainiwa na: Johannes Mainhard | Mkurugenzi | Tarehe: 25 Julai 2024 |

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Suala la utekaji wa watoto lisichukuliwe kwa mihemko

**KWA** takriban awamu tatu za uongozi wa nchi, kumekuwa na taarifa za kuwapo kwa matukio mbalimbali yakiwamo ya watu kutekwa na kupelekwa kusikojulikana huku wengine miili yao ikikutwa katika mazingira ya kutatanisha na mingine ikiwa imenyofolewa baadhi ya viungo.

Katika matukio hayo, pia kulikuwako taarifa za mauaji ya watu wenye ualbino na vikongwe sababu kubwa ikidaiwa kuwa ni ushirikina. Vikongwe walikuwa wanauawa kwa madai ya kuwa wachawi kutokana na ramli chonganishi zilizokuwa zikipotosha jamii kuwa wanahusika na vifo katika jamii. Mauaji ya watu wenye ualbino, yalikuwa yakidaiwa kuwa ni kupata ngozi zao, mtu anaweza kupata manufaa katika shughuli anayoifanya mfano biashara.

Hata hivyo, serikali ilisimama kidete na kukemea huku waliokuwa wakidaiwa kuhusika na vitendo hivyo wakifikishwa kwenye vyombo vya sheria na wengine walichukukuliwa hatua ikiwamo kufungwa jela.

Wakati hayo yakiwa yanaanza kusahaulika, katikati hadi mwishoni mwa miaka ya 2010, liliibuka wimbi la watu kutekwa na watu wasiojulikana.

Ndugu wa watekaji hao walipojaribu kuiomba serikali kuwasaidia kuwapata wapendwa wao, hawakupata msaada.

Pia ziliripotiwa taarifa katika baadhi ya vyombo vya habari kuwa miili kadhaa ya watu imeokotwa kwenye fukwe za bahari na pembezoni mwa mito ikiwa kwenye viroba lakini serikali kupitia vyombo vya ulinzi na usalama, Jeshi la Polisi likiwamo, vilikanusha kwa kusema kuwa habari hizo ni za uongo.

Hivi karibuni, kumeibuka tena hofu ya kutekwa watoto na wengine wakidaiwa miili yao kutupwa kwenye vichaka au kando ya barabara huku baadhi ya viungo vikiwa vimenyofolewa.

Moja ya taarifa zilizotikisa ni za shule moja mkoani Dar es Salaam kudaiwa watoto wawili wametekwa mapema wiki hii. Ilidaiwa kuwa mtu alifika shuleni hapo akiwa na gari aina na Toyota Noah kisha kuwachukua na kutokomea kusiko julikana. Hali hiyo ilisababisha wazazi na walezi wa wanafunzi kujaa shuleni hapo na kutaka kuwachukua wakihofia watoto wao kupotea.

Kama ilivyo ada, Jeshi la Polisi lilitoa taarifa kuwa taarifa hizo si za kweli bali ni uzushi uliokolezwa kutaka kuleta taharuki katika jamii. Jeshi hilo lilitaka taarifa hizo zipuuzwe ilhali wiki iliyopita Rais Samia alikemea vitendo hivyo na kutaka kila Mtanzania ashiriki katika mapambano hayo na kusema serikali isibebeshwe lawama katika hilo.

Kuwapo kwa mikanganyiko hiyo, kumewaibua wanaharakati wa haki za binadamu ambao wamelitaka Jeshi la Polisi kufanyia kazi taarifa za kupotea, kutoa mrejesho mapema na kuweka bayana matukio hayo. Pia wamelitaka jeshi hilo kuepuka kukanusha kwa haraka taarifa zinazotolewa badala yake lichunguze na kueleza ukweli ili kuondoa lawama kuwa linajitetea na kujiosha linapotuhumiwa.

Suala la utekaji watoto ambalo limeakisi mwangwi katika jamii ya Watanzania, linapaswa kuchukuliwa kwa uzito mkubwa na unaostahili kwa kuwa si tu ni fedheha kwa taifa bali linatoa taswira hasi kwa nchi hasa serikali na taasisi zake. Ni vyema Jeshi la Polisi badala ya kujitokeza na kukanusha haraka, likafanya uchunguzi na kutoa taarifa sahihi ili kuwafanya wananchi kuwa na amani.

Ni jambo la kushangaza ofisa wa ngazi za juu katika chombo hicho kilichopewa dhamana ya usalama wa raia na mali zao kuibuka na kutoa matamko makali kuwa habari hizo ni za uzushi na mwenye ushahidi ajitokeze hadharani.

Kauli hizo zinaonyesha wazi kuwa polisi wanaficha udhaifu wao na kuendelea kuwafanya wananchi kukosa imani dhidi yao. Ni vyema wananchi wakapata taarifa sahihi badala ya kuitwa wazushi na kama wahenga wasemavyo lisemwalo lipo kama halipo linakuja, ni dhahiri kwamba kuna jambo lililojificha juu ya taharuki hii.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

Joyce Lameck na Tuntule Swebe

# Tuingie darasani upya kuelewa jinsi kisukari kinavyotugongea hodi mwilini

**AWALI** ugonjwa wa kisukari ulihusishwa na watu wanene pamoja na wazee lakini miaka ya hivi karibuni watoto wachanga, pia wamejikuta wakikabiliwa na maradhi hayo, pindi wanapozaliwa kufikia umri fulani ikiwa mama hakuwa na ugojwa huo kabla.

Utafiti ulifanywa na shirikisho la kimataifa la ugonjwa wa kisukari (IDF), umebaini kuwapo kundi la baadhi ya wazazi ambao hawana uwezo kung'amua dalili mapema za ugonjwa huo kwa watoto wao, ili kufahamu kwanini watoto wanakabiliwa na ugonjwa huo kwa miaka ya hivi karibuni.

Kwa mujibu wa wataaalmu wa matibabu aina hii ya kisukari ni hatari kwa watoto, pale mtoto anapopatikana na aina hii ya kisukari ikiwa seli maalumu zinazotengeneza homoni ya insulini zinapokosekana katika tezi kongosho, pia kongosho zinapoharibika kutokana na sababu yeyote ile husababisha ukosefu kabisa au upungufu wa kichocheo hicho kwenye damu.

Namna ya pili katika aina hii ya kisukari, insulin huzalishwa kwa kiwango cha kutosha isipokuwa tatizo lipo kwenye ufanisi na utendaji kazi wake, mtu anayeugua kisukari kiwango cha sukari huwa juu kwenye damu.

Hii ndiyo sababu ya mtu mwenye ugojwa huu kushindwa kuwa na nguvu za kutosha na wakati mwingine kushindwa hata kutembea kabisa kutokana na kongosho kushindwa kufanya kazi ipasavyo kama ilivyo kawaida kwa kila binadamu.

Mjamzito mwenye kisukari hupata changamoto pamoja na mtoto wakati wa kujifungua kama vile, majeraha wakati wa kuzaliwa kuongezeka kwa hatari ya mtoto kupata (shoulder dystocia) kukwama kwa bega la mtoto wakati wa kuzaliwa.

Pia huchangia mtoto kuzaliwa amekufa, mtoto kuzaliwa na uzito mkubwa (Macrosomia) na kushuka kwa kiwango cha sukari kwenye damu kwa mtoto baada ya kuzaliwa. Hii inaweza kusababisha matatizo ya kupumua.

Hali ya kuwa na kiwango cha juu cha sukari kwenye damu huenda ikaharibu na kuleta madhara ya moyo, macho, miguu na figo, kwa mtoto anaesumbuliwa na ugonjwa wa kisukari, hivyo hupelekea mtoto huyo huyo kuwa na afya dhoofu, pia kushindwa kupata afya bora katika hatua za ukuaji.

Ugonjwa wa kisukari unaweza kutokea hata katika mwaka wa kwanza wa maisha ya mtoto mchanga, dalili zake ni pamoja na kukojoa mara kwa mara, kupumua kwa haraka, na upungufu wa maji mwilini kila mara kwenye mwili wa mtoto.

Inaweza kutambuliwa kwa kupata viwango vya juu vya glukosi katika damu au mkojo, Ukosefu wa insulini unaweza kusababisha mwili kutoa kemikali zinazoitwa ketoni na kusababisha hali inayoweza kutishia maisha inayoitwa ketoacidosis ya kisukari.

Daktari kutoka Hospitali ya Mbweni, Dar es Salaam, Jackson Biganzi, akizungumuza na gazeti la Nipashe alisema "kuna aina mbili za ugonjwa wa kisukari, ya kwanza kurithi kutoka kwa wazazi na hii ndiyo inawapata watoto wachanga pale wanapokuwa wameshazaliwa."

Aidha, aina ya pili hutokana na mwenendo wa maisha kwa mama mjamzito au kwa mtu yeyote, huku chanzo chake kunywa pombe, aina ya vyakula na kutokufanya mazoezi na kupelekea mtu kuwa na uzito uliopitiliza."

Wazazi na walezi wanapoona dalili za ugonjwa huo kwa mtoto ni vema kumuwahisha hospitali, ili kuweza kupata msaada wa tiba kwa haraka na kupata ushauri wa daktari jinsi ya kuishi na mtoto mwenye kisukari kwa kuzingatia maelekezo.

Hata hivyo, tiba maalum na uangalizi mzuri kwa watu wanaougua kisukari, inaweza kuwahakikishia maisha marefu yenye afya bora, watu ambao tayari wapo kwenye matibabu ya ugonjwa wa kisukari.

# TANGAZO

# FIRST HOUSING FINANCE (TANZANIA) LIMITED

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA ZISIZOKAGULIWA KWA UMMA

1st Housing — Homes within your reach

**Imetolewa chini ya kanuni ya 58 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Mikopo ya Nyumba) ya Mwaka 2015.**

## WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30.06.2024

*(Kiasi kwa shilingi elfu)*

| | | Robo Mwaka ya sasa 30th June. 2024 | Robo Mwaka iliyopita 31st Mar. 2024 |
|---|---|---|---|
| A. | MALI | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 1,569 | 278 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | - | - |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 3,599,442 | 3,656,622 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 2,845,810 | 4,007,376 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | - | - |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 31,335,238 | 29,442,028 |
| 12 | Mali Nyingine | 1,081,751 | 1,013,660 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 1,767,980 | 1,622,000 |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 210,332 | 230,560 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **40,842,122** | **39,972,523** |
| | | | |
| B. | B. DHIMA | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | - | - |
| 18 | Amana za Wateja | 2,389,711 | 2,130,169 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 428,545 | 474,975 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 501,281 | 472,498 |
| 27 | Dhima Nyingine | 317,815 | 280,109 |
| 28 | Madeni | 18,206,372 | 17,708,293 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **21,843,724** | **21,066,043** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI *(16 kutoa 29)*** | **18,998,398** | **18,906,480** |
| | | | |
| C. | FEDHA ZA WANAHISA | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 21,800,000 | 21,800,000 |
| 32 | Malipo juu ya bei ya hisa | - | - |
| 33 | Akiba ya Mtaji | 95,831 | 95,831 |
| 34 | Mapato Yaliyobakizwa | (3,273,339) | (3,409,644) |
| 35 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 143,660 | 53,230 |
| 36 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 232,247 | 367,063 |
| 37 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **38** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **18,998,398** | **18,906,480** |
| 39 | Dhima Zisizo Dhahiri | - | - |
| 40 | Mikopo Chechefu | 1,296,473 | 1,110,763 |
| 41 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 360,885 | 300,196 |
| 42 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| | | | |
| D. | BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 46.52% | 47.30% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 4.08% | 3.72% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 1278.45% | 1317.32% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 76.72% | 73.66% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 92.25% | 86.88% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 12.18% | 13.27% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 2.18% | 5.96% |

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA UNAOISHIA 30.06.2024

*(Kiasi kwa shilingi elfu)*

| | Maelezo | Robo ya Mwaka sasa | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) | Limbikizo la Mwaka wa sasa | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 30th June. 2024 | 30th June. 2023 | 30th June. 2024 | 30th June. 2023 |
| 1 | Mapato ya Riba | 1,392,928 | 1,094,465 | 2,724,325 | 2,151,767 |
| 2 | Gharama za Riba | (503,349) | (331,815) | (956,004) | (657,475) |
| 3 | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **889,579** | **762,650** | **1,768,321** | **1,494,292** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (60,689) | (43,838) | (94,167) | (55,573) |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **166,096** | **94,662** | **276,958** | **172,988** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 67 | 142 | 127 | 107 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 114,849 | 87,370 | 206,814 | 165,732 |
| | 6.3 Gawio | 40,100 | - | 40,100 | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 11,080 | 7,150 | 29,916 | 7,150 |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(893,311)** | **(751,892)** | **(1,783,930)** | **(1,494,038)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (556,479) | (399,590) | (992,972) | (791,407) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (336,833) | (352,302) | (790,958) | (702,631) |
| 8 | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **101,675** | **61,581** | **167,181** | **117,669** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (11,245) | (5,946) | (23,521) | (11,624) |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **90,430** | **55,636** | **143,660** | **106,045** |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | - | - | - | - |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa robo ya mwaka /mwaka** | **90,430** | **55,636** | **143,660** | **106,045** |
| | | | | | |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 27 | 25 | 27 | 25 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 0.41 | 0.26 | 0.66 | 0.49 |
| 15 | Idadi ya Matawi | 1 | 1 | 1 | 1 |
| | | | | | |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0.22% | 0.17% | 0.36% | 0.17% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 0.48% | 0.30% | 0.76% | 0.30% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 84.62% | 87.70% | 87.22% | 89.61% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 2.46% | 2.57% | 2.46% | 2.57% |


Katika kuanda taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa, mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8).

| *Jina na Cheo :* | *Saini* | | *Tarehe* |
|---|---|---|---|
| Amulike E. Kamwela **(Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu)** | (Imesainiwa) | ............................ | **25.07.2024** |
| Antidius Kabyemela **(Kaimu Mkuu wa Fedha)** | (Imesainiwa) | ............................ | **25.07.2024** |
| Isambo Binde **(Mkaguzi Mkuu wa Ndani)** | (Imesainiwa) | ............................ | **25.07.2024** |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi).

| *Jina:* | *Saini* | | *Tarehe* |
|---|---|---|---|
| Charles Mugila **Mwenyekiti** | (Imesainiwa) | ............................ | **25.07.2024** |
| Margaret Ikongo **Mkurugenzi** | (Imesainiwa) | ............................ | **25.07.2024** |

## KEY FINANCIAL HIGHLIGHTS




## TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA MWAKA UNAOISHIA 30.06.2024

*(Kiasi kwa shilingi elfu)*

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Robo ya mwaka ya sasa (30.06.2024)** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa robo ya mwaka (01.04.2024)** | **21,800,000** | **-** | **(3,354,925)** | **367,063** | **-** | **95,831** | **18,907,969** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 90,430 | - | - | - | 90,430 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | 134,816 | (134,816) | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa robo ya mwaka (30.06.2024)** | **21,800,000** | **-** | **(3,129,679)** | **232,247** | **-** | **95,831** | **18,998,398** |
| | | | | | | | |
| **Robo ya mwaka iliyopita (31.03.2024)** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka (01.01.2024)** | **21,800,000** | - | **(3,319,721)** | **277,140** | **-** | **95,831** | **18,853,250** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 53,230 | - | - | - | 53,230 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (89,923) | 89,923 | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa robo ya mwaka (31.03.2024)** | **21,800,000** | **-** | **(3,354,925)** | **367,063** | **-** | **95,831** | **18,906,480** |

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA MWAKA UNAOISHIA 30.06.2024

*(Kiasi kwa shilingi elfu)*

| | | Robo ya Mwaka sasa | Robo ya Mwaka iliyopita | Limbikizo la Mwaka wa sasa | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 30th June. 2024 | 31st March 2024 | 30th June. 2024 | 30th June. 2023 |
| I: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | **101,675** | **65,507** | **167,181** | **117,669** |
| | **Marekebisho kwa Ajili ya:** | - | - | - | - |
| | - Hasara Katika Mali | 154,212 | 62,241 | 154,212 | (417,296) |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (2,119,590) | (2,035,538) | (4,133,929) | (3,444,195) |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 259,542 | 249,564 | 509,106 | 335,622 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 47,935 | 486,342 | 495,155 | 238,456 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (95,967) | (209,772) | (266,618) | (183,475) |
| | - Kodi iliyolipwa | (23,521) | (12,276) | (23,521) | (11,624) |
| | - Mengineyo | (40,102) | (2) | (40,102) | 50,841 |
| | ***Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji*** | ***(1,715,817)*** | ***(1,393,936)*** | ***(3,138,516)*** | ***(3,314,003)*** |
| II: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| | Gawio Lililopokewa | 40,100 | - | 40,100 | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (39,817) | (28,333) | (39,387) | 629,873 |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | 57,179 | (56,060) | 1,120 | 2,585 |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji*** | ***57,462*** | ***(84,393)*** | ***1,833*** | ***632,457*** |
| III: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu kwenda CRDB | - | - | - | (161,627) |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| | Deni jipya kutoka CRDB Bank | 498,079 | 1,499,570 | 1,997,649 | 1,078,268 |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | (50,445) |
| | ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha*** | ***498,079*** | ***1,499,570*** | ***1,997,649*** | ***866,196*** |
| | | | | | |
| IV: | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| | **Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha** | **(1,160,275)** | **21,241** | **(1,139,034)** | **(1,815,350)** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 4,007,654 | 3,986,413 | 3,986,413 | 6,696,939 |
| | Badiliko Halisi Katika Mikopo ya mabenki | 0 | 0 | 0 | (398) |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka** | **2,847,379** | **4,007,654** | **2,847,379** | **4,881,192** |

## TARRIF

| S/No | ITEMS | CHARGES/FEES |
|---|---|---|
| 1 | Prime Lending Rate (PLR) | 18% p.a. |
| 2 | Maximum spread above PLR | 4% p.a. |
| 3 | Application Fee (Non-refundable) | TZS 200,000/- |
| 4 | Processing Fee | 1.5 % of the loan value |
| 5 | Facility Fee | 1.5 % of the loan value |
| 6 | Restructuring/Rescheduling Fee | 1% of the restructured/ rescheduling amount |
| 7 | Valuation Fee | Paid by the client as per the invoice |
| 8 | Legal Fee | Paid by the client to FHF account and FHF will pay law firm |
| 9 | Early Repayment | 5% of the amount to be prepaid from Bank or Financial Institution |
| 10 | Annual Review Fee | NIL |
| 11 | Cheque returned Unpaid (Outward & Inward) | TZS 50,000/- |
| 12 | Loan Statement | TZS 20,000/- |


1st Housing
Homes within your reach

Unlike banks we aren't limited to options when it comes to Home Loans.

Being a dedicated mortgage provider, we have a variety of products on home loans which can be cherry picked for every individual.





THE MORTGAGE FINANCIAL INSTITUTION
Dar es Salaam
Plot No. 19, Barack Obama Drive | Postal Address 11990 | +255 22 2113456 |
info@firsthousing.co.tz | www.firsthousing.co.tz

HABARI KITAIFA

# Shahidi asimulia mahakamani mumewe alivyopigwa akazimia

**Na Grace Gurisha**

SHAHIDI Kiran Lalit (52) ameileza Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu Dar es Salaam mume wake alivyopigwa na mshtakiwa Bharat Nathwan (57) hadi kupoteza fahamu kutokana na ugomvi ambao ulikuwa unaendelea wa baina ya familia zao.

Nathwan pamoja na mke wake Sangita Bharat (54), wanaoishi Mtaa wa Mrima - Kisutu, jengo la Lohana Dar es Salaam wanakabiliwa na mashtaka manne, likiwamo la kujeruhi, wanayodaiwa kuyatenda Julai 21, 2023.

Akiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Grace Mwanga, Kiran alidai kuwa anakumbuka Julai 21, 2023, alikuwa nje ya nyumba akiendelea na majukumu huku mafundi wakiweka vigae. Alidai kuwa mshtakiwa Sangita alitoka ndani, akaanza kupaza sauti akitaka atoe malighafi yote yaliyokuwa kwenye kibaraza wakati yote yapo upande wao na si upande wake.

"Aliendelea kupaza sauti, mimi nikamjibu kwamba nitaondoa baada ya mafundi kumaliza kazi, nilipomjibu akaanza kutumia lugha chafu akiwa na maana kwamba niondoe uchafu wangu.

"Nilijaribu kumwelewesha, lakini hakunielewa ndipo nilipompigia simu mume wangu, akakuchukua dakika tano akafika pale," alidai shahidi huyo.

Kiran alidai kuwa baada ya waume zao kufika kwa pamoja eneo la tukio, akajaribu kumwelewesha Bharat kutokana na aliyoyasema mke wake (Sangita), lakini hakumwelewa na pia mume wake alijaribu kuwaelewesha na kuwataka wakayazungumze ofisini hawakuelewa.

"Sangita alianza kutumia maneno machafu tena, na nilipomwelewesha mume wake kuhusu maneno machafu ya mke wake, alikaa kimya, mume wake akamwambia kama hawajamwelewa awaache," alidai.

Shahidi huyo alidai kuwa baada ya kumalizia hiyo sentensi, Bharat alimrukia mumewe na kuanza kumpiga kwa kumkandamiza kifuani na kumpiga mateke.

"Aliendelea kumpiga mume wangu, nilipokwenda kuamulia, Bharat alinishika kichwa changu na kukitumbukiza kwenye ndoo ambayo ilikuwa na mchanganyiko wa saruji na kisha akaendelea kumpiga mateke.

"Watu wote waliyokuwapo kwenye eneo hilo wakaanza kumsukuma Bharat ndipo alipoacha, lakini baadaye akamfuata tena mume wangu, akaanza kumpiga akadondoka chini, akapoteza fahamu. Muda huo uso wangu, macho na masikio yalikuwa yamejaa saruji ila nilikimbia kumsaidia ila hakuweza kuamka," alidai.

Kiran alidai kuwa alimwita mfanyakazi wa ofisi yao ili kumsaidia ndipo alipompa simu yake, akachukua picha, mshtakiwa Sangita baada ya kuona hivyo alichukua simu hiyo ili aitupe. Wakati hayo yote yanaendelea mume wake alikuwa amelala chini.

"Nilifikiria njia ya kumsaidia mume wangu, mafundi walimbeba hadi sakafu ya pili ndipo akaanza kuzinduka, akapewa maji, wakamkimbiza hospitalini kwa ajili ya kupata huduma ya kwanza. Niliondoa saruji baada ya mume wangu kuzinduka, aliulizia simu yake akaanza kupiga simu.

"Niliona wanaume wawili wakiwa wamevaa nguo za polisi, taratibu macho yangu yakaanza kupoteza uoni kwa sababu ya ule mchanganyiko. Waliniambia ninatakiwa niende Kituo Kikuu cha Polisi kuripoti, wakanishauri niite gari la wagonjwa kwa sababu nilikuwa siwezi kutembea vizuri," alidai.

Shahidi huyo alidai alifanikiwa kuita gari hilo, wakati hayo yote yakiendelea Bharat aliendelea kutoa maneno, gari hilo lilimpeleka hadi kituoni huko, akapewa fomu moja akiwa na mume wake, akampelekwa Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa matibabu.

Kesi hiyo imeahirishwa hadi Agosti 6 mwaka huu baada ya Wakili wa Washtakiwa hao, Edward Chuwa kuomba ahirisho kwa kuwa alikuwa anakwenda kwenye shauri lingine mahakama ya juu. Siku hiyo iliyopangwa, atamwuliza maswali ya dodoso shahidi huyo.

## Waziri aagiza wadaiwa sugu waondolewe nyumba za TBA

**Na Halfani Chusi**

WAZIRI wa Ujenzi, Innocent Bashungwa ameagiza Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), kuondoa wadaiwa sugu katika nyumba zao bila kuangalia vyeo vyao.

Aliagiza hayo juzi mkoani Dar es Salaam alipozindua jengo la makazi ya watumishi Magomeni Kota, awamu ya pili B.

Bashungwa alisema kitendo cha baadhi ya wapangaji katika nyumba hizo kutolipa kodi kwa wakati kunakwamisha ujenzi wa nyumba zingine na kusababisha watumishi wa umma kukosa makazi.

"Ninawapongeza TBA kwa namna mnavyofanya kazi hakika, nimependezwa na ubora wa jengo la ghorofa saba nililolizindua ambapo kaya 16 zinaweza kuishi na limejengwa kisasa zaidi.

"Mmeonesha matumizi bora ya ardhi katika eneo hili la Magomeni Kota. Eneo hili lilikuwa na ukubwa wa ekari 32 ambazo zilikuwa zinakaa kaya 645 baada ya ujenzi, kaya hizo zimetosha katika eneo la ekari tisa na eneo lililobaki litatumika kwa matumizi mengine, hili ni jambo zuri," alisema Bashungwa.

Aliagiza barabara zinazongia katika eneo hilo zikarabatiwe kwa kiwango cha lami ili ziendane na hadhi ya nyumba hizo.

"Meneja wa Mfuko wa Barabara, huu mtaa uwekewe lami na jambo hili lifanywe kwa haraka," aliagiza Waziri Bashungwa.

Vilevile, waziri huyo aliagiza TBA kuharakisha ujenzi wa majengo ya awamu ya C, D na E katika eneo hilo.

Alisema kukamilika kwa majengo hayo kutasaidia watumishi wengi kupata makazi na kupunguza malalamiko ya baadhi yao kukosa makazi.







JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI

**UZINDUZI WA UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA KATIKA MKOA WA KIGOMA**

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia wananchi wote kuwa Uzinduzi wa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Awamu ya Kwanza utafanyika Mkoa wa Kigoma tarehe 20 Julai, 2024. Mgeni Rasmi katika uzinduzi huo atakuwa Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (MB). Siku hiyo ya uzinduzi ndiyo itakuwa siku ya kuanza kwa zoezi la uboreshaji wa Daftari Mkoani Kigoma, Tabora na Katavi kwa siku saba hadi tarehe 26 Julai, 2024.

1. **SIKU:** Uboreshaji utafanyika kuanzia siku ya Jumamosi tarehe 20 Julai, 2024 hadi siku ya Ijumaa tarehe 26 Julai, 2024
2. **VITUO:** Uboreshaji utafanyika katika vituo vilivyomo katika Mitaa, vijiji na vitongoji
3. **MUDA:** Vituo vitafunguliwa saa 2:00 Asubuhi na kufungwa saa 12:00 Jioni.

**Uboreshaji utahusisha: -**

1. Kuandikisha Wapiga Kura wapya ambao ni raia wa Tanzania waliotimiza umri wa Miaka 18 na zaidi na hawakuwahi kuandikishwa hapo awali.
2. Kuandikisha Wapiga kura ambao watakuwa wametimiza umri wa miaka 18 siku ya tarehe ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.
3. Kuboresha taarifa za wapiga kura waliohama kutoka eneo moja kwenda eneo lingine la kiuchaguzi
4. Kutoa kadi mpya kwa wapiga kura ambao kadi zao zimepotea au kuharibika.
5. Kuboresha au kurekebisha taarifa za wapiga kura.
6. Aidha,Wapiga kura wanaotaka kuboresha taarifa zao na wanaohama kituo cha kupigia kura au vyote viwili wanaweza kuanzisha mchakato wa kuboresha kwa kujaza fomu maalum kwa njia ya mtandao kupitia tovuti ya Tume www.inec.go.tz au anuwani ya ovrs.inec.go.tz kwa kujaza namba ya kitambulisho cha Taifa, namba ya kadi ya mpiga kura, namba ya simu ya mpiga kura na jina la kata kisha watapokea ujumbe wenye namba ya utambulisho (token number) ambayo wataenda nayo kituo cha kujiandikisha ili kukamilisha taratibu na kupata kadi ya mpiga kura.

**MAMBO YA KUZINGATIA**

- Mwananchi anatakiwa kupanga mstari akiwa kituoni na kusubiri hadi zamu yake ya kuandikishwa itakapowadia. Watu wenye mahitaji maalumu kama vile wazee, wagonjwa, watu wenye ulemavu, wajawazito na akina mama wenye watoto wachanga watakaokwenda nao kituoni watapewa kipaumbele.
- Mwananchi atakapofika kituo cha kujiandikisha atachukuliwa alama za vidole vyote kumi vya mikono na kupigwa picha na kisha kupewa kadi yake mpya hapo hapo kituoni
- Ni muhimu kujiandikisha sasa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ili uweze kupiga kura katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 na chaguzi zijazo
- Zoezi hili halitawahusu wapiga kura ambao waliandikishwa awali, hawajahama maeneo yao ya kiuchaguzi na wana kadi zao za mpiga kura.

**KUJIANDISHA KUWA MPIGA KURA NI MSINGI WA UCHAGUZI BORA**

Limetolewa tarehe 27 Juni, 2024 na:

Kailima, R. K.
MKURUGENZI WA UCHAGUZI



# Serikali ya kijiji matatani kugawa ardhi ya jamii

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

WAKAZI wa Kitongoji cha Darajani kilichoko Kijiji cha Sanya Station, Wilaya ya Hai, wameituhumu serikali ya kijiji hicho, kutaka kugawa ardhi iliyotengwa kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa zahanati na shule ya sekondari.

Wamesema viongozi hao wanataka kugawa ardhi ya kijiji kwa watu waliohamishwa ndani ya eneo linalomilikiwa na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjao (KIA).

Kwa nyakati tofauti jana, baadhi ya wakazi hao waliituhumu serikali ya kijiji hicho, huku wakimuomba Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Deogratius Ndejembi, kuanza kazi kwa kushughulikia malalamiko hayo.

Akizungumzia sakata hilo, Luciana Laizer, mkazi wa Sanya Station, alisema hawako tayari kuona eneo hilo linabadilishwa matumizi kwa kuwa wananchi walikubaliana pajengwe zahanati na shule ya sekondari.

"Hilo eneo tayari wananchi tulishachimba msingi na shule ya msingi, ambayo imeanza kutoa elimu ya awali, ili kuwasogezea karibu huduma hizo kwenye kijiji chetu," alisema Laizer.

Aidha, mkazi wa Sanya Station, Samson Jackson, alisema taarifa walizonazo ni kwamba eneo hilo liko katika mchakato wa kuwapatia watu wanaotaka viwanja, ambao walihamishwa katika eneo la KIA.

"Sasa ukitazama kuna tatizo linaonekana wazi; wanafunzi wanaotoka kwenye kijiji chetu na hasa Kitongoji cha Darajani, wanatembea kilomita tisa kwenda na kurudi, kufuata elimu vijiji jirani.

Na huduma za afya, vivyo hivyo wananchi wanafuata huduma KIA na Mtakuja, ambao ni umbali zaidi ya kilomita tisa," alieleza.

Akijibu tuhuma hizo, Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Joseph Kalala, alisema yuko safarini akirudi atamtafuta mwandishi wa habari ili kulizungumzia.

Hata hivyo, Nipashe ilipomtafuta Mkuu wa Wilaya ya Hai, Amiri Mkalipa kuzungumzia malalamiko hayo, alisema wananchi au serikali ya kijiji wanayo mamlaka ya kupanga mipango yao ya matumizi bora ya ardhi kwa ajili ya shughuli za maendeleo.

Alisema: "Wanayo mamlaka ya kujipangia matumizi yao ya ardhi, lakini hata hivyo ofisi yangu haijapokea malalamiko ya aina hiyo. Nikirejea ofisini nitakutana na pande mbili zinazovutana ili kumaliza malalamiko hayo".



Mkulima wa machungwa katika kijiji cha Kibanda, wilaya ya Muheza mkoani Tanga, Solea Masanja (kushoto), akifafanua jambo kwa waandishi wa habari (hawapo pichani), waliotembelea shambani kwake, wilayani humo juzi, kuhusu ubora wa machungwa anayolima na kuiomba serikali kuwatafutia soko la uhakika la bidhaa hiyo au kujenga kiwanda cha kusindika matunda. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Vyuo 15 Afrika kushiriki maonyesho Arusha

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

VYUO vikuu 15 kutoka nje ya nchi vinatarajiwa kushiriki katika maonyesho ya vyuo elimu ya juu katika Jiji la Arusha, Julai 27 mwaka huu.

Maonyesho hayo yanayolenga kuhamasisha wanafunzi wa kitanzania wanaotaka kwenda kusoma kwenye vyuo hivyo, yameandaliwa na wakala wa elimu ya vyuo vikuu nje ya nchi 'Global Education Link (GEL)'.

Mkurugenzi wa GEL, Abdulmalik Mollel, alisema walianza kufanya maonyesho hayo Zanzibar Julai 15 hadi 21, na katika maonyesho hayo waligundua mahitaji yamekuwa makubwa kwa wanafunzi.

Alisema baada ya kumaliza maonyesho visiwani Zanzibar walifanya maonyesho mengine jijini Dar es Salaam, lakini kutokana na mahitaji kuwa makubwa kwenye mikoa mingine, ndiyo maana wameandaa mengine jijini Arusha.

"Maonyesho Zanzibar yalifana sana na wanafunzi wamekuwa wengi, hivyo tulipoona mahitaji yamekuwa makubwa tumeona tufanye na Arusha ili wanafunzi wengi wapate fursa ya masomo," alisema.

Alisema mwanafunzi atakayeshiriki kwenye maonyesho hayo atapata taarifa zote kuhusu vyuo vikuu nje ya nchi na atakayetaka kudahiliwa atapata udahili hapo hapo.

"Wanafunzi, wazazi na walezi watumie fursa hii kukutana na wawakilishi wa vyuo vikuu vya nje ya nchi kutoka nchi za Uingereza, Canada, India, Cyprus, China Iran na vingine vingi vitashiriki kwa hiyo wanafunzi waje kwa wingi," alisema.

Meneja wa (GEL), Regina Lema, alisema wamekuwa na kampeni ya muda mrefu ya maonyesho ya vyuo vikuu nje ya nchi ambapo walianzia visiwani Zanzibar.

"Napenda kuwakaribisha wakazi wa Kanda ya Kaskazini kuja kwenye maonyesho ya vyuo vikuu vya nje ya nchi ili waone fursa mbalimbali zinazopatikana na kutakuwa na udahili wa hapo hapo kwa watakaohitaji kusoma nje ya nchi," alisema Lema.

Kadhalika alisema: "Huu ni mwendelezo wa maonyesho ya vyuo vikuu nje ya nchi, tulianza Zanzibar, tukaja Dar es Salaam na sasa tunaelekea Arusha. Siku ya Jumamosi hii ni fursa kubwa siyo ya kukosa kwasababu kuna ufadhili wa baadhi ya vyuo kwa asilimia 100".

# Wahasibu kukutana, kujadili uaminifu kwa umma

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WAHASIBU zaidi ya 2,000 kutoka nchi 55 Afrika, wanatarajiwa kushiriki katika mkutano mkuu wa pili wa kimataifa wa wahasibu jijini Arusha, kuanzia Desemba 3 hadi 5 mwaka huu.

Mhasibu Mkuu wa Serikali, Leonard Mkude, alisema mkutano huo unafanyika kwa mara ya pili tangu kuanzishwa kwake Julai 5, mwaka jana.

Alisema umoja wa wahasibu wakuu wa serikali ulizinduliwa rasmi Mombasa, nchini Kenya, Julai 5, 2023 baada ya azimio la kufunga umoja wa wahasibu uliokuwepo katika kanda mbalimbali.

Hata hivyo, alisema lengo la kufanyika kwa mkutano ni kujenga imani ya umma katika mifumo ya usimamizi wa fedha za umma kwa ukuaji endelevu.

Alisema walengwa wa mkutano ni wahasibu, wakaguzi wa hesabu, wataalamu wa masuala ya fedha, Tehama, vihatarishi na kada nyingine, ikiwamo walioajiriwa serikalini, kampuni binafsi pamoja na walioko katika ajira binafsi.

"Tunatarajia kupokea wageni zaidi ya 2,000 ni dhahiri kuwa wafanyabiashara wa nyumba za kulala wageni, hoteli, usafiri, mamalishe na jamii kwa ujumla watafaidika kwa kiasi kikubwa kiuchumi," alisema.

Aidha, alisema washiriki watapata nafasi ya kusikiliza mada mbalimbali ya kitaaluma pia kukutana na wahasibu wakuu wa serikali wa Afrika na kubadilishana uzoefu na kujua fursa zinazopatikana katika nchi za Afrika.

Kadhalika alisema mkutano utakuwa na faida mbalimbali ikiwamo kuwa na Afrika yenye mafanikio yenye msingi wa ukuaji jumuishi na maendeleo endelevu.

Alitaja faida nyingine kuwa ni utawala bora, demokrasia, kuheshimu haki za binadamu na utawala wa sheria, amani na usalama, utambulisho thabiti wa kitamaduni, urithi wa pamoja na maadili.

Mwenyekiti wa Umoja wa Wahasibu Wakuu wa Afrika, Malehlohonolo Mahase, alisema wameichagua Tanzania kufanyika kwa mkutano huo kwa kuwa imekuwa kinara wa matumizi ya mifumo ya kibajeti.

"Nchi ya Tanzania imekuwa na mifumo bora na imara ya kifedha na nchi mbalimba za hapa Afrika zinatamani kuja kujifunza," alisem.

Vilevile, alisema Tanzania, imebarikiwa kuwa na masuala mazuri ya kidemokrasia, amani na upendo, pia kuwapo kwa fursa za uwekezaji, utalii na biashara.





# Watumishi wanne mbaroni tuhuma kuiba mapato

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WATUMISHI wanne wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, wanashikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani humo kwa tuhuma za kuibia mapato serikali kwa kutumia mashine ya mapato (POS).

Akithibitisha kukamatwa kwa watumishi hao, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Janeth Magomi, alisema walipata taarifa ya watumishi hao, kutumia POS mashine ambayo haiingizii mapato serikali.

Alisema walivyofanya uchunguzi wakabaini ni kweli imekuwa ikitumika ndivyo sivyo na kisha kuwakamata.

"Mashine hiyo ilikuwa haingizii serikali mapato ambako bado haijaulikana wameitumia kwa kipindi gani, hivyo polisi bado linaendelea na uchunguzi na ukikamilika watumishi hao watafikishwa mahakamani," alisema.

Katika hatua nyingine Kamanda Magomi alisema Jeshi la Polisi linawashikilia watu watatu kwa tuhuma za wizi wa vipande 20 vya dhahabu, pamoja na brashi ya kusugulia madini hayo na mizani tatu.

Alisema watu hao walikamatwa kufuatia msako uliofanyika katika kupindi cha Juni 26 hadi Julai 24 mwaka huu ambapo pia walikamata vitu mbalimbali vya wizi.

Alivitaja vitu hivyo ni pamoja na dawa za kulevya, pikipiki 14, bomba tatu za chuma, spana 22, redio tatu, simu tano, laptop moja, kinu kimoja cha mashine ya kusaga unga, Tv moja, Solar, betri, kaboni, na deki moja.

Vingine ni mafuta ya dizeli lita 20, bati 10, shock up nne za pikipiki, pombe ya moshi lita 176 na bangi kilogramu 65.

Kuhusu makosa ya usalama barabarani, Magomi alisema Jeshi la Polisi limewafungia leseni madereva wawili kwa kuendesha mwendokasi, huku wakikamata makosa ya barabarani 3,943 magari makosa 2,752, pikipiki na bajaji makosa 1,191.



Mafundi wakimalizia ujenzi wa jengo la maabara ya fizikia katika Shule ya Sekondari Etaro, jimbo la Musoma Vijijini mkoani Mara juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kituo cha elimu athari matumizi ya zebaki kujengwa

**Na Vitus Audax,** GEITA

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limeanza ujenzi wa jengo la kutoa elimu kwa umma kuhusu athari za matumizi ya zebaki kwa wachimbaji wadogo mkoani Geita.

Limesema lengo ni kudhibiti matumizi ya kemikali hizo kwa wachimbaji ambapo ina madhara mengi.

Akieleza kuhusu utekelezaji wa mradi huo unaogharimu Dola za Marekani milioni 1.5, Msimamizi wa mradi wa udhibiti wa matumizi ya zebaki kutoka NEMC, Betrina Igulu, alisema unatarajiwa kukamilika ifikapo Julai, 2025.

Alisema mradi wa usimamizi wa matumizi ya zebaki unatekelezwa na serikali kwa ufadhili wa Benki ya Dunia (WB) kwenye mikoa saba ya Mwanza, Mara Geita , Singida, Mbeya, Songwe na Shinyanga na lengo ni kupunguza au kumaliza kabisa matumizi kwa wachimbaji wadogo.

Aliema kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), zebaki ni miongoni mwa kemikali 10 zenye athari kwa afya ya binadamu.

Hivyo alisema jengo hilo itasaidia jamii kujua matumizi salama ya zebaki, matumizi ya teknolojia mbadala na namna ya kujikinga wasipate maradhi wakati wa kuchenjua dhahabu.

"Tayari tumefanya tathmini ya athari kwa mazingira kwa ujenzi wa jengo hili ili kukidhi Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 na hii ni sehemu ya kutoa mfano kwa jamii kutokana na kuwa sisi ndiyo wasimamizi wa sheria hiyo," alisema.

Mkurugenzi wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira wa NEMC, Lilian Lukambuzi, alisema tayari wameshakabidhi cheti cha tathimini ya athari kwa mazingira kwa ajili ya kujenga kituo hicho baada ya kutimiza masharti yaliyofanywa na NEMC.

Alisema hatua hiyo ni sehemu ya kujihakikishia uendelevu wa mradi wa kudhibiti matumizi ya zebaki kwenye mikoa ya Kanda ya Ziwa.

# Watu 500,000 kuondolewa daftari wapiga kura

**Na Restuta Damian,** KAGERA

TUME Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC) imesema inatarajia kuondoa watu zaidi ya 500,000 katika daftari la kudumu la mpiga kura, kutokana na kupoteza sifa za kubaki katika daftari hilo.

Kauli hiyo imetolewa juzi na mwakilishi wa Mkurugenzi wa Uchaguzi, Giveness Aswile wakati akizungumza na wadau mbalimbali walioshiriki katika kikao cha wadau wa uchaguzi kuhusu uboreshaji wa daftari hilo mkoani Kagera.

Aswile alisema kuondolewa kwa wapiga kura hao ni kutokana na kukosa sifa muhimu za mpiga kura ikiwa idadi kubwa watakaoondolewa ni wale waliofariki dunia na kukosa kabisa sifa ya kuendelea kuitwa wapiga kura.

Alisema kawaida ya hatua hiyo ya uandikishaji inapotakiwa kuanza huwa na makisio yatakayosaidia kuandaa vifaa na kufahamu wapiga kura wapya.

Kadhalika alitaja matarajio yaliyopo kwa mwaka 2024/25 kuwa ni zaidi ya wapiga kura milioni 5.5 sawa na asilimia 18 ya wapiga kura waliokuwepo katika uchaguzi uliopita ambao ni zaidi ya wapigakura milioni 29.

Alisema matarajio kwa ambao wataboresha taarifa zao zaidi walioopoteza kadi za kupigia kura na majina yaliyokosewa katika kuandikisha ni milioni 4.3.

"Tunategemea baada ya zoezi hili daftari litakuwa na jumla ya wapiga kura 3,474,638 na idadi hii inaweza kuongezeka kwa kuwa inawezakana wapo Watanzania ambao walikuwa na sifa za kuandikisha kuwa wapiga kura wakati wa mwaka 2019/20 hawakuwa na sifa za kutumia umri wa miaka 18 uliopo kikatiba," alisema Aswile.

Alisema uboreshaji huo umeanza kwenye Mkoa wa Kigoma, Tabora na Katavi na sasa kuongezeka katika mikoa ya Kagera, na Geita ikiwa lengo ni kueleza jukumu la uboreshaji wa awamu ya kwanza unafanya kakatika mizunguko 13 iliyoanishwa na katiba.

# Wahukumiwa kifungo cha nje, wizi vifaa vya umeme

**Na Shaban Njia,** KAHAMA.

WAKAZI wawili wa Mtaa wa Majengo mkoani Shinyanga, wamehukumiwa kifungo cha nje mwaka mmoja baada ya kukutwa na hatia ya kujaribu kuiba vifaa vya umeme katika mradi wa Usambazaji wa Umeme Vijijini (REA).

Waliohukumiwa ni Johson Alex (27) na Nikodem Kumburu (29) kwa kukutwa na hatia ya kuiba vifaa hivyo vyenye thamani ya Sh.milioni 40 katika kampuni ya Tontan project Teknology inayotekeleza mradi wa usambazaji wa umeme vijijini katika Halmashauri ya Ushetu. Hukumu ya shauri hilo la jinai namba 5102/24 ilitolewa juzi na Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Wilaya ya Kahama, Christina Chovenye baada ya kuridhika na ushahidi uliotolewa na Jamhuri kupitia mashahidi watano. Chovenya alisema kosa hilo ni kinyume na Kifungu cha Sheria Namba 281, Sura ya 2 Marejeo ya Mwaka 2002 na kutoa kifungo cha mwaka mmoja ili iwe fundisho kwa watu wengine wanaohujumu miundombinu ya umeme.

Awali akiwasilisha hoja za upande wa Jamhuri, mwendesha mashitaka wa serikali, Evodia Baimo aliiomba mahakama hiyo kutaifisha gari lililotumika kutenda kosa hilo hoja ambayo ilitupiliwa mbali na mahakama hiyo kwa madai adhabu iliyotolewa dhidi yao inatosha.



Ukurasa 12

MSUGUANO UCHUMI ARDHI

**DC mwenye dhamana abeba jukumu 'mguu kwa mguu' vitani kukabili mauziano feki yaliyokithiri**




Ukurasa 13

Watanzania tumeamua kuwa na nchi ya mawimbi!





Ukurasa 14

**Wizara ya Kilimo yapeleka wapimaji afya udongo, walikohamia wakazi Ngorongoro**

BUFE

IJUMAA JULAI 26, 2024

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

# Katavi, Rukwa zilivyoachiwa trilioni 1.246/-, rekodi ya pekee uwekezaji tangu tarehe uhuru

**Na Ibrahim Yassin,** Songwe

***IKIWA ni mwendelezo wa uchambuzi wa ziara ya wiki moja ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, katika mikoa ya Katavi, Rukwa na Songwe, pata Makala ya majumuisho ya uwekezaji mradi maendeleo ilivyo.***

INAWEZA kuelezwa wiki kamili ya ziara yake, katika baadhi ya mikoa ya Kanda za Juu Kusini yakimaliza kwa kishindo cha maendeleo ndani ya wiki, katikati ya mwezi ulioko sasa, Julai, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akijipanga kimkakati.

Akiwa katika mikoa hiyo ya pembezoni mwa nchi, Katavi, Rukwa na Songwe alikomalizia safari, ni mikoa iliyokuwa na baadhi ya mapengo Rais akipigana kuziba mapengo.

Alishiriki kufunga Wiki ya Wazazi Julai 13, 2024 mkopani Katavi kwenye Viwanja vya Azimio, baada ya hapo akaendeleza mfululizo wa uzinduzi wa uwekezaji wake, hasa wa miradi mikubwa.



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, alipokuwa katika mji mdogo wa Tunduma, mkoani Songwe.
**PICHA: IBRAHIM YASSIN**

Ikatamkwa mkoa wa Katavi umevunja rekodi ya kupata fedha nyingi za maendeleo serikalini, Mkuu wa mkoa wake, Mwanamvua Mrindoko, akikiri haujawahi kupata fedha nyingi za maendeleo kama inavyopata sasa, chini ya Rais Samia; Sh. Trilioni 1.246,776 (Sh. 1,246,776,000,000) za maendeleo.

Mikoa aliyozuru iko juu katika uzalishaji zao kuu la mahindi, kwa mkoani Katavi, Rais Dk. Samia akipandisha bei ya mahindi ya wakulima kwa kilo kutoka Sh. 500 kwa kilo hadi Sh. 600 maeneo ya vijijini na 650 mijini.

Alipofika mkoani Rukwa Julai 17. 2024 akihitimisha ziara yake kwenye Uwanja wa Nelson Mandela, Manispaa ya Sumbawanga, nako akaongeza tena bei ya mahindi hadi Sh. 700, kutoka ya awali Sh. 500.

Hayo yanajiri, huku mkoa wa Katavi kwa sasa unakua kwa kasi katika utalii kwenye mbuga ya Katavi, Bandari ya Kale na 'Center' ya Mpanda, serikali imefanya maboresho kwenye ya Uwanja wa Ndege wa Mpanda, ambako alikagua ujenzi wa jengo la abiria katika uwanja huo wa ndege, uliogharimu Sh. bilioni 1.4.

Mkoa wa Katavi ambayo tangu uhuru hakiuwaji kupata huduma ya umeme wa Gridi ya Taifa, imekuwa ikitumia wastani wa zaidi ya Sh. bilioni mbili kila mwezi kuwasha majenereta ya umeme.

Mageuzi hayo ya Rais Dk. Samia kumetumika Sh. bilioni 48 kujenga kituo kikubwa cha kupoza umeme katika Grid ya Taifa, kilichoko Inyonga Mpanda, ambacho kitaufungua mkoa huo kupata umeme wa uhakika kihistoria.

Katia tafsiri ya mji Katavi kukua kwa kasi, ulinzi na mahitaji ya huduma za ulinzi na usalama wake umekuwa juu, kuchochea shughuli za kiuchumi. Hapo, Rais Dk. Samia, akazindua jengo la kisasa la makao Makuu ya Polisi mkoani Katavi, hata kukaamsha shangwe kwa wananchi.

Upande wa kilimo cha Katavi, ni mkoa wa kilimo unaolisha taifa. Akiwa ziarani, Rais Dk. Samia alizindua maghala na vihenge vya kisasa vya kuhifadhi nafaka vya Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) na Ofisi ya Wataalamu wa NFRA.

Vyote jumla vina uwezo wa kuhifadhi tani 25,000 kwa wakati mmoja, pia akazindua vipimo vya kisasa kupima mazao ya wakulima, pia kukashuhudiwa ziara kwenye hospitali ya rufani inayojengwa kwa awamu mjini Mpanda na inatumika sasa, iliyoainishwa katika gazeti hili Alhamisi wiki iliyopita.

**MKOANI RUKWA**

Mkoani Rukwa, Rais Dk.,Samia akazindua mfululizo wa miradi ya maendeleo, huku mkoa huo ukipata fedha nyingi za maendeleo kiwango chake zikiweka rekodi katika historia ya mkoa huo.

Akikagua na kuzindua hospitali kubwa na ya kisasa, wilayani Nkasi iliyogharimu Sh. bilioni tatu na kunena lengo ni kuwafikishia karibu huduma wananchi, ambao walikuwa wanasafiri kwenda mjini Sumbawanga, takribani kilomitaa 100.

Pia, kukatangazwa serikali imetoa Sh. bilioni 4.5 za kujenga majengo ya kisasa ya Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo, kwenye mji wa Matai, wananchi wasafiri mbali kwenda Sumbawanga kufuata huduma.

INAENDELEA UK.12

UCHUMI

MSUGUANO WA UCHUMI ARDHI

# DC mwenye dhamana abeba jukumu ‘mguu kwa mguu’ vitani kukabili mauziano feki

**Na Julieth Mkireri,** BAGAMOYO

BAGAMOYO ni wilaya iliyoko mkoa wa Pwan na makao makuu yake yalikuwa bandari muhimu ya biashara ya kimataifa katika Karne ya 19 na mwanzoni mwa Karne ya 20.

Mji huo, pia ulikuwa kituo cha biashara ya utumwa, jambo ambalo limeacha alama ya kudumu kwenye historia na utamaduni wa eneo hilo, hadi leo Bagamoyo ni kivutio maarufu cha watalii kinachojulikana kwa fukwe zake nzuri, maeneo ya kihistoria, na tamaduni hai.

Mengi yamefanyika katika wilaya hiyo, kuwafanya wananchi wake waendelee kukua kimaendeleo na kiuchumi ambao wengi wamejikita katika shughuli za biashara za rasilimali za bahari. Wilaya ya Bagamoyo, hivi karibuni imekuwa ikitajwa si kwa utalii sana, bali kwa migogoro ya ardhi husussani katika kata ya Mapinga, jambo ambalo limechangiwa na wengi kuuziwa maeneo ambayo tayari yana hatimiliki.

Katika eneo hilo, wananchi walio wengi wanatoka mkoa jirani wa Dar es Salam na maeneo mengi wamekuwa wakilalamikia kuuziwa maeneo yenye hati miliki na baadhi yao kupata hasara ya kuvunjiwa nyumba zao kutokana na kujenga kwenye maeneo yanayomilikiwa kihalali.

Hali hiyo ilisababisha mawaziri tofauti kutoka Wizara ya Ardhi, wanapofanya ziara zao katika mkoa wa Pwani, ikaawalazimu kufika katika kata ya Mapinga kusikiliza wananchi wenye migogoro.

Pamoja na maeneo mengine ya mkoa wa Pwani kuwa na migogoro ya ardhi katika wilaya za Kibaha, Kisarawe, Mkuranga na Rufiji, bado, lakini Bagamoyo imekuwa ikitajwa kuongoza hususani eneo hilo la Mapinga na Makurunge.

Ni jambo ambalo Ofisi ya Kamishna wa Ardhi wizarani inashuhudia kesi nyingi za ardhi za mkoa huo, inatoka maeneo hayo.



Sehemu ya makazi Kata ya Mapinga, Bagamoyo, ambako mauziano ya viwanja yana msuguano. **PICHA: MTANDAO**

Kutokana na hali hiyo Mkuu wa Wilaya ya Vagamoyo Halima Okash, akaaanzisha Kliniki ya Ardhi, ambayo ilianza kufanyika katika Halmashauri za Chalinze na Bagamoyo, kwa kusikiliza wananchi wenye migogoro akiwa na timu ya watendaji wa ardhi.

Hata hivyo, pamoja na kliniki hiyo, Okash akaona bado ipo sababu ya kuanza oparesheni malaum inayoanza kwenye maeneo yenye migogoro mingi ya ardhi, akiwa na timu ya watendaji wa Idara ya Ardhi, Mwanasheria akiambatana na watendaji kutoka ofisi ya ardhi ya kila Halmashauri.

Jambo analolifanya Okash, ni jipya kwa wakazi wa wilaya hiyo na linawezesha wananchi wengi wenye migogoro kujitokeza kupatiwa ufumbuzi kutoka kwa watalaamu wa ardhi na mwanasheria kuhusiana na maeneo wanayomiliki.

Pamoja na kufanya kliniki hizo kwenye kila Halmashauri za Wilaya ya Bagamoyo, bado Okash anaona kuna malengo hajayafikia katika kutatua migogoro kwenye eneo lake na sasa analazimika kuanzisha Oparesheni Mapinga tokomeza migogoro ya ardhi ambayo aliianza June 24 hadi Julai 15.

Katika Oparesheni hiyo, ofisi ya Mkuu wa Wilaya ikiambatana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya, watendaji kutoka Idara ya Ardhi ya Wilaya hiyo, wanasheria na Ofisi ya Kamishna wa Ardhi mkoa wa Pwani, wakaweka kambi Mapinga, kusikiliza migogoro hiyo..

Ni oparesheni iliyoandaliwa na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo, kwa kushirikiana na watendaji kutoka Ofisi ya Kamishna wa Ardhi Mkoa wa Pwani, wataalamu wa sheria kutoka mahakamani na Halmashauri ya Wilaya Bagamoyo.

Okash anasema, wamelazimika kuanza katika kata hiyo na baadae wataenda Makurunge na Fujayisi, huku akieleza kwamba Oparesheni hiyo kuwa ni kwa ajili ya kusikiliza na kutatua migogoro ya ardhi katika Kata ya Mapinga

Okash anasema, wameona wawafuate wananchi kwenye maeneo yao yenye migogoro,Ili kuyatafutia ufumbuzi kwa kushirikiana na wataalamu wa ardhi na wanasheria.

Anasema katika baadhi ya maeneo kata ya Mapinga kuna mashamba makubwa, nyumba nzuri lakini maeneo wanayoishi hawayamiliki kihalali tofauti na taratibu zinavyoelekeza.

Kadhalika Mkuu huyo wa Wilaya anasema ili kukabiliana na migogoro hiyo pia wameanza kubainisha Makampuni yanayojihusisha na kupima na kuuza ardhi katika wilaya hiyo kutokana na baadhi ya Makampuni hayo kuhusishwa kuuza maeneo yenye hatimiliki.

### WADAU WAKUU

Kamishna Msaidizi wa ardhi Mkoa wa Dar es Salam na Pwani Shukrani Kyando anasema ameungana na Mkuu huyo wa Wilaya kusikiliza changamoto za masuala ya ardhi na kuyatafutia ufumbuzi.

Kamishna Kyando anasema, katika Oparesheni hiyo pia wametumia kutoa ushauri kwa kesi ambazo zipo mahakamani wananchi kuhakikisha wanatii amri Ili kupunguza migogoro isiyo ya lazima.

Pia, ametoa ushauri kwa wananchi kupima maeneo yao sambamba na kufuata taratibu za umiliki wa ardhi kuepusha migogoro ambayo inatokea kwa kutozingatia taratibu.

Rose Leon, ni mmoja wa wananchi waliojitokeza katika oparesheni hiyo ambaye anaiomba serikali kufungia kampuni zinazojihusisha na uuzaji ardhi kutokana na kulalamikiwa kuuza maeneo yenye hati miliki na kuchangia kuwepo kwa migogoro.

Mwinyi Masoud mkazi wa Mingoi, amempongeza Mkuu wa Wilaya hiyo kwa kuanzisha oparesheni hiyo ambayo imekuwa msaada kwa walio wengi kutatuliwa migogoro yao sambamba na kupewa ushauri wa kitaalamu kumaliza migogoro hiyo.

Kupita oparesheni hiyo, Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo, kwa kushirikiana na wataalamu wa ardhi na ofisi ya Kamishna wa Ardhi mkoa wa Pwani wananchi zaidi ya 3,018 walijitokeza kusikilizwa na zaidi ya migogoro 82 ilitatuliwa ikiwemo mikubwa ambayo imedumu kwa zaidi ya miaka 10.

Kupitia Mkuu wa Wilaya, migogoro ambayo ilihitaji suhuhu na maridhiano ambayo kwa kipindi kirefu ilisababisha wahusika kwenda mahakami mara kwa mara hatimaye nayo ilitatuliwa kwa makubaliano ya mmiliki wa eneo na wanaodaiwa kuvamia.

Kupitiaa oparesheni hiyo, Ofisi ya Mkuu wa Wilaya imewabaini baadhi ya vinara wanaodaiwa kuhusika kuchochea migogoro ya ardhi katika kata ya Mapinga na maeneo mengine ya wilaya hiyo, wakiwamo viongozi wa serikali na kichama kuwa mashuhuda wa mauziano ardhi zaidi ya mara moja.

Pia, akasema baadhi wameshiriki moja kwa moja kwenye mauziano maeneo yenye migogoro ambao hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

Baada ya Oparesheni Mapinga Tokomeza Migogoro, Okash anatoa rai kwa wananchi kuzingatia sheria na kanuni za ununuzi na uuzaji wa ardhi kwa kuwashirikisha wataalamu wa idara ya ardhi wa wilaya hiyo kuepusha migogoro isiyo ya lazima.

### ALIYEKUWA WAZIRI

Hivi karibuni Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi Jerry Silaa, naye alifanya ziara katika mkoa wa Pwani na kufanya mkutano wilaya ya Bagamoyo ambayo kupitia kliniki ya ardhi maarufu kama ‘Samia Kliniki.

Alimppongeza Mkuu wa Wilaya-Okash, kwa jitihada alizofanya kutatua migogoro ya ardhi kwa nia ya suluhu na anatumia nafasi hiyo kuwakumbusha wananchi wenye migogoro kuacha kwenda ofisini kwake na badala yake kutmia kliniki za ardhi kwenye maeneo yao kutafutiwa ufumbuzi wa migogoro yao.

Anasema, wananchi wengi wanaoenda ofisini ufumbuzi wa changamoto zao unashindwa kupatikana kwakuwa watendaji pamoja na makamishna wa ardhi wa maeneo yao hawapo ofisini kwake ni lazima watarudishwa kwenye wilaya au mikoa waliyotokea kwa ajili ya utatuzi.

Akawaahidi kuendelea kushirikiana na viongozi wa ardhi kuondoa changamoto za migogoro ya ardhi hapa nchini huku akisema watendaji watakaobainika kuhusika kwenye migogoro hatua za kisheria zitachukuliwa.

Hata hivyo uhalisia unaonyesha kwamba migogoro katika ya ardhi katika mkoa wa Pwani inachangiwa na mashamba ambayo hapo awali yaliachwa bila kuendelezwa kwa muda mrefu na hivyo baadhi ya watu kujichukulia sheria mkononi kwa kuwauzia wananchi bila kufuata taratibu.

## Katavi, Rukwa zilivyoachiwa trilioni 1.246/-, rekodi ya uwekezaji tangu tarehe ya uhuru

**INATOKA UK.11**

Hiyo ndio ikaendana na hatua ya Rais kuzindua barabara kubwa kiuchumi mpaka iliko Bandari ya Kasanga, ikiunganisha Sumbawanga- Matai- Kasanga yenye umbali kilomita 107 kwa gharama Sh. bilioni 150, matarajio baada ya uzinduzi ni kufungua uchumi wa mkoa Rukwa na majirani wa Zambia.

Rukwa, kama ilivyo Katavi ni mkoa uliobobea katika kilimo cha mahindi na ndio zao kubwa la biashara. Huko nako Rais Dk. Samia alizindua maghala na vihenge vikubwa vya kuhifadhi nafaka na mazao yanayolisha taifa.

Rais Dk. Samia alizindua maghala na vihenge hivyo, ili kuongeza uwezo zaidi wa taifa kuhifadhi mazao kwa mauzo nje na matumizi wakati wa dharura vilivyogharimu Sh. bilioni 14 kijijini Kanondo, Sumbawanga, ili kuongeza uwezo wa taifa kuhifadhi mazao kwa mauzo nje na matumizi ya dharura. Ni aina ya msukumo Rais anauweka, kukabiliana na dhana kwamba ‘ilisahaulika.’

Kwenye ziara yake hiyo, Rais Samia akazindua Chuo cha VETA kilichotumia Sh. Bilioni 6.08 kilichopo Kashai Sumbawanga mjini na kimeshaanza kutoa huduma ya kupika vijana kwa fani za ujuzi, pia akaweka katika Uwanja wa Ndege wa Rukwa uliofika asilimia 18.

Vilevile, mkoani Rukwa akazindua Chuo cha Ualimu Sumbawanga, pia akiweka jiwe la msingi la ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Rukwa, kijijimo Mtindile, eneo la Laela.

Rais Samia akaweka jiwe la msingi la ujenzi wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya, Kampasi ya Rukwa, kukidhi kilio cha miaka mingi wakitaka nao wawe na chuo kikuu.

Mjini Sumbawanga, akaweka jiwe la msingi la ujenzi wa barabara ya kilomita sita, kwenda Seminari ya Kaengesa.

### MKOANI SONGWE

Katika eneo la transfoma ya Halmashauri ya Mji wa Tunduma, Rais Dk. Samia akawasalimia wananchi ambako Mbunge wa Tunduma, David Silinde akaeleza jinsi mji mdogo wa Tunduma ulivyopaa kiuchumi, hata kujengwa miradi mikubwa ya maendeleo, akisifu miaka mitatu ya uongozi wa Rais Dk. Samia.

Mbunge wa Viti Maalum mkoani Songwe, Stella Fiyao (CHADEMA), akasifu Serikali ya Awamu ya Sita, kwa ujenzi wa miradi mikubwa na midogo, ikiwamo muuganiko wa kisiasa, kati ya chama tawala CCM na CHADEMA.

Fiyao akatumia nafasi hiyo, kumuomba Rais Dk. Samia kuweka mazingira rafiki ya wafanyabiashara, akisema asilimia 75 ya maduka makubwa yaliyopo upande wa Nakonde nchini Zambia, yanamilikiwa na Watanzania ambao huenda wanakimbilia huko, kukwepa utitiri wa kodi miaka ya nyuma.


George Mwenisongole, Mbunge wa Mbozi na Japhet Hasunga, Mbunge wa Vwawa mkoani Songwe kwa nyakati tofauti baada ya kupewa nafasi, hawakusita kusifu kazi ya serikali, huku Mbunge Hasunga akikazia ombi la mji wa Vwawa kufanywa Manispaa.

Mkuu wa mkoa wa Songwe, Daniel Chongolo, naye akatoa nasaha zake, huku Rais Dk. Samia akiwa juu ya gari, alimuona kijana mwenye mlemavu akamwita na kumuagiza Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, kuhakikisha anamnunulia mguu bandia kwa fedha za ofisi yake.


- **Mwandishi wa makala hii anapatikana kwa simu: 0718 382817-0766936392 na barua pepe: yassin.ibrahimu@yahoo.com**


TAFAKURI YA MLALAHOI

## Watanzania tumeamua kuwa na nchi ya mawimbi!







**NA JOSEPH KULANGWA**
**(+255) 713 410008**
**kulangwasos@gmail.com**


UNAWEZA kusema Tanzania ni nchi ya mawimbi. Maana yake linaibuka wimbi hili, likishuka linaibuka lingine na kelele kibao, huku watu wakilaumiana na kukosa la kufanya.

Miaka ya nyuma liliibuka wimbi la mauaji ya vikongwe, wazee hususan wa kike walioonekana kuwa na macho mekundu, wakihusishwa na masuala ya ushirikina. Mikoa ya Kanda ya Ziwa hususan Shinyanga, ilihusika sana.

Wimbi hilo lilipigiwa kelele na serikali ikiwataka wanajamii kushirikiana nayo kupitia vyombo vya usalama kuyakomesha, hatimaye aliyekuwa bosi wa vyombo hivyo, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Ali Hassan Mwinyi, akajiuzulu.

Mwinyi alijiuzulu uwaziri huo Julai 1976 na si kutokana na yeye kushiriki mauaji hayo, la hasha, bali aliwajibika kutokana na kwamba alikuwa ndiye msimamizi mkuu wa usalama wa raia na mali zao.

Hata hivyo, wimbi hilo halikushuka, liliendelea huku bibi na babu zetu wakiuawa kinyama tu, tena wauaji wengine wakiwa ni ndugu wa karibu, kwa sababu tu ya imani hizo potofu.

Baada ya mapambano ya muda mrefu, wimbi likashuka, lakini likaibuka, likapisha lingine hili likilenga wenye ulemavu wa ngozi, yaani ualbino.

Wauaji kwa imani hiyo hiyo ya kishirikina, wakikata viungo vyao na kuvitumia visivyo. Imani ikiwapeleka kwenye utajiri, kwamba unakata kiungo cha mwenye ualbino, unakipeleka kwa mganga wa kienyeji, anakufanyia ayajuayo na wewe kama ni mchimba madini unatajirika, kama ni mkulima unatajirika na kama ni mwanasiasa unashinda uchaguzi.

Uovu huo pia kama wa mauaji ya vikongwe, ukifanywa na watu wa karibu wa na waathirika. Nchi ikaingia kwenye kimuhemuhe, watu wakikamatwa na voiungo na kufunguliwa mashitaka na kufungwa.

Lawama nyingi zikaelekezwa kwa waganga wa jadi waliorubuni watu kuwa wanawatengenezea dawa hizo, lakini kumbe wakiwakamua fedha na wao kujitajirisha huku wauaji wakiendelea kubaki masikini kama zamani.

Mapambano ya serikali kupitia vyombo vyake, ikishirikiana na wananchi ikashusha wimbi hilo, mauaji hayo yakajipumzisha kidogo mpaka yailivyokuja kuibuka tena mwaka huu, maeneo ya mkoani Kagera.

Katikati hapo likaibuka wimbi, lingine la wasiuojulikana kwamba ni watu wasio na sura, wakiteka wenzao na kuwapoteza ama kwa kuwaua au kuwafanya vinginevyo kusikojulikana.

Kasikia majina ya wanasiasa, wanahabari na wafanyabiashara wakitekwa na wasiojulikana na baadhi yao wakirejea wamejeruhiwa au wakiokotwa wakiwa taabani, lakini wengine mpaka leo hawajulikani waliko.

Mabadiliko ya uongozi wa taifa hili yakatuaminisha kuwa, pengine wasiojulikana, hawa nao walitoweka na awamu iliyopita, lakini kumbe walikuwa wakisubiri muda wao ufike wana kuibuka na wimbi hili lingine.

Hivi sasa ni mshikemshike mitaani katika maeneo mbalimbali nchini, watoto wakitekwa na kupotezwa, wengine wakijeruhiwa na baadhi kuuawa! Sababu yake mpaka sasa haijulikani, inabaki tetesi tu.

Kinachoshangaza na kusikitisha, vyombo vya usalama badala ya kuibuka na kuingia kazini kusaka wanaofanya haya, vinasigana na kuvinatupa lawama kwa wananchi wanaolalamika vikisema ni uongo na nia mbaya ya kuzusha, sintofahamu na taharuki mitaani.

Lakini, vyombo vya habari navyo vinagoma na kuingia mitaani na kutonesha mbashara yanayofanyika mitaani, ambako taharuki imewakuita wenye uchungu, wenye watoto wao.

Wazazi wakiona wenzao wananyolewa nao wanaamua kutia maji nywele zao, kwani kunyolewa kunawakaribia, wakiumwa na nyoka wanaogopa nyasi, hivyo kuzua malalamiko kila kona na kuogopa watu kusogelea watoto wao.

Ni vizuri viongozi wa Jeshi la Polisi nchini. akajiridhisha na hali ilivyo badala ya kuibuka na kusema hakuna kitu kama hicho, bali ni uzushi mtupu unaosababisha taharuki kwa wananchi, wakiwataka kutulia na kuendelea na maisha yao.

Hivi mtoto wa mtu akitekwa na kufanyiwa uovu ikiwa ni pamoja na kulemazwa kama si kuuawa, nani analipa fidia hiyo? Ni vema kujiuliza kulikoni kabla ya kuhitimisha kirahisirahisi.

Yawezekana kuna biashara ya viungo inafanyika ndani au nje ya nchi na tetesi zikisema figo ina soko kubwa, tunadhani wanaosaka fedha wafanyaje kama wanaona kuna bidhaa inayopatikana kwa kuteka Watoto watu?

Tumeamua nchi kuwa ya kamari, hivi sasa kila kona ya nchi kuna michezo ya kubahatisha, hakuna kituo cha redio kisicho na mchezo wa kubahatisha, lipa Sh 1,000 ujipatie maelfu kwa mamilioni ya fedha!

Nani ataacha kubeti na kucheza bahati nasibu au kamari, akaenda kumtafuta Hussein Bashe na mashamba yake ajiunge na kilimo cha BBT?

Kama pesa inapatikana kupitia umekaa nyumbani ukisubiri simu uwe kwa mshindi wa ‘Mshua’, kwanini usijaribu na kuteka mtoto ujipatie figo?

Watanzania tuamke, tuache kusaka utajiri rahisi na wa haraka tutaangamizana bure. Fuatilia anayocheza bahati nasibu hizo, utakuta ni walalahoi wasio na kitu! Kwanini? Usinijibu tafadhali.

UCHUMI

# Wizara ya Kilimo yapeleka wapimaji afya udongo walikohamia wakazi Ngorongoro

**Renatha Msungu,** DODOMA

• Lengo kubaini mazao kulima, ubora wake

SERIKALI inatekeleza uhamishaji kwa hiari, wakazi wa eneo la Hifadhi ya Taifa ya Ngorongoro kwenda vijiji vya Msomera wilayani Handeni mkoani Tanga, Saunyi Wilaya ya Kilindi mkoani Tanga na Kitwai Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara

Ni kazi inayotekelezwa kwa awamu, ikihusisha kuhamisha kaya 503 zenye watu 3,010 na mifugo 15,321 kwenda kijiji cha Msomera na sasa lipo kwenye Awamu ya Pili ya utekelezaji, ikihusisha kuhamisha kaya 5,000 kutoka eneo la Hifadhi ya Taifa ya Ngorongoro kwenda kwenye vijiji vya Msomera, Saunyi na Kitwai.

Baada ya kutekeleza wajibu wa kuwawezesha wananchi hao kuhamahama kwenye eneo Hifadhi ya Taifa ya Ngorongoro , Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akawahakikisha inawawezesha wananchi hao kuwa na mifumo na miundombinu muhimu itakayowawezesha kujikwamua kiuchumi na kujiletea maendeleo.


Serikali iliamua kupeleka wataalamu wa sekta mbalimbali katika vijiji hivyo ili kuwasaidia wananchi hao kuhakikisha wanaweza kuyaendesha maisha yao na hatimaye kujiletea maendeleo. Wizara za kisekta na taasisi mbalimbali nazo zimehusishwa kupangiwa majukumu kuwawezesha wananchi hao. Wizara ya Kilimo, sasa imepewa jukumu endelevu la kutoa elimu ya kilimo na uhakika wa chakula.

Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, katika hatua yake kukuza kilimo, kupitia wizara husika, ikapeleka wataalamu wanaoongozwa na Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Usimamizi na Mipango ya Matumizi ya Kilimo, Mhandisi Godwin Makori, kufika vijiji vya Msomera, Saunyi na Kitwai kwa ajili ya shughuli maalum ya kupima afya ya udongo.

Waziri mwenye dhamana ya kilimo, Hussein Bashe, anasema lazima afya ya udongo ipimwe, ili wakulima wajue aina ya mazao wanayotakiwa kulima katika mkoa husika.

Kutokana na hilo, Wizara ya Kilimo, ilisambaza wataalamu wa kilimo, wakiwaemo maofisa ugani kusaidia katika kijiji kata na kujua afya ya udongo kabla msimu wa kilimo haujaanza ili walime mazao yanayostahili ambayo yatawainua kiuchumi.

Kazi hiyo imefanyika kwa kila eneo, kuna maofisa ugani wanasaidia wakulima kujua afya ya udongo kabla hawajaanza kulima, ili walime mazao stahiki katika eneo husika ili waweze kuvuna mazao mengi katika mashamba wanayolima.



Makazi mapya ya wananchi waliotoka Ngorongoro. **PICHA ZOTE: MTANDAO**



Shughuli za kilimo zikiendelea kijijini Msomera, walikohamia wakazi wa Ngorongoro.

**KIJIJINI MSOMERA**

Akizungumza kijijini Msomera wilayani Handeni mkoani Tanga, wakati wa upimaji wa afya ya udongo , Mhandisi Makori, anasema lengo kuu la kupima afya ya udongo ni kuwezesha kupata taarifa za afya ya udongo zitakazowezesha kufanya maamuzi sahihi na endelevu ya matumizi ya ardhi ya kilimo ikiwemo matumizi, aina na kiwango cha mbolea.

Mkurugenzi Makori anafafanua kuwa taarifa hiyo itawezesha maandalizi ya Mpango Bora wa Usimamizi wa Matumizi ya Ardhi ya Kilimo katika vijiji hivyo.

Mkurungenzi Makori anaongeza kuwa mpango huo na masuala mengi ya kitaalamu kwenye kilimo, utaanisha matumizi ya aina sahihi ya zana za kilimo kwa kutengemea aina za udongo zilizopo kwenye maeneo husika.

Mhandisi Makori anasema, mpango huo pia utaainisha mbinu bora za kilimo zitakazoendana na hali halisi ya udongo katika maeneo hayo.

Upimaji afya udongo unaooendeshwa na Wizara ya Kilimo, umeishirikisha wataalamu wa Wizara ya Kilimo na wataalamu wa kutoka Sekretarieti za Mikoa ya Tanga na Manyara na Halmashauri za Handeni, Kilindi na Simanjiro. Mhandisi Makori zoezi hilo limefanikisha uchukuaji wa sampuli kwenye eneo lenye ukubwa wa zaidi ya hekta 46170.35. Ukubwa wa ardhi hiyo inajumuisha zaidi ya hekta 48,000 kwenye cha Msomera,

Hekta 72,000 katika Kijiji cha Saunyi na Hekta 144,000 katika Kijiji cha Kitwari Mhandisi Makori amefafanua kuwa kaya zote za vijiji vya Msomela, Saunyi na Kitwale zilizokuwa zinaishi hapo awali pamoja na kaya zilizohamia kutoka Ngorongoro zitanufaika na zoezi la upimaji wa afya ya udongo.

Mhandisi Makori anasema, matokeo ya vipimo hivyo yatawezesha wananchi kulima kisasa na kwa ukakika kwani vipimo vya udongo vitawawezesha wakulima kujua matumizi sahihi ya pembejeo zitakazowapa matokeo mazuri.

Kuhusu upimaji wa afya adongo unaofanywa na Wizara ya Kilimo katika maeneo mbalimbali nchini, Mkurugenzi Makori amesema serikali itaendelea kupima afya ya udongo kwenye maeneo yote ya kilimo.

"Zoezi la upimaji wa afya ya udongo kwenye ardhi ya kilimo hapa nchini ni endelevu, lengo la serikali ni kuhakikisha shughuli za kilimo zinafanyika kwa kuzingatia kanuni na mbinu bora za kilimo zitakazowezesha ardhi hiyo kuzalisha kwa tija na uendelevu," anasema Mhandisi Makori.

Viongozi na wananchi wa Kijiji cha Msomera, wamepokea kwa mikono miwili huduma hiyo waliyopelekewa na serikali yao na Mhandisi Makori anapokea, akisema wataalam hao wamepata ushirikiano wa kutosha kutoka kwa viongozi na wananchi wa vijiji hivyo.

Anasema serikali haitoacha kupima afya ya udongo kwa sababu inahitaji kuona wakulima wake wanafanya kilimo chenye tija na sio bora kilimo. Mwenyekiti wa Kijiji cha Msomela kata ya Misima wilaya ya Handeni Mkoani Tanga, Martin Oleikayo, amempongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kuwahakikishia wananchi wa hao maisha bora na yenye uchumi endelevu.

Aidha, Oleikayo anamsifu Waziri wa Kilimo Mhe. Hussein Bashe, kwa kupeleka wataalam wa kupima afya ya udongo kwani huduma hiyo ni miongoni mwa mahitaji makubwa ya wananchi wa wa kijiji hicho na maeneo ya jirani na imelekwa katika muda sahihi.

**WAKAZI WANENA**

Wanasema serikali imefanya jambo jema la kupima afya ya udongo, kwa sababu itawasaidia kwa kiasi kikubwa kujua nini wanatakiwa kulima katika ardhi ya eneo fulani.

Jumanne Ole Naiko, anasema wao wakiwa wakazi wa kijiji cha Msomera, hivi sasa wanaendesha kilimo bila ya wasiwasi wowote kutokana na kwamba udongo wa eneo hilo umepimwa na wanajua ni aina gani ya mazao wanakwenda kupanda.

Anaiasa serikali iendelee na zoezi la upimaji wa afya ya udongo katika maeneo mbalimbali,kwa sababu inasaidia kwa kiasi kikubwa wakulima kujua ni mazao gani wanatakiwa kupanda ili yaweze kustawi katika eneo husika.

> **"Zoezi la upimaji wa afya ya udongo kwenye ardhi ya kilimo hapa nchini ni endelevu, lengo la serikali ni kuhakikisha shughuli za kilimo zinafanyika kwa kuzingatia kanuni na mbinu bora za kilimo zitakazowezesha ardhi hiyo kuzalisha kwa tija na uendelevu.**

# Serikali yatoa maagizo kwa h'shauri kuhusu barabara

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imezitaka halmashauri zote nchini kufanya usafi wa mitaro ya barabara zinazojengwa katika maeneo yao, kwakuwa jukumu hilo ni wajibu wao na siyo Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA).

Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) anayeshughulikia miundombinu, Rogatus Mativila alisema hayo juzi wakati wa ziara yake ya kukaguzi barabara na madaraja yaliyojengwa kwenye Kata ya Kibakwe wilayani hapa.

Matavila alisema halmashauri zielewe kuwa suala la kusafisha barabara zilizojengwa kwenye maeneo yao ya miji na majiji yao ni wajibu wao hivyo wanapaswa kuzisafisha.

"Tumeshaletewa barabara nzuri tuzitunze ili zitusaidie sisi wenyewe, mwananchi una nyumba hapo pembeni ya barabara ni vyema kujitoa kusafisha hizo nyasi kandokando ya barabara", alisisitiza.

Kuhusu ujenzi wa barabara zinazotekelezwa na TARURA wilayani Mpwapwa alisema mji umeanza kupendeza, kwamba tayari ujenzi, madaraja pamoja na uwekaji wa taa unaendelea.

Alisema katika Kata ya Kibakwe TARURA imeshajenga barabara ya lami yenye urefu wa kilomita1.8 na barabara ya kilomita moja iko kwenye hatua za ujenzi, kwamba lengo ni kufikia kilomita 2.8 ifikapo Septemba mwaka huu.

"Tunaishukuru serikali kwa kutafuta fedha za ujenzi wa barabara nchini. Serikali imeona umuhimu wa maendeleo ya barabara za mijini pamoja na kuondoa vikwazo kwa sababu yakukosekana kwa vivuko au madaraja," alisema na kuongeza:

"Rais ametafuta fedha kwa lengo la kuhakikisha makao makuu ya wilaya zote pamoja na miji mikubwa inayokuwa angalau ziwe na lami ili kuunganisha barabara za mijini ambapo sehemu nyingi sana tayari zimejengwa barabara za lami" alisema.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Kibakwe, Baraka Zebedayo alisema wanafanya uhamasishaji kwa wananchi kuendelea kutunza barabara kwa kufanya usafi kwenye mitaro na pembezoni mwa barabara.

Diwani wa Kata ya Kibakwe, Athanas Chisanza aliishukuru serikali kwa kuwapatia fedha za ujenzi wa barabara na hivyo kuchochea kasi ya maendeleo katika kata yao na wananchi kwa ujumla.

Alisema baada ya kuwekewa lami wananchi wamepata maendeleo makubwa kiuchumi kwakuwa kata yao ni wazalishaji wakubwa wa mazao, hivyo imewarahisishia shughuli za usafirishaji.




Mbunge wa jimbo la Singida Magharibi, Elibariki Kingu (kulia), akizungumza katika mkutano wa hadhara wa wananchi wa kijiji cha Iseke, jimboni humo jana, ambapo aliwataka kuhakikisha wanashiriki uchaguzi wa serikali za vijiji na mitaa na uchaguzi mkuu ujao. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Mkalama watakiwa kuwa wazalendo

**Na Thobias Mwanakatwe,** MKALAMA

WATUMISHI wilayani Mkalama mkoani Singida wametakiwa kuwa wazalendo na kufanya kazi kwa bidii, ili kuwaenzi mashujaa wa nchi.

Katibu Tawala Wilaya ya Mkalama, Peter Masindi, alisema hayo jana wakati wa zoezi la usafi liliofanyika katika Hospitali ya Wilaya ikiwa ni sehemu ya kuadhimisha Siku ya Mashujaa nchini.

Alisema serikali inaleta fedha nyingi kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo, hivyo ni wajibu kwa watumishi wawajibike pamoja katika kuhakikisha fedha hizo zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa.

"Kila mmoja katika nafasi yake atimize wajibu wake, huwezi kuwa shujaa kama ukishindwa kutimiza wajibu wako, kwa kufanya hivi tutakuwa tumewaenzi mashujaa wetu," alisema Masindi.

Aidha, aliwataka watumishi kuwahudumia wananchi kwa kutumia lugha nzuri pindi wanapokuwa wanatoa huduma kwa wananchi, kulinda maadili ya kazi pamoja na kudumisha amani na umoja baina yao

"Tuache ubabe, tuache ufalme kwa kutumia ofisi zetu za serikali, bali tuwatumikie Watanzania kwa lugha nzuri,"alisema.

Pamoja na mambo mengine, aliwakumbusha watumishi kulinda maadili ya nchi yetu kwa kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsia, vitendo vya ulawiti na ushoga katika jamii zetu.

Alisema: "Ndugu zangu tuhakikishe maadili ya watoto wetu yanajengwa na sisi wazazi, yanajengwa na sisi jamii iliyopo leo, tuhahitaji jamii yenye utuvuli, amani kwa ajili kufikia maendeleo ya taifa letu, hakikisha mtoto anaenda shule, huo ndiyo ushujaa unaostahili".

# Uchumi wakazi Kilimatinde wapaa kwa asilimia 44

**Na Renatha Msungu,** MANYONI

UCHUMI wa wananchi wa Tarafa ya Kilimatinde Wilaya ya Manyoni umepanda kutoka asilimia 33 hadi 77 kutokana na miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa na shirika la World Vision.

Ofisa Tawala kutoka Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Manyoni, Leila Sawe aliyasema hayo jana wakati wa maadhimisho ya miaka 21 ya hitimisho la utekelezaji wa miradi ya afya, maji, kilimo na ufugaji, ilioongeza mnyororo wa thamani katika maendeleo ya kiuchumi wilayani Manyoni.

Leila alitoa pongezi kwa shirika hilo kutokana na kazi kubwa waliofanya kwenye miradi mbalimbali katika wilaya hiyo ambayo imewasaidia wananchi kuinuka kiuchumi kutoka hatua moja kwenda nyingine.

Alisema World Vision wameweza kufadhili miradi mbalimbali ya kijamii ambayo imeenda kugusa maisha ya wananchi wa Tarafa ya Kilimatinde.

"Hii miradi tunaendelea kuishukuru World Vision wamefanya jambo kubwa sana la kuhakikisha miradi inakuwa endelevu kwa sababu jamii ilishiriki kuanzia kuibua, kuitekeleza na sasa wamekabidhiwa," alisema Sawe.

Katika hatua nyingine, alitoa wito kwa jamii ya Kilimatinde kuhakikisha wanaendelea kuipokea miradi na kuitunza ili iwe na uendelevu hata kesho mfadhili akija aone.

Mwakilishi wa Mkurugenzi wa World Vision Tanzania, Teddy Marke aliwaomba wananchi wa Kilimatinde na Serikali kuhakikisha yale waliyojifunza katika miaka 21 wanayatunza, kuyahifadhi na kuyaendeleza.

"Yale tulojifunza katika miaka 21 tuhakikishe tunayatunza na kuyaendeleza ili kazi hii kubwa mlioifanya ambayo ni ya maana iwe endelevu," alisema.

Aidha aliwapongeza wafanyakazi wa World Vision Tanzania kwa kazi kubwa ambayo wameifaya katika Tarafa ya Kilimatinde ya mradi wa AP, huku akiitaka jamii kuyaenzi yote waliofundishwa kwenye mradi.

Awali Samweli Mazuguni akisoma risala ya wananchi wa Tarafa ya Kilimatinde katika sherehe hizo za kuhitimisha ufadhili wa mradi wa World Vision Kilimatinde AP aliiomba serikali na wadau wengiine wa maendeleo kutoa ushirikiano kwa wanajamii wa Kilimatinde ili kuyaendeleza mafaniko yaliyofikiwa na kutatua changamoto ambazo zinaonekana kuwa kikwazo kwa jamii.

Alisema World Vision Tanzania wamefanya mambo makubwa ambayo yanapaswa kuigwa na kuendeleza ili kuzidi kuwainua kiuchumi wananchi wa eneo hilo.

Alisema wanalishukuru shirika hilo huku akiwasisitiza waendelee kuleta miradi mingine katika eneo hilo ili kuzidi kuwasaidia wananchi wa wilaya hiyo.





# Waraibu dawa za kulevya 280 wasitisha matibabu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WARAIBU 280 wa dawa za kulevya katika mikoa ya Mbeya na Songwe waliokuwa wanapatiwa matibabu ya methadon kwenye vituo mbalimbali wamesitisha matibabu na kutokomea kusikojulikana, hali ambayo inahatarisha afya zao.

Mkurugenzi wa mradi wa HJFMRI Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Dk. Emmanuel Bahemana aliyasema hayo kwenye kikao kazi cha wadau wa kuzuia na kupambana na dawa za kulevya nchini, kilichofanyika katika Mji wa Tunduma mkoani Songwe.

Wadau walioshiriki kikao hicho walikuwa ni maofisa wa vyombo vya dola, mashirika yanayowahudumia waraibu wa dawa hizo na Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kuzuia Dawa za Kulevya (DCEA), Aretas Lyimo.

Dk. Bahemana alisema sababu za waraibu hao kutoroka matibabu hayo ni pamoja na umbali kutoka kwenye maeneo wanayoishi kwenda kwenye kliniki za huduma hiyo.

Vilevile, baadhi yao waliacha kuhudhuria kliniki hizo kutokana na kukosa kipato cha kuwezesha kufika kwenye vituo hivyo. "Kati ya waraibu hao ambao wameacha kuhudhuria kliniki 216 ni waliokuwa wanapata huduma katika Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya na 68 walikuwa wanapata huduma katika kliniki yetu iliyopo mjini Tunduma," alisema Dk. Bajemana.

Alisema wanashirikiana na wadau mbalimbali yakiwemo mashirika yasiyokuwa ya kiserikali kuwafuatilia waraibu hao ili warejee kwenye huduma hiyo.

Kamishna Jenerali wa DCEA, Lyimo alisema mamlaka hiyo inaendelea na juhudi mbalimbali za kukabiliana na uingizaji wa dawa za kulevya nchini.

Alisema moja kati ya mbinu wanazotumia ni pamoja na kushirikiana na wadau mbalimbali kukamata wasafirishaji wa dawa hizo na kuwachukulia hatua kali za kisheria ikiwemo kuwafikisha mahakamani na kutaifisha mali zao.

Alisema katika kipindi cha mwaka mmoja mamlaka hiyo ilifungua mashauri 1417 yanayohusu usafirishaji wa dawa za kulevya na kwamba 1359 tayari yameshatolewa uamuzi na yaliyobakia yanaendelea kushughulikiwa katika hatua mbalimbali.

Baadhi ya waraibu wa dawa hizo wanaoendelea kupatiwa matibabu ya methadone katika kliniki ya Tunduma, waliiomba serikali kuongeza nguvu katika kuwadhibiti wauzaji wa dawa hizo wakidai kuwa bado wanaendelea kuwaharibu vijana katika mji huo.

Mmoja wa waraibu hao, Eliothelios Lusungu alisema katika mji huo wa dawa za kulevya bado zinaendelea kuuzwa hasa katika Mtaa wa Kilimanjaro na maeneo ya mpakani na nchi jirani ya Zambia.




Kamanda wa Kanda Maalumu ya Polisi Dar es Salaam, SACP Jumanne Muliro (katikati) akipokea msaada wa vifaa vya usalama barabarani kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Sigara Tanzania, Takashi Araki, katika Kituo cha Polisi Kati, jijini Dar es Salaam jana, ikiwa ni sehemu ya mipango ya uwekezaji kwa jamii ya kampuni hiyo. Wengine ni Mkurugenzi wa Mawasiliano na Uhusiano wa kampuni hiyo, Patricia Mhondo na askari wa kikosi cha usalama barabarani, Koplo Mwajabu Kamili. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ubovu barabara Njombe wawaibua madiwani

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

BARAZA la Madiwani la Halmashauri ya Mji wa Njombe limeagiza barabara zote zilizopo kwenye halmashauri hiyo ambazo zimejengwa na kuharibiwa na mvua zirudiwe upya.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji wa Njombe, Erasto Mpete alitoa agizo hilo wakati akifunga kikao cha kawaida cha Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Mji wa Njombe kilichofanyika wilayani Njombe juzi.

Alisema barabara nyingi za halmashauri hiyo makandarasi walijenga chini ya kiwango na kipindi cha mvua ziliharibika na kusababisha adha kwa wananchi.

"Barabara iliyokuwa na changamoto kubwa ni Barabara ya Zengerengeti-Utalingolo na Kilenzi Kisilo hadi Luponde kwa sababu hivi sasa inachukua magari mengi," alisema Mpete.

Hata hivyo aliagiza Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) Wilaya ya Njombe kuwasimamia makandarasi ipasavyo ili watekeleze miradi hiyo haraka na wananchi waanze kunufaika kwa kusafirisha mazao.

Kuhusu ukusanyaji mapato, alisema hadi kufikia Juni mwaka halmashauri hiyo imekusanya Sh. bilioni 6.3 sawa na asilimia 99.62 ya ukusanyaji wa mapato ya ndani.

Alisema halmashauri imebakiwa na Sh. milioni 24.3 ili kufikia lengo la asilimia 100 ya makusanyo ambayo bajeti ya mapato ya ndani iliyoidhinishwa mwaka wa fedha 2023/24 ilikuwa Sh. bilioni 6.4.

Kaimu Meneja wa TARURA Wilaya ya Njombe, Kelvini Luoga alisema zipo barabara ambazo zinadaiwa kuwa zimejengwa chini ya kiwango lakini ukweli ni kuwa barabara hizo ujenzi wake bado haujakamilika.

Alisema serikali imeongeza bajeti TARURA ambapo awali ilikuwa shilingi bilioni moja, lakini kwasasa imefikia shilingi bilioni 3.2.

# Viongozi UWT watakiwa kuwaunganisha wanawake

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

VIONGOZI wa Jumuiya ya Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT) Mkoa wa Mbeya, wametakiwa kuwaunganisha wanawake ndani ya mkoa huo, badala ya kuwagawa.

Katibu wa CCM Mkoa wa Mbeya, Langaeli Akyoo aliyasema hayo juzi kwenye Baraza Kuu la UWT Mkoa wa Mbeya lililokuwa na lengo la kupokea taarifa ya utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya chama hicho katika ngazi ya mkoa.

Taarifa ya utekelezaji wa ilani iliwasilishwa na wabunge wa viti maalumu ambao ni Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Maryprisca Mahundi na Suma Fyandomo.

Akyoo alisema chama hicho hakitaruhusu mtu yeyote kuwagawa wanachama kwa namna yoyote na kwamba hiyo ndiyo siri pekee ya kuufanya mkoa kuwa na utulivu.

Alisema agizo hilo ni la chama mkoa na hivyo kila kiongozi na mwanachama wa chama hicho lazima azingatie ili kuepuka kuchukuliwa hatua za kinidhamu.

"Utakapokuwa unapambana na kiongozi yeyote wa jumuiya basi ujue kwamba unapambana na chama na atakayeumia ni wewe mwenyewe, sisi hatutaruhusu mtu yeyote atugawe lazima tutashughulika naye," alisema Akyoo.

Aliwataka wabunge wa viti maalumu kuwahudumia wanawake wa mkoa huo kwa upendo na kuepuka kuingiwa na tamaa ambayo inaweza ikasababisha kuwafarakanisha wanachama.

Mwenyekiti wa UWT Mkoa wa Mbeya, Edna Mwaigomole alisema waliitisha kikao hicho cha baraza kama sehemu ya utekelezaji wa maagizo ya chama mkoa ambayo yalitolewa hivi karibuni ya kuhakikisha wanapokea taarifa ya utekelezaji wa ilani.

Alisema kikao hicho kilitakiwa kiwe kimeshafanyika muda mrefu lakini ratiba zilikuwa zinaingiliana na hivyo wakachelewa kukifanya.

Naibu Waziri wa Habari na Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Maryprisca Mahundi alinunua vitabu vya kanuni za UWT na kuvigawa kwa wajumbe kwa lengo la kuvisoma ili kuondoa migongano kwenye utekelezaji wa majukumu.

Kwa upande wake, Suma Fyandomo alisema katika kipindi cha miezi sita ametumia zaidi ya Sh. milioni 30 kwa ajili ya kuimarisha jumuia na miradi katika wilaya zote.

# 31% ya Watanzania wameunganishwa na intanenti

**Na Gwamaka Alipipi**

IDADI ya Watanzania waliounganishwa na huduma ya intanenti kwa sasa imefikia asilimia 31, kati ya hao asilimia nane ndiyo wanatumia mitandao ya kijamii.

Hivyo, mamlaka za serikali zimetakiwa kushusha kodi za intanenti ili idadi ya watumiaji iongezeke, ufanyaji wa biashara ufanyike zaidi.

Hayo yameelezwa na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Smart Africa Group, Edwin Bruno, wakati wa mjadala katika mtandao wa X uliokuwa mada isemayo 'Ipi nafasi ya huduma za intaneti katika maendeleo ya nchi'.

Akichangia mada katika mada hiyo, Bruno alisema Intaneti ni kama barabara inayounganisha watu, akitolea mfano kwamba zamani ili uende sehemu ni lazima utumie barabara lakini hivi sasa watu wanatumia simu kuwasiliana na kufika popote kupitia intanenti.

"Hivi sasa Watanzania milioni 67 wamejiunga na mitandao ya simu, asilimia 21 wanatumia huduma ya intaneti na asilimia 31 wamekuwa connected (wameunganishwa). Hivyo ni sehemu muhimu ya kufanya biashata na kutengeneza ajira na kuongeza pato la taifa".

Alisema uchumi wa nchi unakuzwa na ajira hali inayochangia ongezeko la maendeleo ya nchi na hatimaye pato la taifa nalo linaongezeka.

Hivyo, alizishauri mamlaka zilizopo zihakikishe kodi za huduma za intanenti zinashuka ili watu wengi wajiunge zaidi na ufanyaji wa biashara ufanyike.

Mkurugenzi wa Utafiti wa Taasisi ya Maendeleo ya Elimu Aga Khan Afrika Mashariki, Dk. Fredick Mtenzi, alisema kwa sasa Tanzania inatakiwa kuwekeza katika kufundisha watu namna ya kutumia teknolojia.

Alisema elimu imekuwa ikitolewa kwa miaka mingi, mafanikio yameonekana lakini matumizi ya teknolojia hususani matumizi ya intanenti yamekuwa yapo chini.

"Lakini inapokuja teknolojia inabadilisha namna elimu inavyotolewa, kutoa nafasi ya kushiriki kwa wananchi wengi. Tunapokwenda na kuwafikia watu wengi ni lazima uhakikishe hawa watu wanauelewa vizuri," alisema Dk. Mtenzi.

Alisema intanenti ina nafasi kubwa katika elimu, hivyo lazima Tanzania iwekeze kwa watu wake ili waweze kufundisha.

Dk. Mtenzi alisema kuna changamoto kubwa wakati wa kufundisha kwa kutumia teknolojia, hivyo ni lazima watu wafundishwe namna ya kutumia teknolojia hiyo.

Alisema: "Tukiwa na watu wenye uelewa mchango wa intanenti itakuwa na mchango mkubwa katika uchumi wetu".

Naye Mkurugenzi wa Mipango na Uhandisi kutoka Kampuni ya simu ya Tigo, Semvua Kisenge, alisema: "Intanet imepitia hatua mbalimbali hadi inafikia sasa".

Alisema kuna mafanikio mbalimbali yaliyopatikana kutokana na matumizi ya huduma ya intanenti ikiwemo watu kupata taarifa za afya, uchumi na elimu, kufundishia shuleni, kufanya biashara, pamoja na kupata mawasiliano ya kijamii.

"Sisi watoa huduma tunatengeneza mazingira wezeshi ili kuhakikisha mtumiaji wa mwisho anafikiwa na kufanya maendeleo yake. Tumepitia teknonolojia mbalimbali na sasa tupo 5G hii inamsaidia mtu kufanya shughuli zake za kila siku," alisema Kisenge. Alisema matumizi ya intanenti imewezesha mambo kuwa rahisi katika nyanja mbalimbali, akisema Tigo wanashirikiana na serikali kuhakikisha huduma hiyo inafika maeneo yote nchini hususani vijijini kupitia UCSAF.

Alisema kupitia matumizi ya intanenti huduma za kifedha, kijamii zimerahishwa ambapo kila mtu anaweza kuzifikia kwa urahisi.

# Mbaroni tuhuma kujifanya ofisa usalama wa taifa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

JESHI la Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja limesema limemkamata mkazi wa Mbweni, Marco Daud Zagamba (32) kwa tuhuma za kujiita mtumishi kutoka Idara ya Usalama wa Taifa (TISS).

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa mjini Magharibi Unguja, ACP Abubakar Khamis Ally, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari Ofisini kwake Mwembe Madema Mjini Unguja.

Alisema mtuhumiwa huyo aliwatapeli wananchi watano na kujipatia Sh. milioni sita kwa njia ya udanganyifu kwenye matukio tofauti ya kuwaahidi ajira.

Alisema Julai 22 mwaka huu eneo la Maisara Zanzibar, mtuhumiwa huyo alimtapeli mwananchi Sh. milioni 1.4 akidai yeye ni mtumishi wa TISS na kwamba atamsaidia kumpatia ajira kwenye idara hiyo, huku akijua kuwa kufanya hivyo ni kosa.


Alisema kwa kutumia mbinu hiyo mtuhumiwa alijipatia Sh. milioni 4.6 kutoka kwa wananchi wanne wakazi wa Zanzibar kwenye matukio mengine taofauti ya utapeli ya kuwaahidi ajira.

"Kwa nyakati tofauti alijifanya yeye ni mtumishi wa umma na kwamba atawasaidia kuwapatia ajira za vikosi maalum vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar" alisema.

Aidha, alisema kuwa mtuhumiwa huyo amefanya matukio ya utapeli kwa muda mrefu akitumia mbinu ya kuwa karibu na ofisi za serikali ili kuwaaminisha anaowatapeli kuwa ni mtumishi wa taasisi hizo na anapofanikisha utapeli huo hutoweka.

"Kuna wakati alifika hapa Madema katika maeneo ya nje na kufanya vikao na wananchi ili kuaminisha kuwa yeye ni ofisa usalama, pia mavazi aliyotumia yalishawishi watu kumuamini" alisema

Kamanda Aboubakary aliwataka wananchi waliopatwa na kadhia ya kutapeliwa, wafike Kituo cha Polisi Madema ili kumtambua mtuhumiwa huyo.



Naibu Kamishna wa Bima Tanzania, Khadija Said (katikati) akipokea zawadi maalum kutoka kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), Joseph Meza (kulia) na Mkurugenzi Mwendeshaji wa Benki hiyo, Arafat Haji, wakati wa utambulisho wa huduma ya bima kupitia benki (Bancassurance), mjini Zanzibar juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mgeni ukiingia Zanzibar, bima ya wasafiri inakuhusu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Saada Mkuya Salum amesema uwepo wa bima ya wasafiri kutaongeza kasi ya idadi ya watalii kufika Zanzibar na serikali kupata mapato yatokanayo na sekta ya utalii.

Aliyasema hayo jana wakati wa utambulisho wa bima hiyo kutoka kwa wadau wa sekta ya usafiri.

Alisema Serikali ya Zanzibar inatarajia kuweka bima ya wasafiri kwa wageni wanaofika Zanzibar ambapo bima hiyo itaanza rasmi mwanzoni mwa Septemba mwaka huu.

Alisema serikali inaendelea na kukamilisha taratibu ya bima hiyo ambao itasimamiwa na Shirika la Bima Zanzibar na itasiadia kuhudumia wageni.

Aidha, alisema pia serikali inaendelea kuboresha miundombinu yao ya kiuchumi pamoja na mifumo ili kuhakikisha wanatoa huduma bora wa wananchi pamoja na wageni.

Hivyo, alisema serikali itajitahidi kuweka miundombinu ambayo itahakikisha wananchi na wageni wanapata huduma bora na wanaendelea na mchakato kuona mambo yao yanakuwa mazuri ili watakapoanza kutumia huduma hiyo kuwe hakuna changamoto.

Kaimu Mkurugenzi wa Shirika la Bima Zanzibar (ZIC), Jape Ussi Khamis, alisema uwepo wa bima hiyo itachangia utalii kuwa mzuri na Zanzibar kuwa salama kwa watalii wanaoitembelea.

Alisema kuwa serikali inatengeneza mambo mengi mazuri kwa ajili ya uchumi wa Zanzibar na miongoni mwa suala ambalo linachangia kwa kiasi kikubwa ukuaji wa uchumi ni sekta ya utalii.

Meneja Biashara, Benki, Bima, Mawakala na Mauzo kutoka ZIC, Hamida Salim Juma alisema bima ya usaifri ni sawa na bima nyingine ambazo mgeni ataipata akiwa nchini na itaukuza uchumi wao na kuupa tija.

Alisema bima hiyo haitatumika katika masuala ya kiafya pekee bali itatumika kwa majanga yote ambayo watakuwa wanapata wageni hao wakiwa nchini au katika mipaka ya Tanzania.

Alisema utaratibu wa kupata bima hiyo utaanzia tangu mgeni huyo atakapoomba kufika Zanzibar.

MCB BANK BETTER TOGETHER

# MWALIMU COMMERCIAL BANK PLC

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

### Imetolewa chini ya kanuni ya 7 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

| WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 JUNI 2024 (Kiasi kwa shilingi milioni) | Robo Mwaka ya sasa 30-Juni-2024 | Robo Mwaka iliyopita 31-Mach-2024 |
|---|---|---|
| **A. MALI:** | | |
| 1. Fedha Taslimu | 638 | 727 |
| 2. Salio katika Benki Kuu ya Tanzania | 14,436 | 8,601 |
| 3. Uwekezaji katika Amana za Serikali | - | - |
| 4. Salio katika Benki nyingine na Taasisi za fedha | 360 | 224 |
| 5. Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 3 | 16 |
| 6. Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7. Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8. Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9. Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 260 | 5,236 |
| 10. Uwekezaji katika Amana Nyingine | - | - |
| 11. Mikopo Halisi Iliyopo | 60,687 | 63,003 |
| 12. Mali Nyingine | 2,391 | 3,061 |
| 13. Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14. Akaunti za udhamini | - | - |
| 15. Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 1,421 | 1,002 |
| **16. JUMLA YA MALI** | **80,196** | **81,869** |
| **B. DHIMA:** | | |
| 17. Amana za Benki nyingine na Taasisi za fedha | 2,000 | 3,900 |
| 18. Amana za Wateja | 55,194 | 50,679 |
| 19. Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20. Amana Maalumu | - | - |
| 21. Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22. Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23. Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 2,372 | 2,808 |
| 24. Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25. Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 3,665 | 5,945 |
| 26. Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo nyingine Zitakazolipwa Baadae | 268 | 182 |
| 27. Dhima Nyingine | 847 | 2,515 |
| 28. Madeni | - | - |
| **29. JUMLA YA DHIMA** | **64,346** | **66,030** |
| **30. MALI/(DHIMA) HALISI** | **15,850** | **15,839** |
| **C. FEDHA ZA WANAHISA:** | | |
| 31. Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 30,912 | 30,912 |
| 32. Akiba ya Mtaji | 114 | 114 |
| 33. Mapato Yaliyobakizwa | (20,400) | (20,400) |
| 34. Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 223 | 213 |
| 35 Akaunti Nyingine za Mtaji (Mtaji tangulizi) | 5,000 | 5,000 |
| 36. Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37. JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **15,850** | **15,839** |
| **38. DHIMA ZISIZO DHAHIRI** | | |
| 39. Mikopo Chechefu | 1,191 | 1,271 |
| 40. Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | (913) | (813) |
| 41 Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| **D. BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| - Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 19.8% | 19.3% |
| - Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 1.9% | 2.0% |
| - Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 104.5% | 113.9% |
| - Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 74.5% | 76.0% |
| - Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 76.0% | 83.4% |
| - Ongezeko la Amana | 4.8% | -13.6% |
| - Ongezeko la Mali | -2.0% | 0.4% |

| TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA ULIOISHIA 30 JUNI 2024 (Kiasi kwa shilingi milioni) | Robo Mwaka ya sasa 30-Juni-2024 | Robo Mwaka iliyopita 31-Machi-2024 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Juni-2024 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 30-Juni-2023 |
|---|---|---|---|---|
| **I. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| Mapato (Hasara) Halisi | 54 | 228 | 282 | 206 |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - | - | - |
| - Hasara katika Mali | 349 | 96 | 445 | 622 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | 4,735 | 2,138 | 6,873 | 3,004 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 14,503 | (10,124) | 4,379 | 3,324 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (12,856) | 8,558 | (4,298) | 1,841 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (27) | 719 | 692 | (2,080) |
| - Kodi Iliyolipwa | (44) | - | (59) | (34) |
| - Mengineyo | (60) | 70 | 10 | (91) |
| **Fedha Halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **6,654** | **1,685** | **8,325** | **6,792** |
| **II. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | - | - | - | - |
| - Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| - Ununuzi wa Mali za Kudumu | (338) | (209) | (547) | (116) |
| - Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| - Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| - Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| - Mengineyo | - | - | - | - |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa(zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(338)** | **(209)** | **(547)** | **(116)** |
| **III. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | - | - | - | - |
| - Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| - Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| - Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| - Gawio Lililolipwa kwa Fedha taslimu | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| - Mengineyo | - | - | - | - |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za Kifedha** | **-** | **-** | **-** | **-** |
| **IV. Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | - | - | - | - |
| - Ongezeko / Punguzo Halisi katika Fedha Taslimu na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu | 546 | 5,200 | 5,746 | 6,676 |
| - Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 5,200 | 4,128 | 9,328 | 6,051 |
| - Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 5,746 | 9,328 | 15,074 | 12,727 |

| TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 JUNI 2024(Kiasi kwa shilingi milioni) | Mtaji wa Hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Ziada ya Kisheria | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 30,912 | (20,400) | 5,000 | 114 | 15,626 |
| Faida (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | 223 | - | - | 223 |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **30,912** | **(20,177)** | **5,000** | **114** | **15,849** |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | |
| Balance as at the beginning of the year | 30,912 | (20,254) | 5,000 | 17 | 15,675 |
| Profit for the year | - | 11 | - | - | 11 |
| Provision General reserve | - | (97) | - | 97 | - |
| Other | - | (60) | - | - | (60) |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **30,912** | **(20,400)** | **5,000** | **114** | **15,626** |

| TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 JUNI 2024 (Kiasi kwa shilingi milioni) | Robo ya Mwaka ya sasa 30-Juni-2024 | Robo ya mwaka Linganishi 30-Juni-2023 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Juni-2024 | Limbikizo la Mwaka linganishi 30-Juni-2023 |
|---|---|---|---|---|
| 1. Mapato ya Riba | 2,539 | 2,516 | 5,143 | 5,187 |
| 2. Gharama za Riba | 1,187 | 1,090 | 2,351 | 2,092 |
| **3. Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2)** | **1,352** | **1,426** | **2,792** | **3,095** |
| 4. Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5. Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 100 | - | 251 | 79 |
| 6. Mapata Yasiyo ya Riba: | 457 | 495 | 933 | 877 |
| 6.1 Faida (Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za kigeni | (9) | 0 | (9) | 0 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 439 | 450 | 888 | 787 |
| 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | 27 | 45 | 54 | 90 |
| 7. Gharama Zisizo za Riba | 1,655 | 1,865 | 3,192 | 3,687 |
| 7.1 Mishahara na Mafao | 740 | 810 | 1,433 | 1,616 |
| 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| 7.3 Gharama Nyingine | 915 | 1,055 | 1,759 | 2,071 |
| **8. Faida (Hasara) ya Uendeshaji** | **54** | **56** | **282** | **206** |
| 9. Tengo la Kodi ya Mapato | 44 | 34 | 59 | 34 |
| **10. Faida (Hasara) Halisi Baada ya kodi ya Mapato** | **10** | **22** | **223** | **172** |
| 11. Mapato Mengine Yaliyojumuishwa | - | - | - | - |
| **12. Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **10** | **22** | **223** | **172** |
| 13. Idadi ya Waajiriwa | 73 | 59 | 68 | 58 |
| 14. Mapato kwa Hisa | 1 | 1 | 5 | 3 |
| 15. Idadi ya Matawi | 2 | 2 | 2 | 2 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| - Uwiano wa Faida kabla ya Kodi ya Mapato na Wastani wa Mali | 0.0% | 0.0% | 0.3% | 0.2% |
| - Uwiano wa Faida baada ya kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 0.1% | 0.1% | 1.4% | 1.1% |
| - Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 91.5% | 97.1% | 85.7% | 92.8% |
| - Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 2.2% | 2.1% | 4.6% | 4.7% |

## BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 JUNI 2024

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Richard L. Makungwa (Ofisa Mtendaji Mkuu) | ......................... (Imesainiwa) | 23 Julai 2024 |
| Mussa Mwachaga (Mkuu wa Fedha) | ......................... (Imesainiwa) | 23 Julai 2024 |
| Joanitha Mashulano (Mkaguzi Mkuu wa Ndani) | ......................... (Imesainiwa) | 23 Julai 2024 |

**Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya sheria ya benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.**

| Jina | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| 1/ Francis Ramadhani (Mwenyekiti) | ......................... (Imesainiwa) | 23 Julai 2024 |
| 2/ Berthasia L. Patrick (Mkurugenzi) | ......................... (Imesainiwa) | 23 Julai 2024 |

## MINIMUM DISCLOSURE OF CHARGES AND FEES MADE UNDER REGULATION 11

| | | |
|---|---|---|
| **Corporate Current Account** | Monthly Account Mainatance fee | TZS 13,000 |
| | Min Opening Balance | TZS 50,000 |
| | Mini Operating Balance | TZS 0 |
| | Counter Cash withdrawal fees | TZS 2,500 for amounts below TZS 5mln, else 0.1% max 100k |
| | Cheque book | TZS 500 per leaf |
| | | |
| **Club/NGO current Account** | Monthly Account Mainatance fee | free |
| | Min Opening Balance | TZS 50,000 |
| | Mini Operating Balance | TZS 0 |
| | Counter Cash withdrawal fees | TZS 2,500 for amounts below TZS 5mln, else 0.1% max 100k |
| | Cheque book | TZS 500 per leaf |
| | | |
| **Foreign Currency Current Account (US$/£/EURO)** | Monthly Account Mainatance fee | USD 12 |
| | Min Opening balance | USD 100 |
| | Min Operating balance | USD 50 |
| | Cheque book | US$ 0.3 per leaf |
| | Counter Cash withdrawal fees | 0.2% of the amount, minimum USD 1, Max USD 100 |
| **Akiba Yangu (TZS Only)** | Monthly Account Maintanance fee | TZS 1,000 |
| | Min Opening balance | TZS 5,000 |
| | Min Operating balance | TZS 10,000 |
| | Counter Cash withdrawal fees | TZS 2,500 for amounts below TZS 5mln, else 0.1% max 100k |
| | Credit Interest | No credit interest |
| | | |
| **Child Savings Account** | Monthly Fee | Free |
| | Min Opening balance | TZS 5,000 |
| | Min Operating balance | TZS 2,000 |
| | Counter Cash withdrawal fees | TZS 2,500 for amounts below TZS 5mln, else 0.1% max 100k |
| | Credit Interest | 1.50% (0 – 100k) , 2.50% (100k – 1mln) , 4% (Above 1 mln) |
| | | |
| **Mwalimu Transactional Account** | Monthly Account Mainatance fee | TZS 1,000 |
| | Min Opening balance | TZS 15,000 |
| | Min Operating balance | TZS 10,000 |
| | Counter Cash withdrawal fees | TZS 2,500 for amounts below TZS 5mln, else 0.1% max 100k |
| | Credit Interest | No credit interest |
| | | |
| **Career Account** | Monthly Account Mainatance fee | Free |
| | Min Opening balance | Free |
| | Min Operating balance | TZS 0 |
| | Counter Cash withdrawal fees | TZS 2,500 for amounts below TZS 5mln, else 0.1% max 100k |
| | Debit Card | Free |
| | | |
| **Tukutane Januari** | Monthly Account Mainatance fee | Free |
| | Min Opening balance | TZS 5,000 |
| | Counter Cash withdrawal fees | TZS 2,500 for amounts below TZS 5mln, else 0.1% max 100k |
| | Credit Interest | 4% pa |
| | | |
| **Student Account** | Monthly Account Mainatance fee | Free |
| | Min Opening balance | TZ10,000 |
| | Min Operating balance | TZS 10,000 |
| | Counter Cash withdrawal fees | TZS 2,500 for amounts below TZS 5mln, else 0.1% max 100k |
| | Credit Interest | 1.00% (0 – 100k), 1.50% (100k – 500k), 2.50% ( Above 500k) |
| | | |
| **Tunu Account** | Monthly Account Mainatance fee | Free |
| | Min Opening balance | Free |
| | Min Operating balance | TZS 10,000 |
| | Counter Cash withdrawal fees | TZS 2,500 for amounts below TZS 5mln, else 0.1% max 100k |
| | Credit Interest | TZS 0.5%(0-500K), 1.5%(500K-1m), 2%(1m-10m), 4%(10m-100m), 5%( >100m) |
| | | USD 0.005%(0-100M) |
| | | |
| **Mtaji Account** | Monthly Account Mainatance fee | Free |
| | Min Opening balance | Free |
| | Min Operating balance | TZS 5,000 |
| | Counter Cash withdrawal fees | TZS 2,500 for amounts below TZS 5mln, else 0.1% max 100k |
| | Credit Interest | 0.5%(0-500K), 1.5%(500K-1m), 2%(1m-10m), 4%(10m-100m), 5%( >100m) |
| **Fixed Deposits** | Negotiable depending on Amount and tenure | |

**MwalimuWakala**

| Transaction Type | Range of Amount | Tariff to Customer (Inclusive of VAT & Excise duty) |
|---|---|---|
| | 1,000 - 4,900 | TZS 500 |
| Cash withdrawals | 5,000 - 9,999 | TZS 750 |
| | 10,000 - 19,999 | TZS 1,000 |
| | 20,000 - 29,999 | TZS 1,500 |
| | 30,000 - 49,999 | TZS 2,000 |
| | 50,000 - 99,999 | TZS 2,500 |
| | 100,000 - 149,999 | TZS 3,000 |
| | 150,000 - 299,999 | TZS 3,500 |
| | 300,000 - 499,999 | TZS 4,000 |
| | 500,000 - 699,999 | TZS 5,000 |
| | 700,000 - 899,999 | TZS 6,000 |
| | 900,000 - 999,999 | TZS 6,500 |
| | 1,000,000 - 1,999,999 | TZS 7,000 |
| | 2,000,000 - 2,999,999 | TZS 8,000 |
| | 3,000,000 - 3,999,999 | TZS 9,000 |
| Balance Enquiry | | TZS 500 |
| Mini statement | | TZS 500 |

***MwalimuMobile***

| Transaction Type | Range of Amount | Tariff to Customer (Inclusive of VAT & Excise duty) |
|---|---|---|
| Balance Inquiry | | TZS 300 |
| Mini Statement | | TZS 500 |
| Fund Transfers (Intra Bank) | | TZS 300 |
| Fund Transfers (Inter Bank) | | TZS 1,300 within UMOJA BANKS, and TZS 10,000 to other banks |
| GEPG-Excluding LUKU | | TZS 1,000 |
| Fund Transfers (Bank to wallet/Vodacom, Tigo, Airtel) | 1,000 - 4,999 | TZS 1,000 |
| | 5,000 - 9,999 | TZS 1,500 |
| | 10,000 - 49,999 | TZS 2,000 |
| | 50,000 - 99,999 | TZS 2,500 |
| | 100,000 - 299,999 | TZS 3,000 |
| | 300,000 - 499,999 | TZS 3,500 |
| | 500,000 - 699,999 | TZS 4,000 |
| | 700,000 - 899,999 | TZS 5,000 |
| | 900,000 - 999,999 | TZS 6,000 |
| | 1,000,000 - 1,499,999] Gold | TZS 8,000 |
| | 1,500,000 - 3,000,000] class | TZS 11,000 |

**MwalimuCard VISA Tariff**

| TRANSACTION FEES | Band | TARIFF TO CUSTOMER |
|---|---|---|
| Cash withdrawal at Umoja ATMs | 1,000 - 99,999 | TZS 1,500 |
| | 100,000 - 400,000 | TZS 1,700 |
| Cash withdrawal Domestic (Out of Umoja ATMs) | | TZS 3,000 |
| Cash withdrawal international | | TZS 7,500 |
| Balance Enquiry | | TZS 700 |
| Merchant & Online Payment | | Free |

| Mwalimu Personal Loan | CHARGES/FEES |
|---|---|
| | Interest rates = 16% |
| | Loan Application Fee = 3% |
| | Life insurance = 0.50% |
| **MSME Loans** | |
| | Interest rates = 22.8% (+/-) |
| | Loan Application Fee = 3% |
| | Life insurance = 0.50% |
| **Personal Loans** | |
| | Interest rates = 16% |
| | Loan Application Fee = 3% |
| | Life insurance = 0.5% |
| **Wastaafu Loan** | |
| | Interest rates = 14% |
| | Facility fees : 1 % |
| | Administration & Life insurance = 1% |
| **Mlinde Mstaafu** | |
| | Interest rates = 14% |
| | Facility fees : 1 %. |
| | Administration & Life insurance = 1% |
| **Plot Loan** | |
| | Interest rates = 17% |
| | Loan Application Fee = 3% |
| | Life insurance = 0.5% |
| **Insurance Premium Financing (IPF)** | |
| | Interest rates = 18% |
| | Loan processing fee 3% |
| **Jenga na MwalimuBank** | |
| | Interest rates = 16% |
| | Loan Application Fee = 3% |
| | Life insurance = 0.5% |
| **Bank Guarantees (off-balance sheet)** | |
| | Commision=1.5% quarterly |
| **Ada chap chap** | |
| | Interest rates = 3.5% per month |
| | Loan Application Fee = 3% |
| | Life insurance = 0.5% |
| **Salary Advance** | |
| | Interest rates = 5% |
| **Mwalimu Jikimu** | |
| | Interest rates = 18% |
| | Loan Application Fee = 3% |
| | Life insurance = 0.5% |

**General Fees and Commissions**

| Statement | CHARGES/FEES |
|---|---|
| **Duplicate Statement** | TZS 2500 per page for more than a month |
| | FREE for current 1 month statement |
| **Cheques** | |
| Bankers Cheque - Customer | TZS 30,000/US$16 |
| Bankers Cheque - Non Customer | TZS 55,000/US$30 |
| | |
| **TISS & EFT charges:** | |
| Outward EFT | TZS 2,000 |
| Internal Transfers | TZS 800 per item |
| Outgoing TISS | TZS 2,000 for amount up to TZS 10mln, TZS 5,000 for amount up to TZS 50mln, TZS 10,000 for amount higher than TZS 50mln |
| | |
| **Standing Order** | |
| Standing orders (within the same bank) | Free |
| Standing orders (to other banks)@Transfer | TZS 12,000 per transfer |
| | |
| **Mwalimucard VISA** | |
| MwalimuCard VISA Issuance fee | TZS 10,000 |
| Replacement *MwalimuCard* (faulty) | Free |
| Replacement *MwalimuCard* (Expiry) | TZS 10,000 |
| Replacement *MwalimuCard* (Lost) | TZS 20,000 |
| Pin re-issuance/replacement for *MwalimuCard* | TZS 5,000 |
| *MwalimuCard* VISA Monthly Maintenance fee | 1500 Monthly |

**ATM - Cash Withdrawal fees**

| Transaction Type | Band | Tariff to Customer (Inclusive of VAT & Excise duty) |
|---|---|---|
| Cash withdrawal at Umoja ATMs | 1,000 - 99,999 | TZS 1,500 |
| | 100,000 - 400,000 | TZS 1,700 |
| ATM Withdrawal from other domestic Banks | | TZS 3,000 |
| ATM Withdrawal from outside Tanzania | | TZS 7,500 |
| ATM Balance Enquiry Domestic | | TZS 700 |
| | | |
| **Cheque** | | |
| Returned Cheque - Insufficient fund | | TZS 100,000 |
| Stop Payment orders | | TZS 40,000 |
| Inward Cheques | | free |
| counter cheque | | TZS 6,000 |
| | | |
| **Others** | | |
| Cash deposit | | Free |
| Dormant Account Activation | | Free |
| Closing Account | | Free |
| Monthly dormant Account charge | | Free |
| Bulk cash Deposit/ Same day deposited above TZS 30M | | Free |
| Bulk cash Deposit/ Same day deposited above USD 50K | | Free |
| Mutilated note deposit | | Free |
| Certificate of balance | | TZS 40,000 |
| Loan balance letter | | TZS 25,000 |
| Letter of introduction/Comfort | | TZS 80,000.00/USD 50 |
| Audit confirmation | | TZS 40,000/USD 40 |
| School fees deposits | | Free |
| TRA collection | | Free |
| Company Search to BRELA | | TZS 22,000 for limited Company and TZS 2,000 for sole proprietor |
| Cash deposit - small denomination ($1,5,10 and $20) | | 0.60% |
| Retrieval of Document | | TZS 5,000 Per Item |
| | | |
| **Documents Search fees(Electronic & Hard copies)** | | |
| Less than 30 days | | Tzs 20,000.00 per item |
| More than 30 days , but less than a year | | Tzs 50,000.00 per item |
| Above One year | | Tzs 70,000.00 per item |

| Product Name | Transaction Type | CHARGES/FEES |
|---|---|---|
| **Personal Current Accout (TZS Only)** | Monthly Account Mainatance fee | TZS 8,200 |
| | Min Opening balance | TZS 50,000 |
| | Min Operating balance | TZS 10,000 |
| | Counter Cash withdrawal fees | TZS 2,500 for amounts below TZS 5mln, else 0.1% max 100k |
| | Cheque book | TZS 500 per leaf |

## HABARI KIMATAIFA/KITAIFA

# Kamala Harris akabiliwa mtihani vita Gaza

**WASHINGTON,** Marekani

MAKAMU wa Rais wa Marekani, Kamala Harris, ambaye anapambana kuteuliwa mgombea wa chama cha Democrat, anakabiliwa na mtihani mgumu kuhusu vita ya Gaza.

Harris anajulikana kuwa na msimamo wa kati kuhusu kinachoendelea Ukanda wa Gaza, anasubiriwa kutoa kauli yake ambayo inaweza kubadilisha sera ya Marekani kwa Israel.

Makamu huyo wa rais ambaye amepata nafasi hiyo baada ya Rais Joe Biden, kujiengua katika kinyang'anyiro, atalazimika kuwashawishi wakosoaji wa sera hiyo ambayo inapingwa na vijana na wafuasi wengi wanaoiunga mkono Palestina.

Harris yuko kwenye kampeni ya kupata uteuzi wa Chama chake cha Democratic amepambanua kuwa haungi mkono katika pande zote zinazopigana kati ya Israel na Hamas.

**Wachambuzi wanaeleza kuwashawishi baadhi ya wapiga kura itakuwa moja ya changamoto kuu inayomkabili Harris ikiwa anataka kuboresha nafasi yake dhidi ya mgombea wa Republican, Donald Trump.**

Katika kikao cha Bunge la Congress, makamu huyo wa rais hakuhudhuria wakati wa Waziri Mkuu wa Israel, Benyamin Netanyahu, alipowahutubia wabunge.

Timu yake ya kampeni ilikuwa ikikimbizana na muda, lakini kwa wanachama wengi wa Democratic, wanaona dalili hiyo ni mabadiliko ya wazi ya kisera dhidi ya taifa hilo la Mashariki ya kati.

Baadhi ya wachambuzi, wanasema hiyo inaonyesha wasiwasi wake kuhusu vita hiyo inayosababisha vifo vya raia. Kumekuwa na mgawanyiko ndani ya chama cha Democratic kuhusu sera ya taifa hilo, ambao ulionekana kuwa karibu sana na Waisraeli na kupuuza hali mbaya inayowakabili Wapalestina.

Kamala Harris kwa sasa anaonekana kuungwa mkono na watu wenye sauti katika chama chake, huku kampeni yake ikiendelea kukusanya zaidi ya dola milioni 100 tangu Joe Biden ajiondoe.

Wademocratic wengi wanajitahidi kuonyesha ushirikiano wenye mashaka hasa linapokuja suala la msaada kwa Israeli na kukemea maovu yanayoendelea Gaza.

Hata hivyo, makamu huyo wa rais atalazimika kuwashawishi wapiga kura, haswa wale waliomkataa Biden kwa sababu ya sera yake kwa Israeli.

Mwezi Machi, Harris alitoa maoni makali kutoka kwa ofisa wake wa utawala, alipotaka makubaliano ya kusitisha mapigano kumalizavita yafanyike kwa kile alichokiita "mateso makubwa" wanayowakabili Wapalestina na kuikosoa Israeli kwa kutotoa misaada ya kutosha.

Wachambuzi wanaeleza kuwashawishi baadhi ya wapiga kura itakuwa moja ya changamoto kuu inayomkabili Harris ikiwa anataka kuboresha nafasi yake dhidi ya mgombea wa Republican, Donald Trump.

Majimbo muhimu kama Michigan na Minnesota, ambayo yana idadi kubwa ya Waarabu na Waislamu yamekuwa yakilengwa katika kumuongezea kura ya ushindi.

Wakati huo huo, Rais wa Marekani Joe Biden, amesema uamuzi wake wa kuacha kugombea muhula wa pili unatokana na kulazimika kuunganisha Chama cha Democratic kabla ya uchaguzi wa urais uliopangwa kufanyika mwezi wa Novemba mwaka huu.

"Katika wiki za hivi karibuni, imedhihirika kwangu kwamba ni lazima niunganishe chama changu katika shughuli hii muhimu," alisema katika Biden katika hotuba yake nzito aliyeitoa jana.

Alisema kwamba wakati ulikuwa umefika wa kusikia sauti mpya ya vijana.

**HATIMAYE**

"Imekuwa heshima ya maisha yangu kuwa rais wenu, lakini utetezi wa demokrasia, ambao uko hatarini, nadhani ni muhimu zaidi kuliko cheo chochote," alisema kiongozi huyo mwenye umri wa miaka 81.

Alimsifia Harris kwa kumwita mshirika wa ajabu kwake, kiongozi wa nchi na aliwaambia ni juu yao Wamarekani kuchagua. **RFI**

# Afungwa jela kwa kuingiliwa kinyume na maumbile

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

MAHAKAMA ya Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara imemhukumu kifungo cha miaka 20 jela Mwalimu Justine Milanzi (39) kwa kosa la kuingiliwa kinyume cha maumbile.

Milanzi ambaye ni mlemavu asiyeona na mwalimu wa Shule ya Msingi Sabasaba katika Halmashauri ya Mji wa Masasi, alikutwa na hatia hiyo baada ya Mahakam kujiridhisha kuwa alifanya kitendo hicho kwa kuruhusu kuingiliwa kinyume cha maumbile na mwanafunzi wake mwenye umri wa miaka 12) (jina la linahifadhiwa).

Katika hukumu hiyo, ilielezwa kuwa mshtakiwa amekutwa na hatia, hivyo kuhukumiwa kifungo hicho cha miaka 20 jela baada ya mahakama kujiridhisha na ushahidi wa upande wa Jamhuri.

Mwalimu huyo alihukumiwa kwa mujibu wa kifungu cha 138 c (1) & 2 (b) cha Kanuni ya Sheria ya Adhabu Sura 16 Toleo 2022

Kesi hiyo Na. 108/2023 iliyofunguliwa Novemba 21, 2023 na mama mzazi wa mtoto huyo, ilisomeka kuwa ya shambulio la kingono kwa kuruhusu kuingiliwa kinyume cha maumbile.

Ilidaiwa na upande wa mashtaka kuwa tukio hilo la shambulio la kingono lilifanyika Oktoba 17, 2023 maeneo ya Kisiwani, Masasi mkoani Mtwara ambako mshtakiwa huyo anaishi.

Kabla ya hukumu hiyo, Mwendesha Mashtaka wa Jamhuri, Haji Kajiru, aliiomba mahakama kutoa adhabu kali Kwa mshtakiwa ili kutoa fundisho kwa watu wengine wanaofanya vitendo hivyo.



Watu wakichimba kifusi kuopoa maiti ya mwathiriwa wa maporomoko ya udongo yaliyotokea juzi katika eneo la Gofa, kusini mwa Ethiopia. **PICHA: REUTERS**

# Walimu, wanafunzi kortini wizi wa mitihani

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WALIMU watatu na wanafunzi wawili wa Shule ya Sekondari Lunguya, Halmshauri ya Msalala mkoani Shinyanga, wamepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Wilaya ya Kahama kwa madai ya wizi wa mitihani ya kidato cha nne iliyofanyika Novemba, 2023.

Washtakiwa hao ni mwalimu Ovan Katunzi (54), Jacob Daniel (36), Ramson Kanyenyemo (35), wanafunzi Lucy Maganda (39) ambaye pia ni muuguzi Paschal Buchanagandi (21) ambao walikuwa wanarudia mitihani.

Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Jukael Jairo, alidai kuwa washtakiwa hao walitenda kosa la kuvujisha mitihani ya kidato cha nne iliyofanyika Novemba, 2023 kinyume cha Sheria ya Baraza la Mitihani Sura Namba 107 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2019.

Alidai kuwa shtaka hilo lina makosa matatu la kwanza likiwahusu wanafunzi wawili ambao walikuwa wakirudia mtihani huo waliokutwa na nyaraka zisizoruhusiwa kwenye chumba cha mtihani kinyume na vifungu cha namba 20 (2) na 24 (1)(2) vya Sheria ya Baraza la Mitihani.

Alidai kuwa kosa la pili linawahusu walimu watatu wa shule hiyo wanaodaiwa kuvujisha mtihani wa somo la Jiografia kwa wanafunzi wakati mitihani ikiendelea kinyume cha Sheria ya Baraza la Mitihani.

Kosa la tatu, alidai linamhusu Mwalimu Katunzi kwa kushindwa kutunza au kulinda karatasi za majibu ya mtihani wa Jiografia.

Mwendesha mashtaka alidai kuwa upelelezi wa shauri hilo umekamilika, hivyo kuiomba mahakama kupanga tarehe kwa ajili ya kusikilizwa.

Baada ya kusomewa mashtaka hayo, washtakiwa wote watano walikana mashtaka dhidi yao lakini walishindwa kukidhi masharti ya dhamana na kurejeshwa mahabusu kusubiri shauri hilo litakapotajwa.

Kabla ya kuahirisha shauri hilo, Hakimu Mkazi Christina Chovenye, alitaja masharti ya dhamana kwa washitakiwa wote ambayo ni kuwa na wadhamini wawili, mmoja akiwa mtumishi wa umma, wakiwa na kitambulisho cha taifa (NIDA) na bondi ya thamani ya Sh. milioni tano, ambayo walishindwa kuyatimiza.

Hakimu Chovenye aliahirisha shauri hilo hadi Agosti 7, mwaka huu, kwa ajili ya washtakiwa kusomewa maelezo ya awali na kupokea ushahidi na mashahidi.

# NADO ATAKA MATAJI MSIMU UJAO AZAM FC

Na Adam Fungamwango

WINGA wa Azam FC, Idd Suleiman 'Nado', amesema amepania kuipa kombe lolote timu yake ya Azam msimu ujao kwani itakuwa ni aibu kutoka kapa kutokana na ubora wa kikosi chao.

Akizungumza akiwa nchini Morocco ambako yupo na kikosi cha timu hiyo kwenye maandalizi ya msimu ujao, Nado alisema kwa sasa yupo fiti kupigania namba na kupambania timu yake kutwaa kombe likiwamo la ubingwa wa Tanzania Bara kwani wana uwezo huo na haiwezekani watoke kapa kama msimu uliopita.

**Aidha, alisema kuwa msimu uliopita alisumbuliwa na majeraha yaliyomfanya akae muda mrefu bila kucheza kiasi cha kusahaulika na mashabiki wengi kwani awali walikuwa wakimuona akifunga mabao katika mechi kubwa ambazo Azam imekuwa ikicheza dhidi ya Simba au Yanga.**

"Kuelekea msimu ujao nimejiandaa vizuri sana na ninaendelea kujiandaa, najua ushindani wa ndani utakuwa mkubwa lakini hilo tunamuachia mwalimu.

"Inabidi na mimi nijitoe kimasomaso ninyanyue kidogo makwapa msimu ujao kwani ni aibu. Hata hivyo, siyo kwamba sijawahi kuchukua makombe huku kwenye ndondo nishachukua sana, Manzese, Temeke wapi, nishachukua sana. Hivyo, msimu ujao nataka ninyanyue Kombe la Ubingwa wa Ligi Kuu, au Kombe la FA nikiwa na Azam kwani haiwezekani kwa kikosi kama hiki tutoke kapa kabisa hata taji moja tusipate," alisema mchezaji huyo ambaye kipaji chake kiliibuliwa kutoka michuano ya mchangani maarufu kama Ndondo Cup.

Alisema tatizo lililomkabili msimu uliopita limeisha na amekuwa akifanya mazoezi ya maandalizi ya msimu kwa bidii kubwa ili kukamilisha alilolipanga.

"Msimu uliopita niliandamwa na majeruhi na sikufanya vizuri ikiwemo kutokufunga kwenye mechi kubwa kwani mimi huwa naonekana sana kwenye mechi kubwa, msimu huu unaokuja hebu tuone, ila nimejipanga vizuri hivyo chochote kinaweza kutokea kitu kikubwa zaidi ya nilivyokuwa nafanya huko nyuma", alisema Nado.



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Michezo, Sanaa na Utamaduni, Suleiman Serera akirusha mpira wa kikapu na kufunga goli kuashiria uzinduzi wa viwanja vitatu vya michezo ambavyo ni cha kikapu, soka na netiboli vilivyojengwa kwa ufadhili wa kampuni ya Alliance One(AOTL) kwenye Shule ya Msingi Kingolwira Manispaa ya Morogoro. Wengine pichani ni Mkurugenzi wa Manispaa ya Mogororo Emmanuel Mkongo (wa pili kulia), Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa AOTL, Blasius Lupenza (wa pili kulia) na Msemaji wa kampuni hiyo Wakili John Magoti (wa tatu kulia). **MPIGAPICHA WETU**

# *Wacheza gofu kuchuana Agosti 3, Lugalo*

Na Shufaa Lyimo

WACHEZAJI wa mchezo wa gofu wanatarajia kuoneshana kazi Agosti 3 kwenye mashindano ya wazi yatakayofanyika kwenye viwanja vya Lugalo jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, Mwenyekiti wa Klabu ya Gofu ya Lugalo, Brigedia Jenerali Mstaafu, Michael Luwongo alisema shindano hilo litashirikisha wachezaji 150 kutoka nchi mbalimbali.

Mwenyekiti huyo alisema lengo ni kutumia mashindano hayo kutafuta wachezaji wanne ambao wataenda kushiriki mashindano ya kimataifa jijini Nairobi, Desemba mwaka huu.

"Maandalizi kuelekea kwenye shindano hilo la wazi yanaendelea vizuri ambapo mpaka sasa tunaendelea kuboresha miundo mbinu ya viwanja vyetu ili shindano lifanyike kwa weledi na ushindani mkubwa," alisema Luwongo.

Alisema baada ya kukamilika kwa shindano hilo wachezaji wanne watakaowapata watakwenda kupeperusha bendera ya Tanzania kwenye mashindano hayo ya kimataifa.

Aidha, aliipongeza Benki ya KCB kutokana na udhamini wao katika shindano hilo na kuwataka wale ambao hawajathibitisha ushiriki wao wathibitishe haraka iwezekanavyo kwa kuwa muda umekwisha.

Kwa upande wake, Mkurugenzi KCB, Cosmas Kimario, alisema benki huyo amekuwa akisaidiana na wanajamii katika kuendeleza michezo mbalimbali ikiwemo riadha, mpira wa miguu, ngumi pamoja na gofu. Aliweka wazi kuwa wameamua kuwekeza katika michezo kwa lengo la kukuza vipaji vya vijana wadogo wanaochipukia kwenye michezo hiyo.

Aidha, kwa upande wake nahodha wa klabu hiyo, Meja Japhet Masai, alisema shindano hilo litachezwa kwa mtindo wa kuhesabu mashimo kwa pointi ambapo atakayepata pointi nyingi ataibuka mshindi.

## Ditto kukata rufaa kupinga hukumu

Na Mwandishi Wetu

MWANAMUZIKI wa kizazi kipya, Lameck Ditto ameamua kukata rufaa kupinga hukumu ya kesi ya madai dhidi ya kampuni ya 'Multchoice Tanzania Limited' maarufu DSTV.

Ditto ambaye jina lake halisi ni Dotto Bwakeya alifungua kesi ya madai Mahakama Kuu kanda ya Dar es Salaam mwaka 2020 akiomba iamuru kampuni hiyo imlipe fidia ya Shilingi bilioni sita kwa kutumia wimbo wa 'Nchi Yangu' aliodai ni wake kwenye matangazo yao ya biashara bila ridhaa yake wakati wa kampeni za fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) mwaka 2019.

Pia, aliiomba mahakama iamuru alipwe milioni 200 kutokana na madhara ya jumla,vilevile alipwe riba ya asilimia 25 tangu siku alipofungua shauri hilo akidai kampuni hiyo imemnyima fursa ya kunufaika na kazi yake.

Naibu Msajili wa Mahakama hiyo, Mery Moyo alisoma hukumu hiyo juzi Julai 23, 2024, ambapo hukumu iliyotolewa na Jaji Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Salma Maghimbi ambaye hakuwepo mahakamani juzi.

Moyo ambaye alisema amepewa jukumu la kuisoma tu hukumu hiyo, alisema mahakama imeshindwa kumtia hatia mdaiwa kwa kuwa wimbo uliotumiwa unaolalamikiwa siyo orijino ambao Ditto ndiye mmiliki.

Moyo alianza kusoma hukumu hiyo iliyokuwa na kurasa 10 kwa kueleza imetolewa na Jaji Maghimbi na yeye amepewa kuisoma tu na kuanza kwa kueleza kwamba katika uumbaji Mungu ametoa karama mbalimbali ambazo ndiyo chanzo cha kipato na mali.

Alifafanua maana ya haki miliki akisema ni neno la kisheria linalotumika kutafsiri haki ya anayetengeneza kazi fulani akizichanganua kazi hizo ikiwamo ya muziki na kuendelea kwa kusema.

Nje ya Mahakama hiyo, Ditto alisema hakubaliani na hukumu iliyotolewa na anachokisubiri ni nakala ya hukumu ili akae na wanasheria wake na kufanya uamuzi mwingine wa kukata rufaa nyingine.

"Uamuzi uliotolewa umenishangaza, kama mahakama inasema wimbo orijino ni wangu, ambapo mtuhumiwa ametumia second version (toleo la pili) ambao tulifanya kwenye urithi festival (tamasha la urithi) hivyo, imeshindwa kumtia hatiani mshitakiwa kwa kuwa alitumia version ya pili, hiyo version ya pili ni ya nani?," alisema Ditto kwa uchungu.

## ZISIKUPITE

### GALLAGHER KUTUA ATLETICO

KLABU ya Atletico Madrid ina imani kubwa kupata dili la kumsaini kiungo wa kati wa Chelsea na England, Conor Gallagher mwenye umri wa miaka 24. ***(Team Talk)***

### C'PALACE KUMNUNUA SARR

CRYSTAL Palace inafikiria kumnunua winga wa Marseille na Senegal, Ismaila Sarr mwenye umri wa miaka 26. ***(Standard)***

### INTER YAMTAKA KIWIOR

INTER Milan inatumaini kuwa harakati za Arsenal kumnunua mlinzi wa Bologna na Italia, Riccardo Calafiori, 22, zitawalazimisha kumuuza mlinzi wa Poland, Jakub Kiwior, 24, ambaye wanamtaka. ***(Standard)***

### HJULMAND ATAKIWA MAN U

KLABU ya Manchester United inafikiria kumnunua kiungo wa kati wa Denmark, Morten Hjulmand, 25, kutoka Sporting Lisbon. ***(FootballTransfers)***

### AKARIBIA CHELSEA

CHELSEA inakaribia kukamilisha dili la kumnunua mlinda mlango wa Villarreal na Denmark chini ya umri wa miaka 21, Filip Jorgensen, ambaye pia amevutiwa na Marseille. ***(Athletic)***

### ALEXANDER ATAKA KUBAKI

MCHEZAJI Alexander-Arnold, 25, anataka kusalia na Liverpool licha ya beki huyo wa pembeni wa England kuivutia Real Madrid. ***(Mail )***

### APERRIBAY AKANUSHA

RAIS wa Real Sociedad, Jokin Aperribay amekanusha kuwa kuna mazungumzo yoyote yanayoendelea na Liverpool kuhusu uwezekano wa kumnunua winga wa Japan, Takefusa Kubo, 23. ***(Mundo Deportivo)***

### THIAW KUNUNULIWA

KLABU ya Newcastle United ina nia ya kutaka kumnunua beki wa AC Milan na Ujerumani, Malick Thiaw, 22, kwa takriban pauni milioni 35. ***(Times)***

### ROWE KUBAKISHWA

KLABU ya Fulham itatoa ofa iliyoboreshwa kwa mchezaji wa Arsenal, Emile Smith Rowe, 23. The Cottagers hao na Crystal Palace zote ziliwasilisha ombi la kutaka kumnunua kiungo huyo Mwingereza lililokataliwa na Washikabunduki hao mwezi huu. ***(Sky Sport)***

### NELSON AGOMBEWA

KLABU ya Leicester City inashindana na West Ham kumnunua winga wa Arsenal, Reiss Nelson, 24. ***(Times)***

### NKETIAH KUUZWA

ARSENAL iko tayari kusikiliza ofa za kumuuza mshambuliaji wa Uingereza, Eddie Nketiah, huku Marseille wakiibuka kama mahali pazuri pa kumuuza mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25. ***(Mirror)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# MANCHESTER UNITED YATAFUTA BEKI MPYA

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United imeongeza kasi ya kutafuta mlinzi mpya wa pembeni, chanzo kiliiambia ESPN, huku Tyrell Malacia akitarajiwa kuachwa nje.

**Malacia hajacheza kwa zaidi ya mwaka mmoja kwa sababu ya jeraha la goti.**

Kulikuwa na matumaini angeweza kurejea mazoezini msimu huu wa majira ya joto lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, ambaye aliichezea United mara ya mwisho Mei 2023, aliondolewa kwenye kikosi kilichosafiri kwenda Los Angeles Jumatano huku akiendelea kujiuguza kule Carrington.

Taarifa kwenye tovuti ya klabu hiyo ilisema, "Tyrell Malacia hayupo kwenye kikosi huku akiendelea na matibabu yake kutokana na jeraha chini ya uongozi wa madaktari huko Carrington."

Upungufu wa mabeki wa kushoto msimu uliopita ukichangiwa na majeraha ya Luke Shaw, uliishawishi United kumsajili Sergio Reguilón kwa mkataba wa muda mfupi msimu uliopita.

Erik ten Hag pia alilazimika kutumia chaguzi za dharura Victor Lindelöf na Sofyan Amrabat.

Shaw pia atakosa ziara ya Marekani baada ya kuichezea England kwenye Euro 2024 akiwaacha United ikiwa na Harry Amass mwenye umri wa miaka 17 na Sam Murray mwenye miaka 19 kama mabeki pekee wa kushoto wanaotambulika katika mechi dhidi ya Arsenal, Real Betis na Liverpool.

Chanzo kiliiambia ESPN kwamba klabu inaangalia chaguzi za beki wa kushoto wakati wa dirisha la majira ya joto ili kuzuia kujirudia kwa shida ambazo ziliisumbua msimu uliopita.

United pia wanaangalia mabeki wa kulia ikiwa wanaweza kupata klabu ya kufikia thamani ya pauni milioni 20 kwa Aaron Wan-Bissaka ambaye ameingia mwaka wa mwisho wa mkataba wake Old Trafford.

Diogo Dalot, Bruno Fernandes, Alejandro Garnacho, Kobbie Mainoo, Lisandro Martínez, Facundo Pellistri na Altay Bayindir pia watakosa ziara ya Marekani baada ya kuongezewa mapumziko kufuatia michuano ya Ulaya na Copa América.

Wakati huo huo, United wametangaza kwamba Rasmus Højlund amechukua jezi namba 9.

Nambari hiyo ambayo awali ilikuwa ikivaliwa na Zlatan Ibrahimovic na Romelu Lukaku, iliachwa na Anthony Martial baada ya Mfaransa huyo kuihama klabu hiyo mwishoni mwa msimu uliopita.

**●●● Klabu hiyo imeongeza kasi baada ya kuumia kwa Malacia ambaye...**

HABARI MICHEZO

# DE GEA AFIKIRIA OFA 3 KUREJEA KWENYE SOKA



**MADRID,** Hispania

DAVID de Gea hatimaye anakaribia kurejea kwenye soka ikiwa ni zaidi ya mwaka mmoja baada ya mkataba wake na Manchester United kumalizika na kuihama klabu hiyo akiwa kama mchezaji huru.

Akiwa na umri wa miaka 33, De Gea bado ana nafasi ya kucheza kama kipa lakini kuondoka kwake United baada ya misimu 11 kulimfanya akose timu. Mhispania huyo hakupungukiwa na ofa msimu uliopita wa majira ya joto lakini alipinga mvuto wa Saudia kwa matumaini ya kupata timu yenye ushindani barani Ulaya.

Ilibadilika kuwa msimu mzima nje ya mchezo, ambao De Gea alitumia wakati wa mapumziko kujishughulisha na vitu vya kufurahisha na masilahi ya nje ya biashara, na vile vile kujiweka sawa na kuzingatia mazoezi binafsi nyumbani.

Sasa anatazamiwa kufanya uamuzi ambao utamrudisha kwenye soka.

Emoji yake ambayo De Gea alichapisha kwenye mtandao wa X Jumamosi iliyopita iliitazamwa mara milioni kumi, ilipendwa mara 87,000.

Kwa mujibu wa gazeti la The Athletic, kurejea kwake katika soka sasa kunaweza kuzingatiwa kuwa ni karibu, kwa ofa kutoka Saudi Arabia, Marekani na Italia.

"Wiki ijayo" ni muda uliotolewa wa sasisho linalotarajiwa uamuzi wa mwisho unapofanywa.

Lakini hakuna mapendekezo kutoka kwa nchi yake ya Hispania, huku De Gea akionekana kutotaka kuchezea klabu yoyote ya England isipokuwa United. De Gea alibaki akiishi nyumbani kwake katika viunga vya matajiri vya Manchester alipoondoka United.

Hata baada ya kuhamia Hispania, ambapo mke wake Edurne ni mwanamuziki maarufu na mtangazaji wa televisheni, alikuwa amerejea kaskazini magharibi mwa Uingereza kwa vipindi vyake vya mazoezi huko Altrincham.

Hata inadaiwa kwamba angerejea Old Trafford ikiwa hali zingekuwa tofauti. Ikiwa itakuwa Marekani, inasemekana kwamba De Gea angependelea kuelekea pwani ya magharibi.

# Mascherano ashangazwa na vioja Olimpiki

**ST-ETIENNE,** Mfaransa

KOCHA wa Argentina, Javier Mascherano alisema hajawahi kushuhudia 'sarakasi' kama iliyotokea wakati wakifungwa 2-1 na Morocco katika mechi yao ya kwanza ya mchezo ya Olimpiki mjini St-Etienne Jumatano.

Cristian Medina alidhani ameokoa sare ya 2-2 kwa Argentina alipofunga dakika za majeruhi, lakini bao hilo lilikataliwa na VAR kuwa ameotea wakati mchezo ulianza kwa dakika chache baada ya kusimama kwa saa mbili na kuwaondoa mashabiki uwanjani.

Mascherano alisema kumekuwa na ukosefu wa mawasiliano kutoka kwa waandaaji kuhusu kitakachotokea wakati timu hiyo ilipokaa kwenye chumba cha kubadilishia nguo cha Geoffroy Guichard kabla ya kuanza tena.

"Siwezi kueleza kilichotokea. Tulitumia takriban saa moja na nusu kwenye chumba cha kubadilishia nguo ambapo hawakuwahi kutuambia kitakachotokea," alisema Mascherano akiwaambia waandishi wa habari.

"Morocco hawakutaka kucheza, hatukutaka kuendelea, na mashabiki walitushia vitu. Ni sarakasi kubwa kuwahi kuona maishani mwangu. Sijui kwanini walitumia saa moja na dakika 20 za kukagua mchezo.

"Kama kuna kuotea kwenye bao la Madina acha mchezo uendelee kwa kasi tuliyonayo, sidhani kama mchezo unapaswa kuchezwa kwa dakika tatu baada ya saa moja na nusu."

Hata hivyo, kiungo huyo wa zamani wa safu ya ulinzi ya Argentina alisema hataki kujiingiza katika kulalamika kupindukia na ameihimiza timu yake kuangazia mechi zao zijazo za Kundi B dhidi ya Iraq na Ukraine.

Argentina itamenyana na Iraq mjini Lyon Jumamosi.

## KUPOTELEWA NA CHETI



**NAUMI SAMSON MWASHIWAWA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S1932-0025 kilichotolewa na **SANTILYA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2013. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MWE/RB/2072/2024.**

## KUPOTELEWA NA CHETI



**KELVIN JOHN SAMWEL** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S1278-0111** kilichotolewa na **MBEZI SECONDARY SCHOOL** mwaka 2022. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/UBU/153622/2024.**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**
**SHAURI LA LA MADAI NAMBARI 65 LA 2024**
**EDITH GEORGE MHEHE…MUOMBAJI/WAOMBAJI**
**DHIDI YA**
**ASWAMADU ABDUL SWAMADU…MDAIWA/WADAIWA**
**WITO KUITWA SHAURINI**
**ASWAMADU ABDUL SWAMADU**
**POPOTE ULIPO/MLIPO**

EDITH GEORGE MHEHE amefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumb lililopo Kinondoni (Mwananyamala). Shauri husika limepangwa kutajwa tarehe 02/09/2024 saa 03:00 asubuhi/mchana mbele ya Mh. J.W. SILLAS hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.

Imetolewa na kutiwa Saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 25 Mwezi 07…2024.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MWANZA**
**SHAURI LA MAOMBI YA MADAI NAMBA 4076 LA MWAKA 2024**

**RAIDEN YAKOBO KINANGE @ ZAKAYO ATHANAS RAIMOND…….MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

**MAGWEIGA CHACHA MAGERE……….MJIBU MAOMBI**

**KUITWA SHAURINI**

UNAJULISHWA KWAMBA SHAURI TAJWA HAPO JUU LIMEPANGWA KUSIKILIZWA NA MAHAKAMA HII TAREHE 05/08/2024, UNATAKIWA KUHUDHURIA WEWE BINAFSI AU WAKILI WAKO KISHERIA.
ZINGATIA KWAMBA KUTOKUFIKA KWAKO KWA TAREHE TAJWA, KESI HII ITAENDELEA KUSIKILIZWA BILA WEWE KUWEPO MAHAKAMANI NA KUTOLEWA MAAMUZI.

HATI HII IMETOLEWA KWA MKONO WANGU NA MUHURI WA MAHAKAMA HII LEO TAREHE 16/07/2024

**NAIBU MSAJILI**

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**SHABANI MBWANA JUMA anatangaza kupotelewa na kadi zake za pikipiki kama zifuatavyo:-**
MC 104 DMY aina ya TVS yenye chassis Na. MD625AE31M1KOO414

MC 769 DEW aina ya HUONIAO yenye chassis Na. G7EPCJL02MA010539

MC 469 CZR aina ya HUONIAO yenye chassis Na. LJEPCJL02MA007002

MC 524 CZC aina ya HUONIAO yenye chassis Na. LJEPCJL04MA006823

Yeyote atakayeziona anaombwa atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/TAN/TAN/7591/2024**

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**SHABANI MBWANA JUMA anatangaza kupotelewa na kadi zake za pikipiki kama zifuatavyo:-**

MC 799 CNC aina ya TVS yenye chassis **Na. MD625AF73L1A00590**

MC 290 CQK aina ya HUONIAO yenye chassis **Na. G7EPCJL04LA004496**

MC 624 CTK aina ya HUONIAO yenye chassis **Na. LJEPCJL03LA007928**

MC 895 CTU aina ya HUONIAO yenye chassis **Na. G7EPCJL00LA009808**

Yeyote atakayeziona anaombwa atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/TAN/TAN/7589/2024**

**FOMU MADAI -3**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo Wilaya ya Moshi Kituo cha Moshi Mjini Mkoa KILIMANJARO.**
**Shauri la Ndoa 122, 2024.**
**Jina la Mdai HELLEN LONGDARE MOLLEL.**
**Jina la Mdaiwa BARAKA ELIMO SARIA .**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**Kwa BARAKA ELIMO SARIA.**

Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta /Wameleta madai yake/ yao kwamba (eleza hapa habari za Madai ) **Fika Mahakamani kujibu madai ya Tsh 4,500,000/=ulizoazimwa na mdai mnamo tarehe 04/12/2023 kwa makubaliano ya kurejesha ndani ya mwezi mmoja .**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 29 mwezi 07 mwaka 2024 saa 6:00 Mchana kwa mujibu wa Mwombaji hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashaidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini,Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya w ewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 22 mwezi 07 Mwaka 2024

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA MWANGA**
**UTHIBITISHO NA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**SHAURI LA MIRATHI NA 14567 YA MWAKA 2024**
**MAOMBI YA BARUA YA USIMAMIAJI WA MIRATHI YA**
**MARIA MICHAEL JOSEPH…………MAREHEMU**
**SHABANI ZUBERI SHABANI…MUOMBAJI**
**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua ya usimamiaji wa mirathi kwa muombaji aliyeomba hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikwa mnamo au kabla ya tarehe 29 Mwezi Julai, Mwaka 2024.

Imewasilishwa Mwanga leo tarehe 22 Mwezi Julai Mwaka 2024.

## KUPOTELEWA NA CHETI



**ASTERIA FREDRICK LUKONGE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba P1261-0008 kilichotolewa na **MERIWA SEKONDARY** SCHOOL mwaka 2011. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DOD/DOD/31558/2024.**

HABARI MICHEZO

## Gamondi afurahishwa ushindani wa namba

INATOKA UK. 24

wabao 1-0, Gamondi, alisema kilikuwa kipimo kizuri kwao.

"Kila mchezaji aliyepata nafasi alionesha kitu, ulikuwa mchezo mzuri na nimefuruhishwa na kile wachezaji wangu walichokifanya hivyo tunaendelea kujenga timu yetu," alisema Gamondi.




Yanga wanatarajia kucheza mchezo mwingine wa michuano ya Kombe la Toyota dhidi ya Kaizer Chief kabla ya kurejea nchini kwa ajili ya tamasha la 'Wiki ya Mwananchi' litakalofanyika Agosti 4.

## Golikipa awatoa hofu mashabiki Simba

INATOKA UK. 24

ndani anacheza na kuelekeza, hana mambo mengi, tunajivunia kuwa naye na tunaomba Mungu abaki kwa muda mrefu kuendelea kuifundisha Simba," alisema kipa huyo.

Alisema kwa msimu mmoja aliojiunga na Simba amejifunza vitu vingi ambayo awali alikuwa havifahamu, hivyo kwake ni somo kubwa.

"Nilijisikia faraja kuingia Simba, nilikaa na wachezaji wakubwa wenye uzoefu akina Aishi Manula, Shomari Kapombe, Mohamed Hussein 'Tshabalala', ambao wamenipa ujasiri mkubwa ingawa haukuwa msimu mzuri kwetu, hata hivyo sijacheza mechi za kimataifa lakini ile kuwapo tu kwenye timu ambayo inacheza mechi hizo nimejifunzaa vitu vingi ambavyo nilikuwa sivifahamu kabla. Kusema kweli ukicheza hizi timu kubwa ni shule tosha," alisema Abel.

Akiizungumzia idara ya makipa, amewahakikisha wanachama na mashabiki kutokuwa na wasiwasi kwani mafunzo wanayoyapata ni ya hali ya juu na ni bora pia.

# SERIKALI YAKABIDHIWA VIWANJA VIPYA VITATU

**Na Gwamaka Alipipi**

SERIKALI imepokea msaada wa viwanja vitatu vya michezo vilivyojengwa katika Shule ya Msingi Kingolwira mkoani Morogoro.

**Akipokea msaada huo, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Sanaa, Utamaduni na Michezo, Suleiman Serera alisema viwanja alivyokabidhiwa ni cha mpira wa miguu, mpira wa pete na mpira wa kikapu ambavyo vimejengwa na kampuni ya tumbaku ya Alliance One (AOTL) kwa gharama ya Shilingi milioni 241.**

"Msaada huu unaenda sambamba na Sera ya Taifa ya Michezo ya Mwaka 1995 pamoja na maelekezo ya Rais Samia ya kufanya kazi kwa karibu na taasisi binafsi katika kuwaletea wananchi maendeleo," alisema.

Alisema msaada huo unaendana na mpango wa serikali wa kujenga miundombinu ya viwanja kwenye shule 56 nchini. Lengo likiwa ni kuweka mazingira bora ya michezo kwa watoto wa shule za msingi na sekondari.

Aidha, Serera aliishukuru kampuni hiyo kwa ujenzi wa viwanja hivyo ambavyo vitasaidia kuboresha mazingira yatakayosaidia kuibua vipaji vya watoto mashuleni.

Aidha, alisema viwanja hivyo vimejengwa kwa hadhi ya kimataifa na kwamba vimewekewa miundombinu ya maji ya umwagiliaji majani ili yasikauke.

"Niwapongeze sana Alliance One kwa ufadhili huu kwani natambua kwamba ziko taasisi nyingi ambazo zinapata faida na zinafanya mambo mengi na hawarudishi fadhila ipasavyo kwa jamii kama ninyi mlivyofanya kwani kutoa ni moyo wala siyo utajiri," alisema.

Msemaji wa kampuni hiyo, John Magoti alisema wametoa msaada huo kupitia sera yao ya misaada kwa jamii.

Aliendelea kuelezea kuwa, gharama za ujenzi wa viwanja hivyo umegharimu Sh. milioni 241, fedha ambazo zimelipwa kwa mkandarasi mzawa ambaye amefanya kazi kwa wakati.

"Tumetoa msaada huu tunaoukabidhi leo lengo likiwa ni kuendeleza michezo kwa watoto kwani tunaamini kwamba baada ya masomo ya darasani, kuna umuhimu kwa watoto kuwajengea watoto afya ya akili kupitia michezo ya aina mbalimbali inayochezwa kwenye mazingira mazuri," alisema.

Akipokea msaada huo, Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro, Emmanuel Mkongo, aliipongeza kampuni hiyo kwa msaada wa viwanja hivyo huku akiahidi kuvitunza.

Aidha, Kaimu Mkurugenzi wa Aliance One, Blasius Lupenza alisema misaada wanayoitoa kwenye shule hiyo ni ya ujirani mwema na wamekuwa wakiifanya kwa miaka mingi.



Wachezaji wa soka wa kituo cha michezo cha Jakaya Kikwete wakiwania mpira walipokuwa wakifaya mzoezi katika uwanja wa Kituo hicho jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Waziri Junior atua Dodoma Jiji FC*

**Na Adam Fungamwango**

KATIKA kile kinachoonekana kujiimarisha kuelekea msimu ujao wa Ligi Kuu, klabu ya Dodoma Jiji imeendelea kufanya usajili wa kishindo ambapo jana mchana ilimtambulisha mshambuliaji wa KMC na timu ya Taifa ya Tanzania, Waziri Junior.

Taarifa iliyotolewa jana na Idara ya Habari na Mawasiliano ya klabu hiyo, inasema kuwa mchezaji huyo amesaini mkataba wa kuichezea timu hiyo yenye makao yake jijini Dodoma kwa miaka miwili, ambapo mategemeo yao ni kuwa na kikosi bora cha msimu ujao kitakacho himili mikimiki ya msimu.

"Tumepata mali safi, ni Waziri ambaye atakuwa mmoja wa wachezaji wetu wapya watakaounda kikosi chetu kuelekea msimu ujao,"ilisema sehemu ya taarifa ya klabu hiyo.

Waziri, ambaye amekabidhiwa jezi namba 10 kwenye timu hiyo, ataungana na wachezaji maarufu ambao Dodoma Jiji imefanikiwa kupata saini zao kuelekea msimu ujao ambao ni straika mwenzake, Reliants Lusajo aliyesajiliwa kutoka Mashujaa FC na Ibrahim Ajibu kiungo mshambuliaji wa zamani wa timu za Simba na Yanga, lakini akitokea klabu ya Coastal Union aliyokuwa akichezea msimu uliopita.

Straika huyo alipachika mabao 12 msimu uliopita na kuongoza kwa ufungaji mabao Ligi Kuu msimu wa 2023/24 kwa upande wa washambuliaji asilia kwani waliokuwa juu yake ni Feisal Salum wa Azam FC aliyefunga mabao 19 na Stephane Aziz Ki wa Yanga aliyetwaa kiatu cha dhahabu kwa kufunga mabao 21 wote ni viungo.

Mbali na KMC alikotoka, straika huyo amewahi kuzichezea klabu za Toto African, Azam FC, Biashara United, Mbao FC, Yanga na hatimaye timu aliyocheza msimu uliopita inayomilikiwa na Manispaa ya Kinondoni, KMC.

Wachezaji wengine wapya ambao wametua Dodoma Jiji FC ni kipa mahiri raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Allain Ngeleka ambaye aliibeba Kagera Sugar msimu uliopita, Dickson Mhilu pia kutoka Kagera Sugar na beki Daudi Milandu kutoka Tabora United.

# Michezo

Ijumaa Julai 26, 2024

Nipashe



Diaby atimkia Saudia

UKURASA 22



Kiungo wa Yanga, Max Nzengeli (kushoto) akiwatoka wachezaji wa TX Galaxy kwenye mchezo wao wa kirafiki juzi nchini Afrika Kusini. Yanga ilishinda bao 1-0. **PICHA: MTANDAO**

# Gamondi afurahishwa ushindani namba Yanga

**Na Faustine Feliciane**

## Ajivunia usajili wao wa kimkakati, aweka wazi malengo ya msimu ujao ambao ni...

KOCHA wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema ushindani wa namba uliopo sasa ndani ya klabu hiyo umeleta matokeo chanya kuelekea msimu mpya wa ligi na mashindano ya kimataifa.

**Miguel, amesema usajili waliofanya msimu huu utawapa matokeo mazuri kwa sababu kila mchezaji anauwezo mkubwa na anataka kuonesha kitu kila anapopata nafasi ya kucheza.**

"Kumekuwa na ushindani mkubwa kuanzia mazoezini hadi katika mechi za ushindani za kirafiki. Aidha, usajili tulioufanya una manufaa makubwa sana na nina uhakika timu itafanya vizuri sana msimu ujao kwani wachezaji wenye kwa wenyewe wanashindana kuwania namba," alisema Gamondi.

Alisema kuwa maingizo mapya ndani ya kikosi chake yanachochea ushindani kwa asilimia kubwa na ndicho alichokuwa akikitaka kitokee.

"Mathalani, ukiangalia usajili wetu ulikuwa ni wa kimkakati kwelikweli na hatukutaka kuruhusu wachezaji wetu nyota waondoke hiyo tulifanikiwa kuwabakisha. Fauka na hilo, hatukutaka kurizika na kikosi chetu hivyo tukamua tuongeze nguvu kidogo kuleta ushindani, na tumefanya hivyo na matokeo yake tunayaona," alisema.

Alisema malengo yao makubwa ni kuutetea Ubingwa wa Ligi Kuu, Komba la FA na kufika mbali zaidi kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Akizungumzia mchezo wao wa juzi dhidi ya TS Galaxy ambao waliibuka na ushindi

INAENDELEA UKURASA 23

# Golikipa awatoa hofu mashabiki Simba

**Na Adam Fungamwango**

SIKU chache baada ya taarifa ya golikipa namba moja wa klabu ya Simba, Ayoub Lakred kuripotiwa kuumia na kutarajiwa kukaa nje ya uwanja kwa angalau wiki sita, kipa mwingine wa klabu hiyo, Hussein Abel, amewatoa hofu mashabiki wa timu hiyo kwa kusema kipa yeyote ana uwezo wa kuanza kwenye mchezo.

Abel, aliyesajiliwa na Simba msimu uliopita akitokea KMC, amewapa kongole pia makocha wapya wa timu hiyo akisema wana uwezo mkubwa na hawamfokei mchezaji anapokosea bali wanamuelekeza.

Alisema kwa sasa hakuna kuwa na hofu mchezaji mmoja anapokosekana kwa kuwa kila mchezaji ana uwezo mkubwa wa kuanza kikosi cha kwanza.

"Mashabiki wasiwe na hofu, hata kama mchezaji fulani atakuwa hayupo, bado mchezaji mwingine ana uwezo wa kufanya vizuri akipata nafasi," alisema Abel na kuongeza,

"Msimu huu nimefurahi wachezaji wengi waliosajiliwa ni vijana kwa hiyo wapinzani wajipange, wachezaji wamekuja na morali nao wanataka umaarufu, wana hamu ya kutwaa makombe, wana njaa ya mafanikio, hivyo watu wajipange kweli," alitahadharisha kipa huyo ambaye kwa sasa yupo na kikosi cha timu hiyo nchini Misri.

Kuhusu benchi la ufundi linaloongozwa na kocha Faldu Davids, alisema wana ufundishaji wa aina ya pekee unaopendwa sana na wachezaji wengi kwani ni rahisi kuwaelewa.

"Walimu wetu wanajua kufundisha, wanakupa moyo, unapokosea hawakufokei, wanakuelekeza ili usirudie tana kosa ulilofanya.

Halafu watu wasichokijua kocha wetu ni kocha mchezaji, yeye mwenyewe anaingia

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >